# Frimasonri

**Huda Publishers**
**Box 90399**
**Dar es salaam**

# Neno la Awali

Kwa karne kadhaa sasa kumekuwa na hofu, gumzo na minong'ono juu ya mitandao inayoendesha siasa za Ulimwengu kwa siri. Mitandao hiyo ni *Freemansory* na *Mafya* ambayo yote iko chini ya nguvu za uzayuni wa kimataifa. Kitabu hiki kimejaribu kuielezea mitandao hiyo zaidi kikiwa kimejikita katika ule mashuhuri wenye jina la *"Freemasonry"* au kwa utohozi usiyo rasmi *"Frimansori"*. Mtandao huu umejengwa na watu walioamuwa kujitowa muhanga wenye kuzingatiya miiko na tahadhari zote ili kufanikisha lile walilolikusudia. *"Frimansonri"* ni tafsiri inayogeuza kidogo matamshi, inatanguliza n kabla ya s na kisha n. Freemansonry-Frimansori. Katika kitabu hiki tutatumia tafsiri hii pamoja na neno Mafya.

Walimwengu wamekuwa wakiushutumu mtandao wa *"Freemasonri"* kutokana na matendo yake maovu na ya uhalifu. Kwa sababu hiyo *"Frimansori"* ni jina linalochukiza masikiyoni mwa wengi. Hata hivyo, wenye mtandao, badala ya kujibu shutuma, wameendelea kupiga kimya huku wakijitahidi kuupa haiba ya asasi ya kawaida ya kijamii. Wamekuwa makini sana katika kuujenga mtandao huwo ambao sasa unaweza kujitapa kuwa umeweza kudhibiti siyasa na uchumi wa duniya kwa sura mbali mbali. Maudhuwi haya yanajaribu kuiweka wazi sura halisi ya *"Frimansori"*.

Ama Chachu ya umoja wa kimafiya ni ile falsafa yao ambayo yaweza kuelezwa kwa maneno ya Usekula. Umoja wa kimafyoso au Umafya umejengwa kwa falsafa potofu iliyojengwa kwa dhanna zisizo sahihi au nadhariya zenye walakini. Hii ndiyo nukta muhimu ya mwanzo ambayo *"Frimansori"* inakosolewa kwayo. Kwa kutumiya rejeleya kadhaa kutoka kwa waandishi mbali mbali walioandika kuhusu *"Frimansori"* itawekwa bayana hapa kuwa ukosowaji huwo ni muhimu si tu kwa kuwaelimisha watu wasiohusika na shirika hili bali piya kuwapa changamoto wahusika wauone ukweli. Katika hao wapo wanaojuwa malengo ya ndani ya shirika hilo na wapo wasiojuwa lolote zaidi kuhusika ili kujipatiya manufaa ya kibiyashara. Bila shaka Wananchama wa *"Frimansori"* , kama walivyo watu wengine wako huru kujiamulia mambo yao na hivyo wanaweza kufuata mtazamo wowote wautakao Duniyani na wakaishi kwa mujibu wa mtazamo huo. Hii ni haki yao ya kimaumbile. Hata hivyo wengine nao wana haki ya kubainisha makosa yao. Tunazingatia kanuni zilezile za ukosowaji kama tunavyozikosowa jamii nyingine.

Kitabu hiki kinakosowa misingi na malengo ya harakati na shughuli za shirika hili. Piya kwa muhtasari kinaelezeya mapisi ya mapambano ya *"Frimansori"* dhidi ya dini zinazoamini Mungu. Frimansori imetowa mchango mkubwa sana katika hila ya Ulaya kujitowa katika dini na katika kuunda utaratibu mpya wa maisha kwa msingi wa falsafa za kumkana Muumba . Aidha "Frimansori" imeshiriki katika kupandikiza itikadi za kukana Muumba katika jamii zisizokuwa za kimagharibi kupitiya mitalaa ya elimu kwa kuhakikisha inakuwa na watu wake

katika sekta hiyo kila nchi. Kitabu hiki piya kitaelezea mbinu na njama ambazo Mafia, Mazayoni na Mayahudi kwa ujumla wamekuwa wakizitumiya kusaidiya kusimamisha na kudumisha mfumo wa jamii uliojengwa kwa dhana hizi. Inatazamiwa kuwa mambo muhimu yatakayoelezwa katika kitabu hii yatatowa changamoto ambayo kwayo wengi wakiwemo wadau wa shirika hilo wataweza kuuangalia ulimwengu kwa mtazamo sahihi zaidi. Baada ya kusoma kitabu hiki maalumu kwa Walinganiaji wa ujumbe wa Mwenyezi Mungu wataweza kutumia kufakari na kuyachambua mambo mbali mbali yatokeayo ulimwenguni kwa uoni mpana zaidi. Wataelewa misingi na mielekeo ya itikadi za kisiasa, falsafa, utitiri wa vyombo vya habari na hasa yale magazeti yanayoandika na kuachapisha habari na picha za ovyo yaliyojazana mitaani hivi na kubaini malengo yaliyofichikana ndani yake.

# Sura ya kwanza
# Chimbuko la Frimasonri

Ufahamu walionao wanahistoria wengi ni kuwa chimbuko la shirika la *"Frimansori"* ni vita vya msalaba-Crusades, ukweli ni kuwa ingawa shirika hili lilianzishwa na kutambulika rasmi nchini Uingereza mwanzoni mwa karne ya kumi na nane, mizizi yake inaanzia nyuma katika karne ya kumi na mbili. Hata kama baadhi ya watu watang'ang'ania kiyasi gani kuwa vita vya msalaba vilikuwa ni misafara tu ya kijeshi iliyofanywa kwa jina la Ukristo, kimsingi, ilikuwa ni misafara iliyofanywa kwa minajili ya kupata maslahi ya kimali. Katika kipindi ambacho Ulaya ilikuwa ikikabiliwa na umaskini mkubwa na ufukara, mafanikiyo na utajiri wa mashariki ya kati uliwavutia sana wazungu wa Ulaya. Hii ndiyo ilikuwa sababu ya mabadiliko ya ghafla ya Wakristo wa Ulaya kutoka zile sera zao za utulivu na kuingia katika vita vya kijeshi. Mwanzilishi wa vita hivi vya msalaba alikuwa Papa Urban wa pili(Pope Urban II). Papa huyu aliitisha baraza lake, *"Council of Clermont"* mnamo mwaka 1095 ambapo ile itikadi ya awali ya utulivu waliyokuwa nayo Wakristo ikawekwa kando. Vikatangazwa vita vitakatifu kwa hila ya kuzipora nchi takatifu kutoka mikononi mwa Waislamu. Kufuwatia azimio la baraza hilo, Jeshi kubwa la wapiganaji wa vita hivyo likaundwa, likishirikisha askari wenye mafunzo ya kitaalamu na maelfu ya wapiganaji wa kujitolea. Wanahistoria wanaamini kuwa hila ya Papa Urban II ilitokana na tamaa yake ya kupata nafasi ya ugombea katika kinyang'anyiro cha Upapa. Tukumbuke kuwa mfumo wa uongozi wa kikatoliki chini ya Papa unatokana na tabaka la Umwinyi uliowakandamiza watu kwa kisingizio cha Dini.

Wafalme wa Ulaya na Warithi wao waliuafiki wito wa Papa kwa shangwe kumbe malengo yao yalikuwa ya kiduniya kama alivyosema Donald Queller wa Chuo Kikuu cha Illinos, wakuu wa Ufaransa walitaka tu kujiongezeya nchi. Nao wafanyabiashara wa kitaliano walitumai kupanua biyashara katika bandari za mashariki ya kati. Idadi kubwa ya watu masikini wakajiunga na misafara hiyo ili nao wakajikomboe kiuchumi kutokana na hali zao ngumu za maisha. Umati huu wa watu wenye uchu wa mali uliuwa Waislamu wengi na hata Wayahudi kila mahali ulipopita. Kwa sababu tu ya uchu wao wa kujipatia dhahabu na vito vya thamani, wanamgambo hawa wa Crusade walitumbua matumbo ya wale waliowauwa ili wapate dhahabu na madini ya thamani ambayo walidhani wahanga wameyameza kabla ya kufa. Uchu wao wa mali ulikuwa mkubwa mno kiasi kwamba hawakusita kufanya chochote. Baada ya safari ndefu na ngumu ya uporaji mwingi na mauaji makubwa dhidi ya Waislamu, genge hili lililoitwa la Wanamsalaba likafika Jerusalem mnamo mwaka 1099. Baada ya Jiji kuzingirwa kwa karibu majuma matano, Makruseda wakaingia ndani. Walifanya ushenzi makubwa sana. Waislamu na Wayahudi wa Jiji hilo walikatwakatwa mapanga. Mwanahistoria anasema, Waliwaua Waarabu, Waturuki wote waliowakuta humo, Wanaume kwa Wanawake mmoja wa Makruseda hao Raymond akajitapa kwa mauaji haya kwa kusema:

“Baadhi ya watu wetu walikatakata vichwa vya maadui zao, wengine wakawachoma mishale, wengine wakawatesa kwa kuwatupa kwenye moto. Malundo ya vichwa, mikono na miguu, yalionekana katika mitaa ya Jiji. Mtu alilazimika kukanyaga miili ya watu na farasi ili kupita njia. Lakini yote hayo ni madogo kulinganisha na ale yaliyotokea kwenye hekalu la Suleiman, mahali ambapo shughuli za kidini hufanyika. Katika hekalu hilo, watu walipita kwenye madimbwi ya damu, miguu ilizama hadi magotini.”

## Historia ya Matempla

Kwa kifupi Matempla hawakutoweka kabisa bali falsafa yao. Imani zao na ibada zao bado zinaendelea chini ya mwavuli wa Frimansori. Dhana hii inatiwa nguvu za ushahidi mwingi wa kihistoria na hivi leo inakubaliwa na idadi kubwa ya Wanahistoria wa magaharibi ima awe Mafyoso au la. Katika kitabu chetu, *The new Masonic Order*, tumeutathmini kwa kina ushahidi huu. Dhana inayoihusisha mazizi ya Mansori na Matempla, mara nyingi inarejewa katika majarida yanachapishwa na Mansori wenyewe kwa ajili ya Wananchama wao. Wanachama wa Frimansori wanaikubali kabisa dhana hii. Mojawapo ya majarida hayo linaitwa Minnar Sinan(ni jarida la Mafyoso wa Uturuki) ambalo linaelezea uhusiano kati ya komandi ya Matempla na Frimansori kwa maneno yafuatayo”

“Mnamo mwaka 1312, pale Mfalme wa Ufaransa kwa shinikizo la kanisa alipolifunga komandi ya Matempla na mali zao kuwapa askari wa mtakatifu John mjini Jerusalem harakati za matempala hazikukoma. Idadi kubwa ya Matempala wakapata hifadhi katika maskani ya Frimansori iliyokuwepo Ulaya wakati huo. Kiongozi wa Matempla, Mabeignac, akiwa na wanachama wengine, wakapata usalama nchini Scotland chini ya mwavuli wa *Wall builder* na chini ya jina la Mac Benach. Mfalme Scotland Robert the Bruce akawakaribisha na kuwaruhusu kuwa na ushawishi mkubwa katika maskani za Frimansori nchini Scotland. Matokeo yake maskani za Scotland umuhimu mkuibwa kwa mtazamo wao wa kiufundi na fikra zao. Leo hii Mafyoso wanatumia jina la Mac Benach kwa heshima. Mafyoso wa Ufaransa waliorithi vitu vya Matempla wakareje zao Ufaransa miaka mingi baadaye na kuimarisha ngome yao ya kaaida ikijulikana kama kaaida ya Scotland(*Scotish Rights*).

Aidha, Mimar Sinan inatoa habari nyingi kuhusu uhusiano wa Matempla na Mafrimasonri. Katika makala yake iliyokuwa iliyokuwa na kichwa Templas and Frimanson inasema sala ya sherehe za uzinduzi wa Komandi ya Matempla ni sawa kabisa na sala Mafyoso wa zama hizi. Kwa mujibu wa makala hiyo hiyo, kama ilivyo katika Mansori wanachama wa Komandi ya Matempla wakiitana Brother(ndugu). Mwishoni mwa makala hayo tunasoma maneno haya; “komandi ya Matempla na shirika la Frimansoni yanashajiishana, kwa kiasi kikubwa hata sala za mashirika haya zinashabihiana kwa maana zimaigwa kutoka kwa Matempla. Kwa ajili hii, Mafyoso kwa kiasi kikubwa wamejifananisha na Matempla na yaweza

kusemwa kuwa, kile kinachoonwa kuwa ni usiri mkubwa wa Frimansonri kwa kiasi kikubwa kimeigwa kutoka kwa Matempla. Kwa kufupisha hapa ni kuwa, kama tulivyoona twaweza kusema kuwa chanzo cha sanaa za Kifalme na usiri wa Frimansori chatokana na Matempla. Mwisho, tunasema kuwa imetokea huko nyuma kwa Matempla na kwamba Mafyoso wamefuata falsafa ya Komandi ya Matempla. Mafyoso wenyewe wanalikubali hili lakini jambo muhimu kwa tafakuri yetu ni nini asili au chanzo cha falsafa hii. Kwa nini Matempla waliachana na Ukristo na kufuata mafundisho mapya. Kitu gani kilichosababisha wafikiye uamuzi huo? Kwa nini walifanya mageuzi hayo kule Jerusalem na je kupitia tawi hili la Frimansoni kumekuwa na athari gani Duniyani kutokana na Falsafa hii iliyofuatwa na Matempla.

## Matempla na Kaballa

Kitabu kilichoandikwa na Mafyoso Christopher na Robert Lomas kiitwacho *The Hiram Key* kinafichuwa mambo fulani ya kweli kuhusu mizizi ya Frimansori. Kwa mujibu wa Waandishi hawa, ni dhahiri kuwa Frimansori ni mwendelezo wa Matempla. Mbali na hivyo, Waandishi hawa piya, wameviangaliya piya vyanzo vya Matempla. Kulingana na dhanna yao, Matempla walipitia hatua kubwa za mabadiliko wakati walipokuwa Jerusalem. Mahala palipokuwa kwa Ukristo wao walianzisha madhehebu nyingine. Katika mzizi wa mabadiliko haya, kuna siri ambayo waliifichua ambayo ni hekalu la Suleiman pale Jerusalem ambalo mabaki yake, walitaka kuyachunguza. Waandishi hawa wanasema kuwa, Matempla walikuwa wakiutumia ule ulioitwa kuwa wajibu wao wa kulinda mahujaji wa Kikristo waliozuru pale Palestina lakini kumbe hiki kilikuwa kisingizio, lengo halisi lilikuwa jingine kabisa. Hakuna ushahidi kuwa wale Waasisi walikuwa wakitoa ulinzi kwa Mahujaji bali tulichokugundua ni kuwa kuna ushahidi mkubwa kuwa walikuwa wakichimbua chini ya mabaki ya hekalu la Herold. Waandishi wa kitabu cha Hiram Key sio wao pekee waliogundua vielelezo vya jambo hili. Gaetani De la Forge, Mwanahitoria wa Ufaransa naye ametoa maelezo kama haya; “jukumu halisi la Wale wanamgambo tisa wa Krusade walikuwa wakifanya utafiti katika eneo hilo ili kupata masalia na kupata kumbu kumbu za maandiko ya awali ambao yanachimbuko ya maelezo ya siri ya dini ya kiyahudi na Misri ya zama za kale.

Mwisho mwa karne ya 14 Charles Wilson wa Royal Engeneers alianza kufanya utafiti wa mabaki ya kale kule Jerusalem. Yeye akafka mahala pa kuona kuwa, Matempla walikuwa wamekwenda Jerusale kutaifiti mabaki ya hekalu. Wilson aligundua chimba chimba na fukua fukua china ya misingi ya hekalu na akahitimisha kuwa kazi hii ilifanywa kwa zana ambazo zilikuwa za Matempla.

Vifaa hivi vingalipo katika hazina ya mabaki ya kale ya Robert Brydon, ambaye anamiliki hifadhi ya kumbu kumbu zinazohusiana na Matempla. Waandishi wa kitabu cha the

Hiram Key wanadai kuwa chimba chimba ya Matempla haikuishia matupu, kwamba ile Komandi iligundua kumbukumbu fulani pale Jerusalem ambayo ndiyo iliyobadili mtazamo wao. Mbali na hao watafiti wengine nao wana maoni hayo hayo. Yumkini lazima kulikuwa na jambo lililowapelekea Matempla kubadili mfumo wa imani na falsafa yao tafauti na Ukristo licha ya ukweli kuwa hapo awali walikuwa wakristo waliotoa katika nchi ya Kikristo. Kwa mujibu wa fikra za watafiti wengi jambo hili lilikuwa Kaballa.

Maana ya neno Kaballa, ni fasihi simulizi. Maandiko na makamusi yanalifafanua neno hili kama siri kubwa, tawi la siri siri la dini ya Uyahudi. Kwa mujibu wa ainisho hili neno la Kaballa linachukua maana iliyofichikana katika Taurati na maandiko mengine ya dini Uyahudi. Lakini tunapochunguza kwa undani jambo hili tunaona kuwa ukweli wa mambo ni mwingine kabisa. Hakika ya mambo inatuplekea kufikiri hitimisho jingine kuwa Kaballa ni mfumo wenye mizizi ya ushirikina wa kipagani, kwamba ilikuwepo kabla ya Taurati na ilienea ndani ya dini ya Uyahudi hata baada ya kufunuliwa kwa Taurati. Ukweli huu wa kuvutia kuhusu Kaballa unafafanuliwa kuwa ndio chanzo hasa. Murat Orgen, Frimansori wa kituruki yeye anasisitiza yafuatayo katika kitabu chake Masonluk Nedir Ve Nasirdir?(Frimasonri ni nini, ikoje?).

“Hatujui vizuri wapi ilikotokea Kabbalah au namna ilivyojiendeleza ni jina la jumla la falsafa moja ya siri iliyojengwa kwa iami i ya kiroho hasa hasa inayohusiana na dini ya Uyahudi Huu ni Usufi wa dini ya kiyahudi lakini baadhi ya mambo iliyonayo yanaonesha kuwa likusanywa zamani zaidi kabla ya Taurati. Mwanahistoria wa Ufaransa Gougenot Des Mousseaux yeye anasema kuwa, Kaballa ni ya zamani kabla ya Uyahudi.

## Historia ya Matempla

Kwa muda wa siku mbili tu jeshi la msalaba liliwaua kinyama Waislamu wapatao 40,000. baada ya hapo Wanamgambo hao katili wakaifanya Jerusalem kuwa mji wao mkuu na kuanzisha utawala wa Kifalme wa Kilatini ambao ulijitanua kutoka mipaka ya Palestina hadi Antiokia. Baadaye Wapiganaji hao wa vita vya msalaba wakaanzisha mapambano ya kuimarisha utawala wao katika eneo la mashariki ya kati. Wakaanzisha kambi za mafunzo ya kijeshi kwenye majumba kama yale ya kitawa. Washiriki katika mafunzo hayo walitoka Ulaya kuja Palestina na wakaishi katika majumba hayo. Mojawapo ya Komandi zao za kijeshi ilitafautiyana kabisa na nyingine yenyewe ilibadilika muundo kukidhi haja ya wakati. Komandi hii mahususi ilikuwa ya wale walioitwa mashujaa watakatifu yaani Templars. Templar hii au kwa jina kamili, askari dhaifu wa Yesu Kristo na hekalu la Suleiman, iliundwa mwaka 1118, miaka ishirini baada ya wanamgambo wa msalaba kuitwaa Jerusalem. Waanzilishi wa Komandi hii walikuwa ni Wafaransa wawili, Hugh de Payens na Godfrey dest Omer. Mwanzoni kulikuwa na askari lakini Komandi ikazidi kuimarika. Sababu ya wao kujipa jina templar ni kuwa mahali walipochagua kuwa kituo chao palikuwa na kilima cha temple ambako ndiko

hekalu hili gofu liliko. Japo Wanamgambo hawa walijiita Templer yaani askari wanyonge lakini kwa kipindi kifupi tu wakawa matajiri sana. Mahujaji wa Kikristo kutoka Ulaya kuja Palestina walikuwa chini ya udhibiti wa Komandi hii na kwa pesa zake nao wakawa matajiri. Mbali na hivyo, kwa mara ya kwanza wakaanzisha mfumo wa hundi na mikopo sawa na ule wa Benki. Kwa mujibu wa Waandishi wa Kiingereza Michael Baigent na Richard Leigh, walianzisha aina fulani ya ubepari na wao ndio waliopelekea kuanzishwa kwa shughuli za sasa za mabenki zinazotoza riba kutokana na ule mfumo wao wa uchumi uliojengwa kwa msingi wa riba. Walikuwa ni hawa Matemplar ambao walihusika na mashambulizi na mauaji dhidi ya Waislamu. Kwa sababu hii Kamanda mkuu wa kiislamu Salahuddin aliyelishinda jeshi la Makruseda mnamo 1187 katika vita ya Hattin na baadaye kuikomboa Jerusalem, aliwahukumu kifo Matemplar kwa mauaji waliyokuwa wameyafanya na akawasamehe Wakristo wengi. Ijapokuwa waliipoteza Jerusalem na kupata madhara makubwa, Matemplar wakaendelea kuishi na licha ya kupungua kwa Wakristo Palestina, wakaongeza nguvu zao Ulaya wakianzia na Ufaransa na kisha katika nchi nyingine. Ikawa dola iliyokuwa ndani ya dola. Bila shaka nguvu zao za kisiasa ziliwanyima raha watawala wa Ulaya. Pia kulikuwa na jambo ambalo nalo liliwatia homa Makasisi. Kamandi ilianza kujitoa kidogo kidogo katika imani ya Kikristo.

Na wakiwa Jerusalem wakaanza kufuata madhehebu ya kikuhani. Kukawa na uvumi pia kwamba walikuwa wakifanya ibada za ajabu ajabu. Mwishowe mnamo mwaka 1307 Mfalme wa Ufaransa Philip akaamua kuwatia mbaroni Matempla hao. Baadhi yao wakafanikiwa kutoroka lakini wengi walikamatwa. Papa Clement wa Tano(Popedement V) pia nae akafanya hivyo. Baada ya kipindi kirefu cha mahojiano na mashitaka, Matempla wengi walikiri kufuata imani ya kikristo na kumtusi Yesu katika mihadhara yao. Hatimaye viongozi wa Matempla ambao waliitwa mabwana wakubwa akiwemo yule kigogo wao, Jecques de Moky wakamnyonga mwaka 1314 kwa amri ya Kanisa na mfalme. Wengi wao wakafungwa jela na Kamandi ikasambaratika na kutoweka kabisa. Baadhi ya wanahistoria wanakawaida ya kuonesha kuwa shitaka lililowakabili Matempla lililotokana na njama za Mfalme wa Ufaransa kwa kuwataja wapiganaji hao wa vita vya msalaba kuwa si watu wenye hatia. Nesta H. Webster, Mwanahistoria mashuhuri wa kiingereza mwenye elimu kubwa ya Histori ya ukuhani anayachambua masuala haya katika kitabu chake, Secret Society and Subversive Movement.

Kwa mujibu wa Webster, kitendo cha kuwatoa Matempla hatiani kwa yale waliyoyafanya katika kipindi cha mashitaka hakiwezi kukubalia kwanza wakati wa mahojiano, si Matempla wote walioteswa. Isitoshe je yale maneno ya kukiri ya Matempla yametokana na mateso waliyopewa? Kwa kweli ni vigumu kusadiki kuwa maelezo yanayotolewa na watu katika nchi mbali mbali yote yakishabiiana kabisa, eti yote yatokane na uzushi. Kama wahanga wangelishurutisha kwa mateso basi wangetoa maelezo yenye mgongano katika kuelezea aina mgongano katika kuelezea aina zote za sala za ajabu ajabu zilizokuwa zikifanyika. Lakini hasha, kila mmoja anaonekana kuelezea vile vile sala zile zile. Vyovyote iwavyo, shauri la Matempla lilikwisha Sawia na Komandi. Japo Komandi ilikoma rasmi kufanya kazi lakini kwa kweli haikutokomea kabisa. Katika kamatakamata ya mwaka 1307, baadhi ya Matempla

walifanikiwa kutoroka. Kwa mujibu wa tasnifu zilizoambatanishwa nyaraka mbali mbali za kihistoria, idadi fulani ya watu miongoni mwao walipata hifadhi katika falme moja ya Ulaya ambayo haikutambua mamlaka ya Kanisa Katoliki katika karne ya kumi na nne, nayo ni Scotland.

Huko walijikusanya upya chini ya ulinzi wa Mfalme wa Uskochi Robert the Bruce. Baada ya muda fulani, wakagundua mbinu muafaka ya kujificha ili waendelee kuishi kisirisiri. Walijipenyeza kwenye makazi muhimu katika visiwa vya Uingereza-the wall builders Lodges. Hatimaye wakapata mamlaka kamili ya kumiliki majumba haya. *The wall builders Lodges*, ikabadili jina lake, mwanzoni mwa zama hizi na sasa ikajiita the Masonic Lodge. Kwa desturi ya Scotland-The Scotish Rite ndiyo tawi kongwe kabisa la Frimansori, hiyo ikiwa ni mwanzoni mwaka Karne ya kumi na nne, pale Matempla- Mashujaa wa msalaba walipopata hifadhi nchini humo.

Mwanahistoria wa Kiyahudi, Theodore Reinach anasema kuwa kabbalah ni sumu ya ajabu kabisa inayoingia ndani ya vena za Uyahudi na kuziathiri kabisa. Salomoni Reinach anaiainisha kabbalah kama ni moja ya pogo za akili ya mwanadamu. Sababu ya maelezo haya ya Reinach kuwa kabbalah ni moja ya pogo za akili ya binadamu ni kuwa mafundisho yake yananasibiana kwa kiasi kikubwa na uchawi. Kwa maelfu ya miaka, kabbalah imekuwa moja ya misingi ya kila Ibada ya uchawi. Inasadikika kuwa wasomi wa kiyahudi (Rabbis) wanaosomea kabbalah wana nguvu kubwa za kichawi. Aidha watu wengi wasiokuwa wayahudi wameathiriwa na kabbalah na wamejaribu kutumia uchawi kwa kutumia mafundisho yake. Mambo ya siri ambayo yalikita mizizi Ulaya mwishoni mwa zama za kati hasa yale yaliofanywa na wanakemia, kwa kiasi kikubwa mizizi yake ipo katika kabbalah. Jambo la ajabu ni kuwa Uyahudi ni dini ya Mungu mmoja inayokwenda kwa ufunuo wa Taurati ya Musa (a.s) lakini ndani ya dini hii kuna utaratibu unaoitwa kabbalah ambao unafuata yale mafundisho ya msingi ya uchawi yaliyoharamishwa na dini hii. Hii inathibitisha ukweli tuliouelezea hapo juu na inabainisha kuwa kabbalah kwa uhalisi wake ni jambo ambalo limeingia katika Uyahudi kutoka nje ya dini hii. **Lakini nini chanzo cha jambo hili?**

Mwanahistoria wa Kiyahudi Fabre d'Olivet anasema kuwa kabbalah ilitokea katika Misri ya kale. Kwa mujibu wa mwandishi huyu, mizizi ya kabbalah imetambaa kutoka Misri ya kale. Kabbalah ni hadithi iliyosikiwa na baadhi ya viongozi wa Waisrael katika Misri ya kale na ikawasilishwa kwa njia ya fasihi simulizi kutoka kizazi hadi kizazi. Kwa sababu hiyo, lazima tuiangalie Misri ya kale ili tuone vyanzo hasa vya kabbalah- matempla na Frimansori.

## Wachawi wa Misri ya zamani

Misri ya kale ya Mafirauni(Mafarao) ilikuwa moja ya nchi zilizokuwa na tamaduni kuu za enzi hizo ulimwenguni. Ilikuwa moja ya nchi za kidhalimu kabisa. Minara mikubwa ambayo bado ipo tangia enzi hizo za Misri ya kale kama mapiramidi yalijengwa na mamia kwa maelfu ya watumwa waliofanya kazi,kwa vitisho vya bakora na kunyimwa chakula hata kufikia mahala pa kufa. Mafirauni, watawala wakuu wa Misri walijitapa kuwa wao ni miungu na kwamba waabudiwe na watu. Moja ya vyanzo vya habari kuhusu Misri ya Kale ni maelezo yao wenyewe.Maelezo haya yaligunduliwa katika karne ya 19 na baada ya kazi ngumu, herufi za Kimisri zikasomeka na hivyo taarifa nyingi kuhusu nchi hiyo zikapatikana. Lakini kwa vile maelezo haya yaliandikwa na Wanahistoria waliokuwa serikalini, yamejaa maelezo ya upendeleo ambayo yalikusudiwa kuitukuza dola.

Bila shaka, kwetu sisi, chanzo cha habari juu ya jambo hili ni Qur'an. Katika Qur'an, katika kisa cha Musa, tunapewa habari muhimu kuhusu utawala wa Misri. Aya za Qur'an zinabainisha kuwa kulikuwa na mamlaka kuu mbili za utawala nchini Misri; Firauni na baraza lake la ndani. Kazi ya baraza hili ilikuwa ni kumtukuza Firauni; mara zote firauni alikuwa akikutana nalo na katika nyakati fulani fulani alikuwa akifuata maoni ya baraza lake . Aya zinazonukuliwa hapa chini zinaonyesha kazi ya baraza hilo; "Na alisema Musa; Ewe Firauni! Mimi ni Mtume nitokae kwa Mola wa walimwengu. Yanipasa nisiseme juu ya Mwenyezi Mungu lolote ila haki tu. Kwa yakini nimekufikieni kwa dalili waziwazi zitokazo kwa Mola wenu. Basi wapeleke wana wa Israel pamoja nami katika (nchi waitakayo, usiwazuilie hapa Misri ukawa unawatesa). Firauni akasema kama umekuja na hoja basi ilete ukiwa ni miongoni wa wasemao kweli. Hapo Musa akaitupa fimbo yake (chini). Na mara ikawa nyoka dhahiri. Na akatoa mkono wake. Mara ukawa mweupe kwa watazamao. Wakasema wakuu wa kaumu ya Firauni (pamoja na yeye Firauni); hakika huyo ni mchawi ajuae (uchawi vema). Anataka kukutoeni katika ardhi yenu. Basi mnatoa shauri gani? Wakasema (kumwambia firauni). Muache kidogo yeye na ndugu yake (huyu Haruni anayejipa Utume pamoja naye, usiwaue). Na watume (wakusanyao mijini wakukusanyie wachawi wakubwa wakubwa wote). Wakuletee kila mchawi ajuae Qur'an sura (7:104-112). Izingatiwe kuwa hapa limetajwa baraza la Firauni ambalo linamshauri, na ambalo linamuhamasisha kupambana na Musa na linapendekeza mbinu fulani. Tukiziangalia kumbukumbu za Historia ya Misri, tunaona kuwa kada kuu mbili za baraza hili zilikuwa ni jeshi na Taasisi ya Ukasisi. Hakuna haja ya kufafanua umuhimu wa jeshi; Jeshi hili ndilo lililojenga nguvu za tawala za Mafirauni. Ila tulitazame kwa mazingatio zaidi jukumu la Makasisi hawa. Makasisi wa Misri ya kale walikuwa ni tababaka la watu ambao katika Qur'an wametajwa kama wachawi. Hawa waliwakilisha dhehebu ambalo liliunga mkono utawala. Iliaminika kuwa nao walikuwa na madaraka maalum na walikuwa na elimu ya sihiri. Kwa madaraka haya, waliwavuta watu wa Misri na kuimarisha nafasi yao katika utawala wa Mafirauni. Tabaka hili kwa mujibu wa kumbukumbu za Misri, lilijulikana kama Makasisi wa Amoni. Hawa walikuwa na kazi ya kufanya uchawi na kuendesha dhehebu lao la kipagani;

mbali na hivyo pia walisomea sayansi mbalimbali kama vile unajimu, hesabati na Jiometri. Tabaka hili la makasisi ilikuwa ni Taasisi iliyokuwa na elimu maalum. Katika jarida lililoitwa Mason Dergisi, Jarida lililosambazwa kwa mafyoso wa Uturuki, Mizizi ya Frimansori inatajwa kuanzia katika Taasisi hii ya siri, na wanatajwa rasmi makasisi wa Misri ya kale. Tafakuri inavyozidi kukuwa kwa wanadamu, Sayansi nayo inazidi kupiga hatua na kadri Sayansi inavyopiga hatua siri nyingi zinazidi kuongezeka katika mfumo wa siri. Katika hatua hii ya maendeleo shughuli ya siri ambayo kwanza ilianzia Mashariki, China na Tibet na kisha kuenea India, Mesopotamia na Misri ikajenga msingi wa elimu ya ukasisi ambayo imefanyiwa kazi kwa maelfu ya miaka na kujenga msingi wa madaraka ya makasisi nchini Misri. Kuna uhusiano gani kati ya falsafa ya siri ya Makasisi wa Misri ya zamani na Mafrimansori wa hivi leo? Misri ya zamani ni mfano hai wa mfumo wa siasa usio na Mungu uliotajwa katika Qur'an,ambao ulitokomea maelfu ya miaka iliyopita. Je waweza kuwa na athari hadi leo? Kupata jibu la maswali haya lazima tuziangalie Imani za Makasisi wa Misri ya kale kuhusiana na chanzo cha Ulimwengu na maisha. Kwa kifupi Matempla hawakutoweka kabisa bali falsafa yao. Imani zao na ibada zao bado zinaendelea chini ya mwavuli wa Frimansori. Dhana hii inatiwa nguvu za ushahidi mwingi wa kihistri na hiv leo inakubwaliwa na idadi kubwa ya Wanahistoria wa magaharibi ima awe Mafyoso au la. Katika kitabu chetu, The new Masonic Order, tumeutathmini kwa kina ushahidi huu. Dhana inayoihusisha mazizi ya Mansori na Matempla, mara nyingi inarejewa katika majarida yanachapishwa na Mansori wenyewe kwa ajili ya Wananchama wao. Wanachama wa Frimansori wanaikubali kabisa dhana hii.

Mojawapo ya majarida hayo linaitwa Minnar Sinan(ni jarida la Mafyoso wa Uturuki) ambalo linaezea uhusiano kati ya komandi ya Matempla na Frimansori kwa maneno yafuatayo". "Mnamo mwaka 1312, pale Mfalme wa Ufaransa kwa shinikizo la kanisa alipolifunga komandi ya Matempla na mali zao kuwapa askari wa mtakatifu John mjini Jerusalem harakati za matempala hazikukoma. Idadi kubwa ya Matempala wakapata hifadhi katika maskani ya Frimansori iliyokuwepo ulaya wakati huo. Kiongozi wa Matempla, Mabeignac, akiwa na wanachama wengine, wakapata usalama nchini Scotland chini ya mwavuli wa Wall builder na chini ya jina la Mac Benach. Mfalme Scotland Robert the Bruce akawakaribisha na kuwaruhusu kuwa na ushawishi mkubwa katika maskani za Frimansori nchini Scotland. Matokeo yake maskani za Scotland umuhimu mkuibwa kwa mtazamo wao wa kiufundi na fikra zao. Leo hii Mafyoso wanatumia jina la Mac Benach kwa heshima. Mafyoso wa Ufaransa walioritihi vitu vya Matempla wakareje zao Ufaransa miaka mingi baadaye na kuimarisha ngome yao ya kaaida ikijulikana kama kaaida ya Scotland(Scotish Rights). Aidha, Mimar Sinan inatoa habari nyingi kuhusu uhusiano wa Matempla na Mafrimasonri. Katiika makala yenye kichwa Templas and Frimanson inasema sala ya sherehe za uzinduzi wa Komandi ya Matempla ni sawa kabisa na sala Mafyso wa zama hizi. Kwa mujibu wa makala hiyo hiyo, kama ilivyo katika Mansori wanachama wa Komandi ya Matempla wakiitana Brother(ndugu). Mwishoni mwa makala hayo tunasoma maneno haya; "komandi ya Matempla na shirika la Frimansoni yanashajiishana, kwa kiasi kikubwa hata sala za mashirika haya

zinashabihiana kwa maana zimaigwa kutoka kwa Matempla. Kwa ajili hiyo, Mafyoso kwa kiasi kikubwa wamejifananisha na Matempla na yaweza kusemwa kuwa, kile kinachoonwa kuwa ni usiri mkubwa wa Frimansonri kwa akisai kikubwa kimeigwa kutoka kwa Matempla. Kwa kufupisha hapa ni kuwa, kama tulivyosema katika anuani ya makala haya, twaweza kusema kuwa chanzo cha sanaa Kifalme na usiri wa Frimansori chatokana na Matempla. Mwisho, tunasema kuwa imetokeya huko nyuma kwa Matempla na kwamba Mafyoso wamefuata falsafa ya Komandi ya Matempla. Mafyoso wenyewe wanalikubali hili lakini jambo muhimu kwa tafakuri yetu ni nini asili au chanzo cha falsafa hii. Kwa nini Matempla waliachana na Ukristo na kufuata mafundisho mapya. Kitu gani kilichowapelekea kufikia uamuzi huo? Kwa nini walifanya mageuzi hayo kule Jerusalem na je kupitia tawi hili la Frimansoni kumekuwa na athari gani Duniyani kutokana na Falsafa hii iliyofuatwa na Matempla.

## Matempla na Kaballa

Kitabu kilichoandikwa na Mafyoso Christopher na Robert Lomas kiitwacho The Hiram Key kinafichua mambo fulani ya kweli kuhusu mizizi ya Frimansori. Kwa mujibu wa Waandishi hawa, ni dhahiri kuwa Frimansori ni mwendelezo wa  Matempla. Mbali na hivyo, Waandishi hawa pia, wameviangalia pia vyanzo vya Matempla. Kulingana na dhanna yao, Matempla walipitia hatua kubwa za mabadiliko wakati walipokuwa Jerusalem. Mahala palipokuwa kwa Ukristo wao walianzisha madhehebu nyingine. Katika mzizi wa mabadiliko haya, kuna siri ambayo waliifichua ambayo ni hekalu la Suleiman pale Jerusalem ambalo mabaki yake, walitaka kuyachunguza. Waandishi hawa wanasema kuwa, Matempla walikuwa wakiitumia ule ulioitwa kuwa wajibu wao wa kulinda mahujaji wa Kikristo waliozuru pale Palestina lakini kumbe hiki kilikuwa kisingizio, lengo halisi lilikuwa jingine kabisa. Hakuna ushahidi kuwa wale Waasisi walikuwa wakitoa ulinzi kwa Mahujaji bali tulichokugundua ni kuwa kuna ushahidi mkubwa kuwa walikuwa wakichimbua chini ya mabaki ya hekalu la Herold. Waandishi wa kitabu cha Hiram Key sio wao pekee waliogundua vielelezo vya jambo hili. Gaetani De la Forge, Mwanahitoria wa Ufaransa naye ametoa maelezo kama haya; “jukumu halisi la Wale wanamgambo tisa wa Krusade walikuwa wakifanya utafiti katika eneo hilo ili kupata masalia na kupata kumbu kumbu za maandiko ya awali ambao yanachimbuko ya maelezo ya siri ya dini ya kiyahudi na Misri ya zama za kale. Mwisho mwa karne ya 14 Charles Wilson wa Royal Engeneers alianza kufanya utafiti wa mabaki ya kale kule Jerusalem. Yeye akafka mahala pa kuona kuwa, Matempla walikuwa wamekwenda Jerusale kutaifiti mabaki ya hekalu. Wilson aligundua chimba chimba na fukua fukua china ya misingi ya hekalu na akahitimisha kuwa kazi hii ilifanywa kwa zana ambazo zilikuwa za Matempla. Vifaa hivi vingalipo katika hazina ya mabaki ya kale ya Robert Brydon, ambaye anamiliki hifadhi ya kumbu kumbu zinazohusiana na Matempla. Waandishi wa kitabu cha the Hiram Key wanadai kuwa chimba chimba ya Matempla haikuishia matupu, kwamba ile Komandi iligundua kumbukumbu fulani pale Jerusalem ambayo ndiyo iliyobadili mtazamo wao.

Mbali na hao watafiti wengine nao wana maoni hayo hayo. Yumkini lazima kulikuwa na jambo lililowapelekea Matempla kubadili mfumo wa imani na falsafa yao tofauti na Ukristo licha ya ukweli kuwa hapo awali walikuwa wakristo waliotoa katika nchi ya Kikristo. Kwa mujibu wa fikra za watafiti wengi jambo hili lilikuwa Kaballa. Maana ya neno Kaballa, ni fasihi simulizi. Misahafu na makamusi yanalifafanua neno hili kama siri kubwa, tawi la siri siri la dini ya Uyahudi. Kwa mujibu wa ainisho hili neno la Kaballa linachukua maana iliyofichikana katika Taurati na maandiko mengine ya dini Uyahudi. Lakini tunapochunguza kwa undani jambo hili tunaona kuwa ukweli wa mambo ni mwingine kabisa. Hakika ya mambo inatuplekea kufikiri hitimisho jingine kuwa Kaballa ni mfumo wenye mizizi ya ushirikina wa kipagani, kwamba ilikuwepo kabla ya Taurati na ilienea ndani ya dini ya Uyahudi hata baada ya kufunuliwa kwa Taurati. Ukweli huu wa kuvutia kuhusu Kaballa unafafanuliwa kuwa ndio chanzo hasa. Murat Orgen Frimansori wa kituruki yeye ansisitiza yafuatayo katika kitabu chake Masonluk Nedir Ve Nasirdir?(Frimasonri ni nini, ikoje?).

“Hatujui vizuri wapi ilikotokea Kabala au namna ilivyojiendeleza ni jina la jumla na kuwa ilikusanywa zamani zaidi kabla ya Taurati. Mwanahistoria wa Ufaransa Gougenot Des Mousseaux yeye anasema kuwa, Kaballa ni ya zamani kabla ya Uyahudi.

# Imani ya kale ya Misri juu ya dhana ya evolusheni

Katika kitabu chao kiitwacho,*The Hiram Key*, waandishi wa frimansori wa kiingereza Christopha Knight na mwenzie Robert Lomas wanadai kuwa Misri ya kale inachukua sehemu muhimu kuhusiana na vyanzo vya frimansori. Kwa mujibu wa waandishi hao,fikra muhimu ambayo imezaa frimansori ya sasa kutoka Misri ya kale ni ile ya ulimwengu kujiendesha wenyewe na kutokea kwa bahati nasibu.Wanaifafanua dhana hii kwa maneno haya:

Wamisri waliamini kuwa maada ilikwishakuwepo siku zote; kwao wao lilikuwa ni jambo lisilo kuwa na mantiki kufikiri kuwa Mungu ndiye anayefanya kila kitu kutokana na hamna. Dhana yao ilikuwa kwamba ulimwengu ulianza pale ilipotokea mvurugano,na kwamba tokea hapo kumekuwa na ugomvi baina ya nguvu za asili. Hali hii ya machafuko iliitwa Nun, na kama yalivyo maelezo ya Sumaria kulikuwa na giza tupu sehemu zote, hapakuwa na jua ndipo nguvu kujiumba ilipoamuru maisha yaanze.Nguvu hii isiyoonekana ambayo ilikuwa ndani ya machafuko haikujijua kuwa yenyewe ilikuwepo. Itakumbukwa kuwa imani zilizoelezwa hapa zinafanana kabisa na madai ya walahidi wa zama hizi, imani zinakuzwa na ajenda ya jamii ya wanasayansi wakitumia maneno kama vile nadharia ya evolusheni, nadharia ya mchafuko(chaos theory)na mjumuiko wa maada(essential organization of matter).

Knight na Lomas wanaendelea kusema; Cha kushangaza, maelezo haya juu ya maumbile yanaiolezea kikamilifu dhana inayoshikiliwa na sayansi ya leo hasahasa chaos theory. Knight na Lomas wanadai kuwa kuna uwiano kati ya imani za kale za Misri na sayansi ya leo, lakini wanapozungumza juu ya sayansi ya leo, kama tulivyosema, wanamaanisha dhana za kilahidi,kama vile nadharia ya evolusheni na nadharia ya machafuko. Licha ya ukweli kwamba nadharia hizi hazina msingi wa kisayansi,zimewekwa kinguvunguvu katika fani ya sayansi kwa takriban karne mbili zilizopita, na zinawasilishwa kama nadharia zilizohalalishwa kisayansi.(Katika vifungu vifuatavyo tutawatazama wale walioweka nadharia hizi katika ulimwengu wa sayansi.)

Sasa tumefikia nukta muhimu. Tuelezee kwa kifupi kile tulichokigundua hadi hapa tulipofika;

1.Tulianza mjadala wa kujadili oda ya matempla ambayo ndiyo inayodhaniwa kuwa chanzo cha frimansori.Tumeona kuwa, ingawaje matempla kimsingi walionekana kama wakristo lakini waliathiriwa na mafundisho ya siri waliyoyagundua yerusalemu, wakachana kabisa na ukristo na wakawa na Taasisi inayopinga kabisa dini hii wakitekeleza ibada mpya.

2.Pale tulipouliza ni itikadi gani hiyo iliyowakumba matempla,tukaona kuwa kimsingi ilikuwa kabbalah.

3.pale tulipoichunguza kabbalah ,tukapata ushahidi kuwa ilikuwa ni itikadi ya kipagani ambayo ilikuwa ya zamani mno kuliko uyahudi japo inafanana na usufi wa kiyahudi, kwamba ni baadaye kabbalah iliingia katika dini hiyo, na kwamba mizizi yake halisi inaonekana katika Misri ya kale.

4.Misri ya kale ilitawaliwa kwa utaratibu wa kipagani wa Mafirauni na huko tukaikuta dhana inayojenga msingi wa falsafa ya kikafiri ya hivi leo;kwamba ulimwengu unajiendesha wenyewe na kwamba umetokea kwa bahati nasibu.Hii kwa hakika inatoa picha maridadi.Je ni bahati tu kwamba falsafa ya makasisi wa Misri ya kale bado ipo,na kwamba bado kuna alama za mlolongo wa (kabbalah –matempla –frimansori) .?

Je hawa mafyoso ambao wameweka kumbukumbu katika historia ya ulimwengu tokea karne ya 18 wakifanya mapinduzi wakiendeleza falsafa na mifumo ya siasa ni warithi wa wachawi wa Misri ya kale?

Ili kujibu maswali haya vizuri hebu tuyachunguze kwa undani zaidi matukio ya kihistoria ambayo tumeyagusia kwa kifupi tu.

## Habari ya ndani juu ya kabbalah

“Kutoka” ni jina la kitabu cha pili cha Taurati. Kitabu hiki kinaelezeya jinsi wana wa Israel chini ya uongozi wa Mussa, walivyoondoka Misri kuepuka udhalimu wa Firauni. Firauni aliwashurutisha wana wa Israel kuishi kama watumwa na hakukubali kuwaachia huru. Lakini pale alipokumbana na miujiza aliyoonesha Mwenyezi Mungu kupitia kwa Mussa na maangamizi aliyowapelekea watu wake Firauni alitulia. Kwa hiyo usiku mmoja wana wa Israel wakakusanyika na kuanza safari yao kuhama Misri. Baadaye Firauni akawashambulia waisrael lakini Mwenyezi Mungu akawanusuru kwa muujiza mwingine zaidi aliouonesha kupitia kwa Mussa. Lakini katika Qur’an tunakuta maelezo sahihi zaidi ya kuhama kwao kutoka Misri, kwa sababu Taurati imehujumiwa baada ya kufunuliwa kwa Musa. Ushahidi muhimu wa hili ni kuwa katika vitabu vitano vya Taurati- Kitabu cha mwanzo, kutoka, walawi, hesabu na kumbukumbu la Taurati- kuna migongano mingi. Ukweli kuwa kitabu cha kumbukumbu la Taurati kimeishia na maelezo ya kufa na kuzikwa kwa Mussa ni ushahidi usiopingika kwamba sehemu iliyobaki itakuwa imeongezwa baada ya kifo cha Musa. Katika Qur’an, katika maelezo ya kuhama kwa wana wa Israel kutoka Misri kama ilivyo katika habari zote zinazohusiana na jambo hili, hakuna mgongano hata kidogo. Habari hii inaelezwa kwa usahihi kabisa. Isitoshe kama zilivyo habari nyingine, Mwenyezi Mungu anafunua hikma na siri nyingi katika jambo linalozungumziwa. Kwa sababu hii pale tunapoziendea habari hizi kwa undani, tunaweza kupata mafundisho mengi ndani yake.

## Ndama wa Dhahabu

Moja kati ya mambo muhimu kuhusiana na kuhama kwa wana wa Israel kutoka Misri, kama ilivyoelezwa katika Qur'an, ni kuwa waliasi dhidi ya dini iliyofunuliwa kwao na Mungu licha ya ukweli kwamba Mwenyezi Mungu aliwanusuru na udhalimu wa Firauni kupitia kwa Musa. Wana wa Israel hawakuweza kufahamu ile Tawhiid ambayo Musa aliwafikishia bali wao walizidi kuielekea Ibada ya Sanamu. Qur'an inaulezea hivi muelekeo huu wa ajabu- "Na tukawavusha wana wa Israel baharini (wakasalimika na balaa la Firauni) na wakawafikia watu waliokuwa wakiabudu masanamu yao. Wakasema Ewe Musa! Tufanyie waungu na sisi (yaani masanamu) kama wao walivyo na miungu. Musa akasema hakika nyinyi ni watu mfanyao ujinga. Hawa yaataangamia haya waliyonayo na ni bure waliyokuwa wakiyafanya. (7:138-139).

Licha ya maonyo ya Musa, wana wa israel waliendelea na upotevu huo, na Musa alipowaacha na kwenda mlima wa Sinai, upotevu wao ukadhihirika zaidi. Wakitumia fursa ya kutokuwepo kwa Musa, mtu mmoja aliyeitwa Sammir akawajia. Akawashawishi watengeneze sanamu la ndama na kisha waliabudie.

Musa akarudi kwa watu wake kwa ghadhabu na masikitiko. Akasema Enyi watu wangu je Mola wenu hakukuahidini ahadi nzuri, je umekuwa mrefu kwenu muda wa ahadi hiyo (mnaona haitimizwi) au mumetaka ikushukieni ghadhabu kutoka kwa Mola wenu; na kwa hivyo mmevunja ahadi yangu? Wakasema sisi hatukuvunja ahadi yako kwa khiyari yetu walakini tulibebeshwa mizigo ya watu; (vyombo vya dhahabu tulivyoviazima kwa wanawake wa kimisri). Na namna hivi alitia Samir (sehemu yake). Na akawatolea (akawaundia katika myayusho huo) ndama, kiwiliwili kamili kinacholia. Na wakasema; huyu ndio Mungu wenu na Mungu wa Musa lakini Musa amesahau (amekwenda kumtafuata majabalini). (20:86-88).

### Ibada ya masanamu ya Waisrael

Kwanini kulikuwa na ung'ang'anizi miongoni mwa wana wa Israel katika kukita na kuabudia masanamu? Nini hasa kilikuwa chanzo cha mwelekeo huu? Ni wazi jamii ambayo hapo kabla haikuwahi kuamini masanamu isingeweza kwa ghafla kufuata mwenendo huo wa kipumbavu kwa kutengeneza sanamu na kuanza kuliabudia. Ni wale tu ambao ibada ya sanamu ilikuwa ya kawaida kwao ndio ambao wangeweza kuamini upuuzi huo.

Hata hivyo, wana Israel walikuwa watu ambao hapo kabla waliamini Mungu mmoja tokea zama za mzee wao Ibrahimu. Jina hili "Waisrael" au "wana wa Israel" kwanza kabisa ilitolewa kwa watoto wa Yaqub, mjukuu wa Ibrahimu. Baadaye jina hili likatumika kwa Mayahudi wote waliotokana naye.

Waisrael walikuwa wameichunga Imani ya Mungu mmoja ambayo waliirithi kutoka kwa wazee wao; Ibrahimu, Is-haqa na Yaqub (a.s). Wakiwa pamoja na Yusufu (a.s), walikwenda Misri na wakaichunga Imani yao ya Mungu mmoja kwa kipindi kirefu, licha ya ukweli kwamba waliishi pamoja na washirikina wa Kimisri.

Inabainika wazi katika maelezo yaliyotolewa katika Qur'an kuwa pale Mussa alipowajia, Waisrael walikuwa watu walioamini Mungu mmoja. Isipokuwa tu ni kwamba pamoja na kuamini kwao Mungu mmoja, Waisrael waliathiriwa na Wapagani waliokuwa wakiishi nao pamoja na wakaanza kuwaiga wakibadili dini waliochaguliwa na Mwenyezi Mungu na kufuata Ibada ya Sanamu ya jamii nyingine.

Tunapolichunguza swala hili kwa undani kwa kuzingatia kumbu kumbu za historia, tunaona kuwa dhehebu la kipagani lililowaathiri Waisrael lilikuwa lile la Misri ya kale. Ushahidi muhimu wa kushadidia hitimisho hili ni kuwa yule ngamia wa dhahabu waliyemuabudia Waisrael wakati Mussa alipowenda mlima Sinai, alikuwa mfano wa masanamu ya Misri, Hatha na Aphis. Katika kitabu chake Too Long in the Sun, muandishi wa Kikristo Richard Rives ameandika hivi;

**Hatha na Aphis Ng'ombe jike na fahari miungu ya Misri ilikuwa ikiwakilisha Ibada ya Jua. Ibada yao ilikuwa ni muendelezo wa historia ya utukuzo wa Jua. Yule ndama wa dhahabu wa mlima Sinai alikuwa ushahidi tosha wa kuthibitisha kuwa karamu iliyotangazwa ilihusiana na ibada ya Jua. Athari ya dini ya kipagani ya Misri ilionekana katika sura nyingi tofauti. Mra baada ya kuwashinda wapagani imani yao ya kishirikina ikadhihirika kama aya inavyosema; Ewe Mussa! Tufanyie waungu na sisi (yaani masanamu) kama wao walivyo na miungu. (7:138).**

Na kumbukeni habari hii pia (mliposema, Ewe Mussa hatukuamini mpaka tumuone Mwenyezi Mungu waziwazi. (2:55). Maneno yao haya yanadhihirisha kuwa wao walitaka kuabudia Mungu wa kimaada ambayo wangemuona kwa macho kama dini yao ya kipagani ilivyo wapatia wamisri mungu kama huyo.

Muelekeo huu wa Waisrael kufuata upagani wa Misri ya kale ambao tumeuelezea, ni muhimu ueleweke kwani ndio unaotupa ufahamu wa jinsi kilivyohujumiwa kitabu cha Torati na unatufahamisha chanzo cha Kabbalah. Tukiyatafakari mafundisho haya kwa mazingatio, tutaona kuwa ni katika vyanzo hivi unapokutikana upagani wa Misri ya kale na falsafa ya kilahidi.

## Kutoka Misri ya kale hadi Kabbalah

Wakati Mussa angali hai, waisrael walianza kutengeneza masanamu kama yale yale waliyoyaona Misri na kuyaabudia. Baada ya Mussa kutawafu (kufariki Duniya), hakukuwa na kizuizi cha kuzuia Imani potofu. Bila shaka haiwezi kusemwa kwamba ni Mayahudi wote waliokengeuka lakini baadhi yao walifuata upagani wa Misri. Kwa kweli walishikilia mafundisho ya ukasisi wa Misri (wachawi wa Firauni) ambayo yalijengwa kwa msingi wa imani za jamii hiyo, na wakaihujumu Imani yao kwa kutumbukiza mafundisho haya ndani

yake. Itikadi mabayo ilitumbukizwa katika Uyahudi kutoka Misri ya kale ilikuwa ni Kabbalah. Kama ulivyokuwa mfumo wa makasisi wa Misri, Kabbalah nao ulikuwa mfumo wa siri, na msingi wake ulikuwa utamaduni wa uchawi. Kabbalah inatoa maelezo ya maumbile tofauti kabisa na yale yaliyokutwa katika Torati. Ni maelezo ya kilahidi yaliyoegamia dhana ya Misri ya kale juu ya uhai wa milele wa maada. Murat Ozgen mwana frimansori wa Kituruki ana haya ya kusema juu ya swala hili;

Ni dhahiri kuwa Kabbalah iliundwa miaka mingi kabala ya Taurati haijaja. Sehemu zaidi ya Kabbalah ni nadharia juu ya muundo wa ulimwengu. Nadharia hii iko tofauti kabisa na maelezo juu ya maumbile yaliyopokewa na dini zinazoamini Mungu. Kwa mujibu wa Kabbalah, mwanzoni kabisa mwa hatua ya kuumbwa kwa ulimwengu, vitu vinavyoitwa Sefiroth maana yake ni duara au mihimili ikiwa na sifa za kiroho na kimaada iliibuka. Idadi ya jumla ya vitu hivi ilikuwa 32.

Ile kumi ya mwanzo ndiyo iliyoshikilia Solar System na mingine iliyobaki imeshikilia makundi ya nyota angani. Imani hii ya kipekee ya Kabbalah inabainisha kuwa inahusiana kwa karibu na mifumo ya Imani ya unajimu. Kwahiyo Kabbalah inatenganishwa mbali kabisa na dini ya uyahudi na inanasibishwa kwa karibu zaidi na dini za kale za siri za mashariki. Kwa kufuata mafundisho ya siri na ya ulahidi ya Misri ya kale ambayo yalijengwa kwa msingi wa uchawi, Mayahudi wakapuuza mambo yaliyoharamishwa katika Taurati. Wakashikilia Ibada za kichawi za wapagani na hivyo Kabballah ikawa itikadi ndani ya uyahudi lakini ikienda kinyume na Taurati. Katika kitabu chake kiitwacho Secrety Societies and Subversive Movements, mwaandishi wa Kingereza Nesta H Webster anasema;

Uchawi kama tuujuavyo ulikuwa ukifanywa na Wakanan kabla ya kuvamiwa kwa Parestina na waisrael. Misri, India na ugiriki nazo zilikuwa na wachawi wao na Miungu yao. Licha ya makemeo dhidi ya uchawi yaliyomo katika sheria ya Musa, Mayahudi wakipuuzilia mbali makemeo haya walijiingiza na kuuchanganya utamaduni mtukufu waliorithi na mawazo ya kichawi yaliyotokea katika jamii nyingine.

Wakati huo huo kwa upande wa Kabbalah ya Uyahudi iliyochukuliwa kutoka katika Falsafa ya Persian Magi na ya Neo Platonists, na ya Neo Pythagoreans hapo ndipo penye maelezo kuwa tunachokijua sisi hivi leo kuhusu Kabbalah hakitokani kabisa na uyahudi. Kuna aya katika qur’an inayozungumzia jambo hili. Mwenyezi Mungu anasema kuwa Waisrael walijifunza tamaduni za kichawi za kishetwani kutoka nje ya dini yao; Wakafuata yale waliofuata Mashetwan, (wakadai kuwa yalikuwa) katika Ufalme wa Suleiman; na Suleiman hakukufuru, bali Mashetwani ndio waliokufuru, wakiwafundisha watu uchawi (waliokuwa wakiujua wenyewe tangu zamani), na (uchawi) ulioteremshwa kwa malaika wawili, Haruta na Maruta katika (mji wa) Babil. Wala (Malaika hao) hawakumfundisha yeyote mpaka wamwambie; hakika sisi ni mtihani (wa kutazamwa kutii kwenu); basi usikufuru.

**Wakajifunza kwao ambayo kwa mambo hayo waliweza kumfarakanisha mtu na mkewe (na mengineyo). Wala hawakuwa wenye kumdhuru yeyote kwa hayo ila kwa idhini ya Mwenyezi Mungu. Na wanajifunza ambayo yatawadhuru wala hayata wafaa. Na kwa yakini wanajua kwamba aliyekhiyari haya hatakuwa na sehemu yoyote katika Akhera. Na bila shaka ni kibaya kabisa walichouzia nafsi zao laiti wangelijua. (2:102).**

Aya hii inabainisha kuwa japo Wayahudi fulani walijuwa kuwa watapata khasara katika maisha ya Akhera lakini bado walijifunza na kufuata tamamduni za uchawi. Hivyo walikengeuka na kutoka katika sheria ambayo Mungu aliwashushia, wakiwa wameuza nafsi zao wenyewe na kutumbukia katika upagani (itikadi za kichawi). Ni kibaya walichojiuzia nafsi zao kwa maneno mengine maana yake waliacha imani yao. Mambo yaliyozungumziwa katika aya hii yanaonesha vipengele vikuu vya mfarakano katika historia ya Uyahudi. Mapambano yalikuwa kati ya mitume ambao Mwenyezi Mungu aliwashusha kwa mayahudi pamoja na mayahudi walioamini na kuwatii kwa upande mmoja dhidi ya wale mayahudi waliopotoka na kuasi amri za Mungu na kuiga tamaduni za kipagani wa watu walioishi nao ambao walifuata ada za utamaduni wao badala ya sheria ya Mungu.

## Waliokuwa Matempla ndio hao wakaja kuwa Mafrimansori

Katika nadhariya ya mafundisho ya kabala, sio tu kulikuwa na utitiri wa miungu bali hata ule upweke wa mwanzo wa mungu usiojulikana na wenye maelezo tata juu ya asili yake pia una pande mbili; upande wa kiume na wa kike yaani ubaba na umama. Hokhmah na Binah ndizo zilizokuwa sehemu mbili za mungu. Wanakabala walitumia wazi wazi tamathali za kijinsia kuelezea maingiliano ya kimaumbile kati ya Hokmah na Binah yaliyozalisha maumbile mengine zaidi. Jambo jingine la kuchekesha katika theolojia hii ya kishirikina ni kuwa, kwa mujibu wa theolojia hii binadamu hawakuumbwa bali kwa kiasi fulani na wao wana asili ya kiungu. Bwana owens, mtafiti wa kiamerika anaielezea hivi dhana hii;

Picha ya ajabu ya Mungu iliyobuniwa na kabala ina sura ya upweke na wingi. Kwa dhana hii ya kabala Mungu alikuwa Adamu kadmon: yaani binadamu mkubwa wa kwanza. Mtu alikuwa sawa na Mungu katika ile sifa ya asili ya kutoumbwa na katika lile umbile la kutatanisha. Dhana hii ya ajabu inayomuelezea Adamu kama mungu ilishadidiwa na mafundisho ya kabala: thamani ya tarakimu ya majina Adamu na Yehova katika kiebrahania ni 45 kila moja. Kwa hiyo katika mafunzo ya kabbala Yehova na Adam walikuwa sawa, hivyo Adam alikuwa mungu. Kwa dai hili binadamu wote wanapofikia daraja la juu kabisa huwa sawa na Mungu

Theolojia hii inayojumuisha dhana ya Upagani ndiyo iliyojenga msingi uliopotosha dini ya Uyahudi. Wanakabbala wa kiyahudi wakakiuka mipaka ya akili ya kawaida ya binadamu kiasi kwamba wakafika mahala pa kuthubutu kuwafanya binadamu miungu. Mbali na hivyo,

kwa mujibu wa theolojia hii, sio tu binadamu walikuwa miungu bali miungu wenyewe walikuwa Wayahudi peke yao; Watu wa jamii nyingine walihesabiwa kama binadamu tu wa kawaida.

Matokeo yake ndani ya dini ya uyahudi ambayo kimsingi ilianzishwa kwa ajili ya kumtumikia na kumtii mungu, itikadi hii potofu ilianza kumea, lengo lake likiwa kutimiza ujinga wa wayahudi. Licha ya kupingana kwake na Taurati , kabbala ikaingizwa katika uyahudi na hatimaye ikaanza kuihujumu Taurati. Jambo jingine la kuzingatia kuhusiana na mafundisho potofu ya kabbala ni ule uwiano wa fikira baina yake na Upagani wa misri ya zamani. Kama tulivyosema awali, wamisri wa zamani waliamini kuwa maada ilikuwa na uhai; kwa maneno mengine walikanusha kuwa maada iliumbwa pasipo kitu chochote. Kabbala nayo inadai hivyo hivyo kuhusiana na binadamu. Inadai kuwa binadamu hawakuumbwa na kwamba wanajiendeshea wenyewe maisha yao. Kulizungumza hili kwa maneno ya sasa ni kuwa wamisri wa kale walikuwa walahidi na kimsingi itikadi ya kabbala yaweza kuitwa secular humanism. Ni muhimu kukumbuka kuwa dhana hizi mbili ulahidi na secular humanism ndizo zilizotoa itikadi ambayo imetawala Duniyani kwa zaidi ya karne mbili zilizopita. Yafaa kuuliza iwapo kuna watu ambao wameziendeleza itikadi za misri za kale na kabbala tangia katikati ya kipindi cha nyuma cha historia hadi leo hii.

Wakati tulipowazungumzia Matempla huko nyuma, tulisema kuwa kundi hili maksusi la makuruseda liliathiriwa na “siri” waliyoikuta Jerusalem, kutokana na siri hiyo wakaachana na Ukirsto na wakaanza kufuata mafundisho ya kichawi. Tukasema kuwa watafiti wengi waliishia kutoa maoni yao kuwa siri hii ilihusiana na kabbala. Kwa mfano katika kitabu chake, Histoire de la Magie (Historia ya uchawi ) mwandishi wa kifaransa, Eliphas Le’vi, anatoa ushahidi wa kina kuwa Matempla walijingiza katika itikadi ya siri ya kabbala, kwamba walifundishwa itikadi hiyo kwa siri. Ndio kusema itikadi hii pamoja na mizizi yake ya misri ya kale ilipandikizwa kwa Matempla kupitia kabbala. Katika kitabu chake Foucault’s Pendulum, mwanafasihi mashuhuri wa Italia, Umberto Eco, naye anausimulia ukweli huu. Katika riwaya yake nzima anasimulia kupitia vinywa vya wahusika wakuu wa riwaya yake kuwa Matempla waliathiriwa na kabbala na kwamba wale makabbala walikuwa na siri ambayo chanzo chake chaweza kuwa Mafirauni wa misri ya kale. Kwa mujibu wa Eco, baadhi ya mayahudi mashuhuri walijifunza siri fulani zilizo toka kwa wamisri wa zamani na baadaye wakazipenyeza katika vitabu vitano vya kwanza vya Agano la kale. Lakini siri hii ambayo ilisambazwa kwa siri ilikuwa ikifahamika kwa wana kabbala peke yao. (zohari, iliyoandikwa Hispania na kuunda kitabu cha msingi cha kabbala inazungumzia siri za vitabu hivi vitano. Baada ya kueleza kuwa Wanakabbala waliisoma siri hii ya Misri ya kale katika vipi hekalu la Suleiman , Eco pia anaandika kuwa Matempla nao wakaisoma siri hii kutoka kwa walimu wa kabbala mjini Jerusalem. Siri hii ilikuwa ikijulikana na kikundi kidogo sana cha walimu wa kiyahudi waliobakia Palestina matempla wakaisoma kutoka kwa walimu hao. Pale matempla walipofuata itikadi mchanganyiko ya wamisri na wakabbala ndipo walipofarakana na dhehebu

la kikiristo lililokuwa likitawala Ulaya. Ulikuwa ni mfarakano ambapo wao walishirikiana na nguvu nyingine kubwa ya mayahudi. Baada ya matempla kutiwa mbaroni kwa amri ya pamoja ya Mfalme wa Ufaransa na Papa mnamo mwaka 1307 , kundi hili likatokomea chini chini lakini athari zake zikabakia, Tena zikawa hatari zaidi na zenye uelekeo madhubuti.

Kama tulivyosema awali idadi ndogo ya Mtempla ilinusurika katika kamata kamata na kukimbilia kwa Mfalme wa Scotland, utawala pekee wa kifalme wa Ulaya ambao haukuyakubali Mamlaka ya Papa. Kule Scotland wakajipenyeza katika jumuiya ya *Wall-builders* na wakaitwaa. Jumuiya zikafuata utamaduni wa Matempla na hivyo mbegu ya frimansori ikapandwa Scotland. Hadi leo hii kanuni kuu ya Frimansori ni ule utaratibu wa kale wa maombi wa Scotland. Kama ilvyofafanuliwa kwa kina katika kitabu kiitwacho *The New Masonic Order*, kuanzia karne ya kumi na nne ndipo yanapoonekana masalia ya Matempla na Mayahudi kadhaa walioshirikiana nao katika vipindi mbalimbali vya Historia ya Ulaya. Bila kutoa maelezo ya kina zifuatazo ni nukta muhimu za utafiti:

-Katika Mji wa Province nchini Ufaransa kulikuwa na kambi ya Matempla waliokimbilia nchini humo. Wakati wa ile kamatakamata Matempla wengi sana walijificha huko. Kielezeo kingine cha eneo hilo ni kuwa hilo ndilo lililokuwa kituo mashuhuri cha Ukabbala barani Ulaya. Province ndipo mahala ambapo fasihi simulizi ya Kabbala ilandikwa katika kitabu.

- Kwa mujibu wa wanahistoria,uasi wa Wakulima nchini Uingereza mwaka 1381 ulichochewa na Jumuiya fulani ya siri. Watafiti wanaoitafiti Historia ya Frimansori wanakubaliana kuwa Jumuiya hii ya siri ilikuwa ya Matempla. Ule uasi haukuwa tu wa kiraia bali pia ulikusudiwa kulishambulia Kanisa Katoliki.-Nusu karne baada ya uasi huu, kasisi mmoja wa Bohemia, John Huss akaanzisha vurugu kulipinga Kanisa Katoliki. Kama kawaida nyuma ya vurugu hizi walikuwepo Matempla. Isitoshe Huss mwenyewe alikuwa akiipenda sana Kabbala. Yeye alikuwa akimpenda sana Avigdor Ben Isaac Kara. Mtu huyu alikuwa Mwalimu mashuhuri wa Kiyahudi katika jamii ya kiyahudi katika mji wa Prague na pia alikuwa Mwanakabbala.

Vielelezo kama hivi vinaonesha kuwa ushirikiano kati ya Matempla na Wanakabbala ulilenga kubadilisha mfumo wa jamii ya Ulaya. Mabadiliko haya yalijumuisha misingi ya utamaduni wa Kikristo ambao ndiyo utamaduni-mama wa Ulaya na badala ya utamaduni huu uwekwe utamaduni uliojengwa kwa msingi wa mafundisho ya kipagani, kama vile Kabbala na baada ya mabadiliko haya, yafuate mabadiliko ya kisiasa. Mifano ni mapinduzi ya Ufaransa na Italia.

Huko mbele tutaona vipindi vya mabadiliko ya Historia ya Ulaya. Katika kila kipindi tutakutana na ukweli kuwa kulikuwa na nguvu iliyotaka kuitenganisha Ulaya na mafundisho ya Kanisa na badala yake iweke itikadi ya Kisekula na hivyo izisambaratishe taasisi zote za dini. Nguvu hii ilijaribu kuichagiza Ulaya kuikubali itkadi iliyorithiwa kutoka Misri ya kale kupitia

Kabbala. Tulikwishaeleza huko nyuma kuwa msingi wa itikadi hii ni dhana hizi mbili; Humanism na Materialism (Utumtu na Ulahidi).

## Mafundisho ya kipagani yalivyoongezwa katika Taurat

NI muhimu kukumbuka kuwa maovu ya Wayahudi wapotevu, yameandikwa katika kitabu kitakatifu cha Mayahudi-Agano la Kale. katika kitabu cha Nehemia ambacho ni kitabu cha historia kilichomo katika Agano la Kale, Wayahudi wanakili dhambi zao na kutubu. Waliokuwa wazawa wa Israel wakajitenga na wageni wote, wakasimama, wakaziungama dhambi zao, na maovu ya Baba zao. Basi wakasimama mahali pao, wakasoma katika kitabu cha Torati ya Bwana, Mungu wao, muda wa robo ya siku; na robo nyingine wakaungama, wakamuabudu Bwana, Mungu wao. Ndipo wakasimama madarajani pa Walawi, Yeshua, na Bani, na Kadimieri, na Shebania, na Bani, na Sherebia, na Bani, na Kenani, wakamlilia Bwana, Mungu wao kwa sauti kuu.

(Wakasema;) Walakini (Baba zetu) hawakutii, wakakuasi, wakaitupa sheria yako nyuma yao, wakawaua Manabii wako walioshuhudia juu yao wapate kuwarejeza kwako; wakatenda machukizo makuu. Kwasababu hiyo ukawatia katika mikono ya adui zao, waliowasumbua; na wakati wa shida yao, walipokulilia, uliwasikia kutoka mbinguni; na kwa wingi wa rehma zako ukawapa waokozi walio waokoa katika mikono ya adui zao. Lakini walipokuwa wamekwisha kustarehe, walitenda mabaya tena mbele zako; kwahiyo ukawaacha katika mikono ya adui zao, nao wakawatawala; hata hivyo waliporejea na kukulia, uliwasikia toka mbinguni, ukawaokoa mara nyingi kwa rehma zako; ukawashuhudia ili uwarudishe tena katika sheria yako; lakini walitakabari, wasisikilize amri zako, bali waka zikhalifu hukumu zako, (ambazo mtu akizitenda ataishi katika hizo) nao wakayaondowa mabega yao, wakafanya shingo zao kuwa ngumu, wasitake kusikiliza. Ila kwa rehema zako nyingi hukuwakomesha kabisa wala kuwaacha; kwa maana wewe u Mungu mwenye neema, Mwenye rehema. Basi sasa, Ee Mungu, Mkuu, mwenye uweza, Mungu wa kuogofya mwenye kushika maagano na rehema, mashaka yote yaliyotupata sisi, wafalme wetu, na wakuu wetu, na makuhani wetu, na manabii wetu, na Baba zetu, na watu wako wote, tangu zamani za wafalme wa Ashuru hata leo, na yasihesabiwe kuwa ni madogo. Lakini wewe u mwenye haki, katika hayo yote yaliyotupata; maana wewe umetenda yaliyo kweli lakini sisi tumetenda yaliyo mabaya; na wafalme wetu, na wakuu wetu, na makuhani wetu, na Baba zetu, hawakushika sheria yako wala hawakusikiliza amri zako na shuhuda zako ulizo washuhudia. Kwa kuwa hawakukutumikia wewe katika ufalme wao, na katika wema wako mkuu uliowapa, na katika nchi ile kubwa yenye neema uliowapa mbele yao, wala hawakughaili na kuacha mabaya yao. (Nehemia 9, 2-4, 26-29-31-35).

Kifungu hiki kinaelezea tamaa ya kurejea katika Imani ya Mungu mmoja ambayo Wayahudi wengi walikuwa nayo, isipokuwa katika kipindi cha historia ya Wayahudi kundi

moja lilimeguka na kupata nguvu kidogo kidogo, na likaja kuwatawala wayahudi na baadaye likaegeuza kabisa dini yenyewe.  Kwasababu hii katika Torati na katika vitabu vingine vya agano la kale kuna masalia yanayotoka katika mafundisho ya Kipagani, na pia kama yaliyotajwa hapo juu yanawasukuma kurejea katika dini sahihi.  Mathalani;

- Katika kitabu cha mwanzo cha Taurati, inasemwa kuwa Mungu aliumba ulimwengu mzima kwa siku sita kutokana na hamna.  Hii ni sahihi na inatokana na ufunuo sahihi.  Lakini, hapo hapo inasema kuwa Mungu alipumzika siku ya saba, huu ni uzushi kabisa.  Ni dhana potofu iliyotoka katika upagani ambao unampachika Mungu sifa za kibinadamu.  Katika aya hii ya Qur'an, Mwenyezi Mungu anasema;

**Na Tumeziumba Mbingu na Ardhi na vilivyomo kati yao katika nyakati sita, wala hayakutugusa machovu (50:38).**

Katika sura nyingine za Taurati kuna staili ya uandishi ambayo ni ya utovu wa heshima kwa Mungu, hasa hasa katika zile sehemu ambazo sifa za kibinadamu anapewa Mungu.  Imani hizi potofu za kulinganisha udhaifu wa kibinadamu ndizo imani ambazo wapagani walikuwa nazo kwa miungu yao bandia. Maneno mengine ya kufuru ni yale yanayodai kuwa Yakobo, Baba wa Waisrael alipigana myeleka na Mungu, na akashinda.  Ni wazi kabisa hiki ni kisa cha kutungwa ili kuwatukuza Waisrael, ni mwigo kutoka katika jamii za wapagani.  Katika Agano la kale kuna mtindo wa kumuelezea Mungu kama Mungu wa utaifa – yaani Mungu wa Waisrael peke yao.  Lakini Mungu ni Mola wa Ulimwengu na viumbe vyote.  Dhana hii ya dini ya utaifa, katika Agano la kale inafanana na dhana za kipagani ambapo kila kabila linaabudia Mungu wake.

-Katika baadhi ya vitabu vya agano la kale (mfano, Yeshua)  amri zinatolewa kufanya maovu dhidi ya watu wasiokuwa wayahudi.  Mauaji ya halaiki yanaamrishwa bila kujali wanawake, watoto wala wazee.  Mwenendo huu wa kinyama uko kinyume kabisa na sheria ya haki ya Mungu, bali badala yake unarandana na ushenzi wa tamaduni za kipagani za kuabudia Mungu bandia wa vita.

Mawazo haya ya kipagani ambayo yametumbukizwa katika Taurati yumkini yana chanzo chake.  Lazima kuna mayahudi ambao walifuata mila isiyokuwemo katika Taurati. Wakaishika na kuitukaza mila hiyo.  Baadaye wakatumbukiza katika Taurati mawazo yaliyotoka katika mila hii ambayo wao waliyaunga mkono.  Chimbuko la mila hii linaanzia nyuma kabisa kwa makuhani wa Misri (Wachawi katika utawala wa Firauni ).

Kwa kweli ni Kabbala iliyorithiwa na wayahudi wengi.  Kabbala ilikuwa na sura ambayo iliziwezesha itikadi za Wamisri na Wapagani kujipenyeza katika dini ya uyahudi na kustawi ndani yake.  Wahusika wa Kabbala  hapana shaka wanadai kuwa Kabbala inafafanua tu kwa

kina siri zilizofichikana kabisa katika Taurati, lakini , kwa kweli kama asemavyo mwanahistoria wa kiyahudi aliyezungumzia Kabbala kuwa Kabbala ni sumu isiyotambulika ambayo imeingiya katika dini ya uyahudi na kuiathiri kabisa. Hapo sasa inawezekana kukuta ndani ya Kabbala masalia ya itakdi ya Ulahidi ya Wamisri wa zama za kale.

Kabbala – Itikadi inayopingana na dhana ya kuumbwa kwa ulimwengu.

Katika Qur'an , Mwenyezi Mungu anabainisha kuwa Taurati ni kitabu cha Mungu ambacho kilishushwa kama muongozo kwa Wanadamu,

**Hakika tuliteremsha Taurati yenye uongozi na nuru; ambayo kwayo Manabii waliojisalimisha (kwa Mwenyezi Mungu waliwahukumu Mayahudi, na Watawa na Maulamaa pia (walihukumu kwa hiyo Taurati), kwasababu walitakiwa kuhifadhi kitabu (hicho) cha Mwenyezi Mungu; nao walikuwa mashahidi juu yake. (5:44).**

Kwahiyo, Taurati, kama ilivyo Qur'an, ni kitabu chenye elimu na amri zinazohusiana na Tawhiid yanayoelezya kuwepo kwa Mwenyezi Mungu na upweke wake, sifa zake, kuumbwa kwa wanadamu na viumbe wengine, lengo la kuumbwa kwa binadamu, na sheria za maadili za Mwenyezi Mungu kwa wanadamu. Hata hivyo ile Taurati ya asili haipo tena hivi leo. Tuliyonayo hivi leo ni Taurati iliyoandikwa upya na kuhujumiwa na mikono ya binadamu. Kuna nukta muhimu kuwa ile Taurati ya asili na Qur'an zinashabihiana, Mwenyezi Mungu anatambuliwa kama muumba. Anatambuliwa kama aliyetakasika na aliyeepukana na mapungufu yote na amekuwepo bila mwanzo. Chochote minghairi yake ni kiumbe chake. Yeye ndiye aliyeumba ulimwengu wote, maumbile ya angani, maada isiyo na uhai, binadamu na viumbe vyote hai. Mungu ni mmoja tu. Wakati huu ukiwa ndio ukweli halisi, kuna maelezo tofauti kabisa yanayokutikana katika Kabbala, ambayo ni sumu iliyopenya katika mishipa ya uiyahudi na kuuathiri kabisa. Mafundisho yake juu ya Mungu yanapingana kabisa na ule ukweli halisi juu ya maumbile unaokutikana katika ile Taurati ya asili na katika Qur'an.

Katika moja ya maandiko yake juu ya Kabbala, mtafiti mmoja wa Amerika, Lance S. Owens anatoa fikra yake juu ya vyanzo vya itikadi hii ambapo imani ya Kabbala imesababisha dhana kadhaa kuhusu Mungu, nyingi miongoni mwa hizo zimetoka kabisa katika mtazamo wa dini. Msingi mkuu wa imani ya Waisrael ulikuwa ni kalima kuwa Mungu wetu ni mmoja. Lakini Kabbala ikadai kuwa wakati Mungu akiishi katika umbile la peke yake ambalo katika Kabbala linaitwa Ein Sof asiye na udhaifu – upweke huu usiojulikana lazima utakuwa umeanzia katika maumbile mengi ya kiungu. Yaani kundi la Miungu. Miungu hii ambayo mwana Kabbala aliita Sefiroth yaani sura au nyuso za Miungu. Njia ambayo Mungu alitokea katika umoja usioeleweka na kuingia katika wingi ilikuwa ni siri ambayo wana Kabbala walihangaika kuitafuta. Ni dhahiri hii sura ya Miungu mingi inakubaliana na madai ya washirikina. Siyo tu Mungu alikuwa katika wingi katika itikadi ya Kikabbala bali hata kule kutokea kwake mwanzoni katika upweke usiojulikana kulichukuwa sura mbili ya kiume na ya kike, Baba na Mama, Hokhmah na Binah hizi ndizo sura za mwanzo za Mungu. Wafuasi wa

Kabbala walikuwa wakitumia tamathali za kijinsia kuelezea jinsi maingiliano ya kijinsia ya Hokhmah na Binah yalivyozaa maumbile mengine.

## Dhana ya 'humanism'

Yasadikiwa na wengi kuwa Humanism ndio itikadi madhubuti. Inampandikiza mtu hisia za upendo, utulivu na Udugu. Lakini kifalsafa dhana hii ina maana kubwa zaidi. Humanism ni utaratibu wa fikra ambao unaichukulia dhana ya ubinadamu kama ndio msingi na lengo lake kuu. Kwa maneno mengine inawataka watu wajitenge mbali na Mungu, Muumba wao na washughulike na maisha yao na utu wao. Kamusi ya Kiingereza iitwayo Common dictionary inaliainisha neno humanism kama ni mfumo wa itikadi uliojengwa juu ya msingi wa maadili, sifa na tabia ambazo zinaaminika kuwa bora zaidi kwa vigezo vya binadamu wenyewe bila kutegemea muongozo wowote wa Kiungu.

Ainisho la wazi zaidi la humanism limetolewa na wale wanaounga mkono itikadi hii. Mmoja kati ya wapiga debe wakuu wa dhana ya humanism ni bwana Corliss Lamont. Katika kitabu chake kiitwacho The philosophy of Humanism, mwandishi huyu ameandika hivi: Kwa ujumla Humanism inaamini kuwa maumbile yanatokana na mkusanyiko wa vitu halisi ambavyo msingi wake ni nguvu ya maada. Maada ndio msingi wa Ulimwengu na kwamba nguvu za Kiungu hazipo. Dhana ya nguvu za Kiungu, kwa upeo wa binadamu, haina uthibisho. Kwamba watu hawana roho za kudumu milele yaani zisizo kufa na ulimwengu kwa ujumla hauna Mungu aliyeuumba wala Mungu wa milele.

Kama tunavyojionea wenyewe katika nukuu hizo, itikadi ya humanism karibu inafanana kabisa na Itikadi ya atheism, na ukweli huu unakubaliwa bila ubishi na wanahumanisti. Kulikuwa na ilani mbili muhimu zilizochapishwa na wanahumanisti katika karne iliyopita. Ilani ya kwanza ilichapishwa mwaka 1933, na ikapitishwa na watu muhimu wa wakati huo. Miaka arobaini baadaye, mnamo mwaka 1973, ilani ya pili ya wanahumanisti ilichapishwa. Ilani hii iliithibitisha ile ya kwanza lakini ikatiwa nyongeza kufuatia hatua fulani za maendeleo ambazo zilipigwa wakati huo. Maelfu ya wanafikra, Wanasayansi, Waandishi na Wanahabari walisaini ilani ya pili ambayo inaungwa mkono na chama cha harakati za wana humanisti wa Amerika.

Tunapoziangalia ilani hizi, tunakuta kuwa katika kila ilani kuna huu msingi mmoja mkuu, ambao ni Dhana ya atheism ambayo inasema ulimwengu na wanadamu hawakuumbwa bali wanaishi kwa kujiendesha wenyewe, kwamba binadamu hawawajibiki kwa mamlaka yoyote isipokuwa kwao wenyewe, na kwamba Imani juu ya Mungu imedumaza maendeleo ya watu na jamii. Kwa mfano vipengele sita vya kwanza vya ilani ya kwanza vya wanahumanist ni hivi vifuatavyo:

Mosi:Wanahumanist wanaitakidi kuwa ulimwengu unajiendeshea wenyewe maisha yake na haukuumbwa.

Pili: Dhana ya humanism ina itakidi kuwa Mtu ni sehemu ya maumbile na kwamba ameibuka kutokana na mfumo unaojiendesha wenyewe.

Tatu: wakishikilia mtazamo wa maisha wakioganiki, Wanahumanisti wanaona kuwa dhana ya pande mbili za nafsi na mwili lazima ipingwe kabisa.

Nne:Itikadi ya humanism inatambua kuwa utamaduni wa kidini wa mtu na ustaarabu wake kama ulivyoelezwa na historia ni zao la hatua za polepole za maendeleo zitokanazo na mahusiano baina yake na mazingira yake na urathi wa jamii yake. Mtu anayezaliwa katika utamaduni fulani kwa kiasi kikubwa anajengeka kwa utamaduni huo.

Tano: Dhana ya humanism inatangaza kuwa maumbile ya ulimwengu yalioelezwa na sayansi ya leo yanatupilia mbali nguvu yoyote ya mbinguni kuhusiana na maadili ya binadamu.

Sita: Tunaamini kuwa dhana za theism, deism, modernism na aina kadhaa za itikadi mpya zimepitwa na wakati.

Katika vipengele hivyo tunaiona wazi nafasi ya falsafa ya common ambayo inajidhihirisha yenyewe kwa majina ya materialism, Darwinism, atheism na agnosticism. Katika kipengele cha kwanza dhana ya ulahidi ya uhai wa milele wa ulimwengu imewekwa wazi.

Kipengele cha pili kinasema kuwa binadamu hawakuumbwa, hivi ndivyo inavyosema nadharia ya evolusheni. Kipengele cha tatu kinakanusha kuwepo kwa roho kikidai kuwa viumbe wanatokana na maada. Kipengele cha nne kinapendekeza mageuzi ya kiutamaduni na kinakanusha kuwepo kwa silika aliyopewa bindamu (Silika maalum ya binadamu katika maumbile).

Kipengele cha tano kinakanusha mamlaka ya Mungu juu ya ulimwengu na walimwengu na kipengele cha sita kinakataa Imani juu ya Mungu. Itakumbukwa kuwa madai haya ndiyo yale yale ya zile duru zenye chuki na dini sahihi. Sababu ni kuwa dhana ya humanism ndio msingi mkuu wa hisia zote zinazopinga dini. Hii ni kwa sababu dhana hii inasema kuwa mtu ataachwa hivyo hivyo bila kuhesabiwa. katika historia yote. Huu ndio umekuwa msingi wa madai ya kumkanusha Mungu. Katika aya moja ya Qur'an Mwenyezi Mungu anasema:

Je! Anafikiri binadamu kuwa ataachwa bure, (asipewe amri za Mwenyezi Mungu wala makatazo yake)? Je! Hakuwa tone la manii lililotonwa? Kisha akawa kidonge cha damu, kisha akamuumba na akamsawazisha (kuwa mwanadamu kamili)? Kisha akamfanya namna mbili, Mwanaume na Mwanamke. Je ! Hakuwa huyo ni muweza wa kuhuisha wafu?

Mwenyezi Mungu anasema watu hawakuachwa tu hivi hivi na anawakumbusha kuwa wao ni viumbe vyake. Hii ni kwa sababu pale mtu anapotanabahi kuwa yeye ni kiumbe wa Mungu, basi aelewe kuwa haishi bila ya kuangaliwa bali anawajibika kwa Mwenyezi Mungu.

Kwa sababu hii, dai kuwa binadamu hawakuumbwa ndio limekuwa msingi wa falsafa ya humanism Vipengele viwili vya ilani ya kwanza ya wanahumanisti vinatoa maelezo ya itikadi

hii.  Isitoshe wana humanisti  wanashikilia kuwa Sayansi inaunga mkono madai haya. Lakini ni waongo.  Tokeya ilani ya kwanza ya wanahumanisti ilipochapishwa Premesia mbili ambazo wanahumanisti wameziainisha kama hakika za kisayansi, kwamba ile dhana kuwa ulimwengu ni wa milele pamoja na nadharia ya evolusheni zote zimesambaratika.

1. Dhana kuwa Ulimwengu ni wa milele ilivunjiliwa mbali na mlolongo wa vumbuzi za angani zilizofanywa pale ilani ya kwanza ya wanahumanisti ilipokuwa inaandikwa..  Vumbuzi kama vile ulimwengu kutanuka, chanzo cha mionzi ya angani na mahesabu ya uwiano ya Haidrogen hadi helium, zimeonyesha kuwa ulimwengu ulikuwa na chanzo chake na kwamba uliibuka kutokana na hamna  takribani miaka bilioni 15-17 iliyopita kwa mlipuko mkubwa ulioitwa  Big Bang.

Ingawaje wale wanaounga mkono falsafa  ya kihumanisti na kilahidi walikataa kukubali nadharia ya Big Bang lakini hatimaye walishindwa kabisa.  Kutokana na  ushahidi wa kisayansi ambao umejitokeza, jamii ya wanasayansi hatimaye imeikubali nadharia ya Big Bang kwamba ulimwengu ulikuwa na mwanzo wake na hivyo wanahumanisti hawana hoja.  Hivyo mwanaatheist Antony Flew alilazimika kukiri hivi:

……………….Sasa nitaanza kukiri kuwa mwanaatheisti lazima atatizike kwa hizi fikra za sasa za maumbile.  Kwani inaonekana kuwa Wanakosmolojia wanatoa ushahidi kuwa kile alichodai Mtakatifu Tomas hakiwezi kuthibitishwa kifalsafa hii ikiwa na maana kuwa ulimwengu ulikuwa na mwanzo wake.

2. Nadharia ya evolusheni ambayo ndiyo hoja kuu iliyomo katika ilani ya kwanza ya humanism ikaanza kupoteza nguvu  miongo kadhaa baada ya kuandikwa kwake. Inafahamika hivi leo ubabaishaji uliofanywa na wana evolusheni na wakiatheisti (na bila shaka wakihumanisti), kama vile A.I. Oparin na J.B.S. Haldane katika miaka ya thelathini kuhusiana na chanzo cha uhai hauna msingi wa kisayansi.

3. Viumbe haviwezi kutokea kwa bahati nasibu kutokana na maada isiyo na uhai kama ilivyodaiwa katika ubabaishaji huu.  Kumbukumbu ya mabaki ya kale inaonyesha kuwa viumbe hai hawakuwa hivi walivyo kutokana na hatua za mabadiliko madogo madogo bali walitokea kwa pamoja wakiwa na sifa zao mbali mbali.

4. Ukweli huu umekubaliwa na wana evolusheni wenyewe  tangia miaka ya Sabini.  Sayansi ya viumbe hivi leo imebainisha kuwa viumbe hai hawakutokana na bahati nasibu  na kanuni za maumbile bali katika kila kiumbe kuna mfumo madhubuti unaothibitisha kuwa Msanii mwenye hekima ndiye aliyeviumba.  Ukitaka maelezo zaidi rejea kitabu kiitwacho, Darwinism Refuted.

Zaidi ya hivyo dai la uongo kuwa imani ya dini ndio sababu inayowakwaza watu kuendelea na kuwatumbukiza katika mifarakano limetupiliwa mbali na ushahidi wa kihistoria. Wanahumanisti wamedai kuwa kuondolewa kwa imani ya dini kutawaletea watu furaha na faraja.  Hata hivyo hali imekuwa kinyume cha mambo.

Miaka sita baada ya kuchapishwa kwa ilani ya humanism, vita vya pili vya Duniya vikalipuka, hii ni kumbukumbu ya misiba mikubwa iliyoletwa na itikadi za kifashisti za

kisekula. Itikadi ya Humanism ya Ukomunisti ikachipuka, kwanza ilianzia kwa watu wa Urusi kisha kwa watu wa China, Cambodia, Vietnam, Korea kaskazini, Cuba na katika baadhi ya nchi za afrika na Latin Amerika, kulikuwa ni ushenzi usio na mfano.

Jumla ya watu Milioni 120 waliuawa na tawala za Kikomunisti au jumuiya za kikomonisti. Ni dhahiri kuwa kundi la wanahumanisti wa Magharibi (mifumo ya kibepari) nalo limeshindwa kuleta amani na furaha katika jamii zao na katika maeneo mengine ya Duniya.

Kuvunjwa kwa hoja ya humanism juu ya dini pia kumedhirishwa katika fani ya saikolojia. The Freudian myth, msingi wa dhana ya kiatheist tokea mwanzoni mwa karneya ishirini imebatilishwa na matokeo ya uchunguzi. Patric Glynn wa Chuo Kikuu cha George Washington anaufafanua ukweli huu katika kitabu chake kinachoitwa God: The Evidence, The Reconciliation of Faith and Reason in a PostSecular World.

## Matempla na Misri ya zamani

Wanachoelewa wanahistoria wengi kuhusiana na Frimansori ni kuwa chimbuko la Jumuiya hii ni vita vya msalaba. Ukweli ni kuwa ijapokuwa Mansori , kimsingi iliasisiwa na kutambuliwa rasmi nchini Uingereza mwanzoni mwa karne ya kumi na nne, mizizi ya Jumuiya hii imeanzia katika vita vya msalaba mnamo karne ya kumi na mbili. Katika mkasa huu mashuhuri ndimo linamokutwa kundi la wanamgambo wa vita hivyo vya msalaba waliojulikana kama Knights Templar au Templars. Katika mfululizo wetu tumekuwa tukitumia tafsiri isiyo rasmi ya majina hayo ambayo ni Matempla. Kwa mapana na marefu historia ya Matempla imeelezewa katika kitabu kiitwacho The New Masonic Order. Hivyo basi katika mfululizo huu tumeielezea kwa mukhtasari tu. Kwani kuichambua kwetu mizizi ya Mansori na athari zake katika Duniya kwatosha kabisa kufichua maana nzima ya Frimansori. Ijapokuwa baadhi ya watu wanashikilia kuwa vita vya msalaba vilikuwa ni vita vilivyofanywa kwaajili ya Imani ya Kikristo, lakini kimsingi vita hivyo vilifanywa kwa maslahi ya kiuchumi. Katika kile kipindi ambacho Ulaya ilikuwa katika hali ya umasikini na ufukara, Waislamu wa mashariki ya kati walikuwa katika hali bora ya kiuchumi. Mafanikio hayo ya kiuchumi pamoja na utajiri wa Mashariki ya kati uliwatamanisha sana wazungu wa Ulaya.

Uchu wa utajiri waliokuwanao Wazungu hao wa Ulaya ukavikwa sura ya kidini na kupambwa kwa sifa za Ukristo, japo kwa kweli wazo hasa la kuanzisha vita hivyo lilitokana na tamaa ya maslahi ya kiDuniya. Ndio sababu kukawa na mabadiliko ya ghafla katika sera za Wakristo wa Ulaya. Wakaachana na zile sera za amani na utulivu walizokuwa nazo katika nyakati za mwanzo za historia yao na badala yake wakachukuwa mwelekeo wa vita vya kijeshi. Mwanzilishi wa vita vya Msalaba alikuwa Papa Urban wa Pili au Pope Urban II. Papa huyu aliitisha mkutano wa baraza lake, Council of Clermont mnamo mwaka 1095. Katika mkutano huo ile itikadi ya awali ya utulivu waliyokuwanayo Wakristo ikatupiliwa mbali. Vikatangazwa

vita vitakatifu kwa shabaha ya kuzipora nchi takatifu kutoka mikononi mwa Waislamu. Kufuatia tangazo hili la vita, Jeshi kubwa la wanamgambo walioitwa Crusaders likaundwa. Kwa kiswahili tutatumia neno makruseda hapa na pale katika kutafsiri neno hilo Crusaders. Jeshi hilo lilijumuisha askari waliokuwa na mafunzo ya kijeshi pamoja na makumi kwa maelfu ya watu wa kawaida. Wanahistoria wanaamini kuwa hila ya Papa Urban wa pili kuanzisha vita hivyo ilitokana na tamaa yake ya kushinda kinyang'anyiro cha Upapa.

Isitoshe Wafalme, wana wa wafalme, watawala na watu wengine wa Ulaya waliupokea wito wa Papa kwa furaha kwani walikuwa na malengo ya kujipatia maslahi ya kiDuniya kama alivyosema bw. Donald Queller wa Chuo kikuu cha Illinois, kwamba mashujaa wa Ufaransa walitaka tu kujiongezea nchi. Nao wafanyabiashara wa Italia walitumai kupanua biashara yao mashariki ya kati…….. Idadi kubwa ya makapuku au walala hoi walijiunga na misafara hii ya kijeshi ili kukimbia maisha magumu waliokuwa wakiishi makwao. Kote lilikopita, Jeshi hili la wachumia tumbo lilichinja Waislamu na hata mayahudi kwa tamaa ya kujipatia dhahabu na vito vya thamani. Makruseda hawa walitumbua matumbo ya watu waliowaua ili eti watowe dhahabu na madini ya thamani ambayo wahanga huenda waliyameza kabla ya kufa. Tamaa ya mali iliwazidia mno Makruseda kiasi ambacho hawakusita kuvamia na kuteka jiji la Wakristo la Constantinople (Istanbul) katika vita ya nne ya Msalaba. Baada ya safari ngumu na ndefu na baada ya kufanya unyang'anyi na uporaji sambamba na mauaji ya Waislamu, kundi hili la wauaji waloitwa Makruseda likafika Jelusalem mnamo mwaka 1099. Makruseda hawa waliingia katika jiji hili baada ya kulizingira kwa takriban majuma matano. Walifanya ushenzi wa kupindukia. Waislamu na Mayahudi wote wa jiji hilo walifyekwa mapanga. Kwa maneno ya mwana historia mmoja, Makruseda waliua Warabu, Waislamu na Waturuki wote waliowakuta humo…Wanaume kwa Wanawake. Mmoja wa Makruseda hao, bwana Raymond alijitapa hivi kwa hujuma waliyoifanya:

Baadhi ya watu wetu walifyeka vichwa vya maadui zao, wengine wakawachoma mishale, wengine waliwatesa sana kwa kuwatupa maadui kwenye moto. Malundo ya vichwa, mikono na miguu yalionekana katika mitaa ya jiji. Ilibidi mtu akanyage miili ya watu na farasi ili aweze kupita njia. Lakini yote haya ni madogo kulinganisha na yale yaliyotokea kwenye hekalu la Suleiman mahala ambapo ibada za kidini hufanyika mara kwa mara…Kuanzia ndani ya hekalu hadi kwenye baraza ya hekalu hilo, watu walipita kwenye madimbwi ya damu ambapo damu ilizamisha miguu yao hadi magotini. Kwa muda wa siku mbili tu jeshi la makruseda liliwaua kinyama Waislamu wapatao 40,000. Baada ya hapo Makruseda wakaifanya Jelusalem kuwa mji wao mkuu na wakaanzisha utawala wa kifalme wa kilatini uliojitandaza kutoka mipaka ya Palestina hadi Antiokia. Baadaye tena makruseda wakaanzisha mapambano ya kuimarisha mamlaka yao mashariki ya kati. Ili kuidumisha dola waliyoianzisha, ilibidi waiunganishe. Katika kutimiza lengo hilo wakaanzisha Komandi za Kijeshi ambazo hazikuwa na mfano wake hapo kabla. Watu waliounda komandi hizi walitokea Ulaya kwenda Palestina na wakaishi katika majengo mithili ya yale ya Watawa ambamo

walipatiwa mafunzo ya kijeshi ili kupambana na Waislamu. Mojawapo ya Komandi hizi ilikuwa tofauti kabisa na nyinginezo. Yenyewe ilibadilika muundo na kubadili mwelekeo wa historia. Komandi hii ilikuwa ya Matempla.

## Matempla

Watu waliounda Komandi hizo walitoka Ulaya kuja Palestina na wakaishi katika nyumba za kitawa ambamo walipewa mafunzo ya kijeshi ili kupambana na Waislamu. Kundi moja miongoni mwa vikundi hivi lilitofautiana na makundi mengine. Lenyewe likabadilika muundo na kubadili mwelekeo wa historia. Kundi hili lilikuwa la Matempla. Matempla au kwa jina kamili askari dhaifu wa Yesu Kristo na hekalu la Selemani ni kundi lililoanzishwa mwaka 1118 yaani miaka 20 baada ya Makruseda kuitwaa Jelusalem. Waanzilishi wa kundi hili walikuwa Askari wa Ufaransa, Hugh dee Payens na mwenziye Godfrey d St. Omer. Mwanzoni kabisa kundi hili lilikuwa na watu tisa lakini baadaye likazidi kukuwa. Sababu iliyowapelekea kujiita jina hilo (Matempla) ambalo linatokana na Nomino Temple ni kuwa sehemu waliyochaguwa kuwa ngome yao ni mahali ambapo lipo hekalu la Selemani (Temple of Solomon) au pia panaitwa Temple Mount (kilima cha hekaluni). Japo Matempla walijiita "askari dhaifu" lakini kwa kipindi kifupi tu wakawa matajiri wakubwa. Mahujaji wa Kikristo waliotoka Ulaya kuja Palestina wote walikuwa chin i ya himaya ya kundi hili na kutokana na fedha zao wakatajirika sana. Mbali na hivyo, kwa mara ya kwanza kabisa matempla wakaanzisha mfumo wa hundi na karadha, sawa na ule wa Benki. Kwa mujibu wa waandishi wa kingereza, Michael Baigent na Richard Leigh, matempla ndio walioanzisha mfumo wa kibepari wa zama za kati na ndio waliotoa mwelekeo wa kuanzishwa mfumo wa sasa wa Benki unaojengeka kwa misingi ya riba. Walikuwa ni hawa Matempla waliohusika kwa kiasi kikubwa na mashambulizi ya makruseda na mauaji ya Wailsmu. Kwas sababu hii Kamanda mkuu wa Waislamu Saladin aliyelishinda Jeshi la Makruseda katika vita vya Hattin 1887, na baadaye kuikomboa Jelusalem, aliwahukumu Matemplsa adhabu ya kifo kwa mauaji waliyoyafanya, na akawasamehe Wakristo wengi sana. Ingawaje waliipoteza Jelusalem na kupata madhara makubwa, bado matempla waliendelea kuwepo. Na licha ya kupungua kwa idadi ya Wakristo nchini Palestina, Matempla waliimarisha mamlaka yao barani Ulaya kuanzia Ufaransa hadi nchi nyingine hivyo pakawa na dola ndani ya dola. Hapana shaka kuwa nguvu zao za kisiasa ziliwaweka roho juu wafalme wa Ulaya. Aidha kulikuwa na jambo jingine ambalo liliweka Taasisi ya Ukasisi katika hali mbaya. Kundi hili la matempla lilianza kidogo kidogo kujitoa katika Imani ya Kikristo. Na wakati walipokuwa bado wapo Jelusalem, walianza kufuata itikadi za ajabu za kikuhani. Pia kulikuwa na uvumi kuwa walikuwa wanafuata utaratibu wa ajabu wa sala unaorandana na Itikadi hizo. Hatimaye, mnamo mwaka 1307, Mfalme wa Ufaransa Filip le Bel aliamua kuwakamata wafuasi wa kundi hili. Baadhi yao wakafau lu kutoroka lakini wengi wao walitiwa mbaroni. Papa Clement wa tano, naye akaunga mkono hatua hiyo. Kufuatia kipindi

kirefu cha mahojiano na mashtaka, matempla wengi walikiri kufuata imani mpya kwamba waliikana Imani ya Kikristo na kumtukana Yesu katika mikutano yao.

Mwishowe viongozi wa Matempla ambao waliitwa “Mabwana wakubwa” kuanzia yule kiongozi wao mkubwa kabisa bwana Jacques de Molay wote walinyongwa kwa amri ya Mfalme na Kanisa mwaka 1314. Wengi miongoni mwao walifungwa Jela na kundi likasambaratika na kutokomea. Baadhi ya Wanahistoria wanakasumba ya kuielezea kesi ya Matempla kama ni njama ya Mfalme wa Ufaransa na kuwatoa hatiani Matempla. Lakini tafsiri hii ya mambo ina upungufu katika vipengere kadha wa kadha. Mwanahistoria mashuhuri wa Uingereza Nesta H Webster ambaye ana ufahamu mkubwa wa historia ya mambo ya siri anavichambua vipengele hivi katika kitabu chake, *Secret Societies and Subversive Movements*.

Kwa mujibu wa mwanahistoriya huyu ile kasumba ya kuwaondoa hatiani Matempla kwa mambo ambayo wenyewe walikiri kuyafanya katika kile kipindi cha mashtaka haina mashiko. Mosi wakati wa mahojiano, si matempla wote walioteswa licha ya kukabiliwa na shitka moja. Vyovyote iwavyo kesi ya Matempla ilikwisha sambamba na kukomeshwa kwa kundi lao. Lakini, ijapokuwa kundi hili lilikoma rasmi hata hivyo halikutoweka kabisa. Katika ile kamata kamata ya kushitukiza mwaka 1307, baadhi yao walinusurika. Kwa mujibu wa tasnifu zilizoegamia nyaraka mbali mbali za kihistoria, idadi ndogo ya matempla ilipata hifadhi katika utawala pekee wa kifalme barani Ulaya ambao haukutambua mamlaka ya Kanisa Katoliki katika karne ya 14, huo ni utawala wa Scotland. Huko walijikusanya upya chini ya hifadhi ya mfalme wa nchi hiyo, Robert The Bruce. Baada ya muda fulani wakabuni mbinu muafaka ya kujificha ili waendelee kuwepo kwa siri. Wakajipenyeza katika jumuiya moja kubwa kwenye visiwa vya Uingereza- Wall builders’lodge na baadaye wakapata mamlaka kamili ya kudhibiti Maskani za Jumuiya hiyo. Mwanzoni mwa zama hizi, jumuiya hii ikabadili jina lake, sasa ilijiita “Masonic Lodge.” Kaida ya Scotland ndio tawi kongwe kabisa la Masonri ambalo limeanza tokea karne ya 14 kwa wale Matempla waliopata hifadhi nchini Scoland. Kwa kifupi matempla hawakutoweka moja kwa moja falsafa yao, Imani zao na Ibada zao bado zingalipo chini ya mwamvuli wa Friimansuri. Dhana hii inathibitishwa na ushahidi mwingi wa kihistoria na inakubaliwa na wanahistoria wengi wa Magharibi wale wa Friimansuri na wasio Friimansori. Katika kitabu, *The New Masonic Order* ushahidi huu umeelezwa kwa kina.

Jarida liitwalo Mimar sinan linaelezea uhusiano kati ya lile kundi la Mtempla na Frimansori kwa maneno yafuatayo:

Mnamo mwaka 1312 pale Mfalme wa Ufaransa alipolikomesha kundi la matempla kwa shinikizo la kanisa, harakati za matempla hazikukomeya hapo. Matempla wengi sana walijificha katika maskani za Frimansori za Ulaya. Kiongozi wa Matempla, Mabeignac pamoja na wafuasi wengine wachache walipata hifadhi nchini Scottland wakijificha chini ya jumuiya ya Wall builder kwa kutumia jina la Macbenach.

Mfalme wa Scotland Robert the Bruce akawakaribisha na kuwaruhusu kujijengea nguvu kubwa katika maskani za Masoni nchini humo. Matokeo yake maskani hizo zikajipatia umuhimu mkubwa kutokana na kazi zao za ufundi na mawazo yao. Hivi leo Frimansori wanalitumia kwa heshima jina la Macbenach. Masoni wa Scotland waliorithi mila ya matempla wakaenda nayo ufaransa miaka mingi baadaye na huko wakajenga msingi wa Kaida (rite) ijulikanayo kama Kaida ya Scotland (Scottish Rite). Aidha Jarida hilo limetoa maelezo mengi kuhusiana na uhusiano baina ya Matempla na Frimansori. Katika makala yenye kichwa "Templars and Freenasonry" inaelezwa kuwa sala za sherehe za uzinduzi wa ile Komandi ya Matempla ni sawa kabisa na zile za Frimansori hivi leo. Kwa mujibu wa makala hiyo hiyo, kama ilivyo kwa Mansori, wafuasi wa kundi la Matempla nao pia walikuwa wakiitana kwa jina la Brother (ndugu).

Katika sehemu ya mwisho ya makala hiyo tunasoma haya yafuatayo:

Kundi la Matempla na jumuiya ya Masoni ni pande mbili ambazo zimeathiriana kwa kiasi kikubwa. Hata sala za washirika hawa zinalingana zikiwa zimeigwa kutoka kwa matempla. Kwa ajili hii Masoni, kwa kiasi kikubwa wanafanana na matempla na hivyo yaweza kusemwa kuwa ile inayoonwa kama itikadi ya siri ya masoni imerithiwa kutoka kwa Matempla. Hivyo inadhihirika wazi kuwa mizizi ya frimansori inaanzia kwa Matempla na kwamba Masoni wamefuata falsafa ya matempla. Masoni wenyewe wanakubaliana na jambo hili. Lakini hapa, jambo muhimu kwetu ni chanzo cha falsafa hii. Kuna maswali haya; kwa nini matempla waliachana na Ukristo na kuwa kundi lenye itikadi mpya? Nini kilichowapelekea kufanya hivyo? Kwanini walibadilika kule Jelusalem? Kupitia shirika la Masonri kumekuwa na athari gani ulimwenguni kutokana na falsafa hii iliyofuatwa na Matempla?

## Matempla na Kabbalah

Kitabu kiitwacho The Hiram Key kilichoandikwa na Masoni wawili Christopher Knight na Robert Lomas kinafichuwa mambo muhimu kuhusu mizizi ya frimansori. Kwa mujibu wa waandishi hawa, ni dhahiri kuwa Mansonri ni muendelezo wa Matempla. Mbali na hivyo waandishi hawa pia wamevitafiti vyanzo vya Matempla. Kwa mujibu wa tasnifu yao, Matempla walibadilika kwa kiasi kikubwa wakati walipokuwa Jerusalem. Badala ya Ukristo, Matempla walifuata itikadi nyingine. Katika mabadiliko haya kuna siri kubwa ambayo Matempla waliigundua katika hekalu la Selemani kule Jerusalem.

Waandishi hawa wamefafanua kuwa Matempla walitumia kisingizio cha kuwalinda mahujaji wa Kikristo waliokuwa wakitembelea Palestina kwa minajili ya kufikia malengo mengine kabisa:

Hakuna ushahidi wowote kuwa Matempla hawa waliwahi kutoa ulinzi wowote kwa mahujaji hao bali badala yake tunaona kuwa kuna ushahidi kamili kuwa walikuwa wakifanya kazi kubwa ya kuchimba Magofu ya hekalu…

Si waandishi hawa pekee waliogundua jambo hili. Mwana historia wa Kifaransa Gaetan Delaforge naye anazungumzia jambo hilo hilo:

Kazi kubwa ya wale Matempla tisa ilikuwa ni kufanya utafiti katika eneo lote ili kupata masalio na maandiko yenye maudhui juu ya tamaduni za siri za dini ya Uyahudi na Misri ya zamani.

Mwishoni mwa karne ya 19 Charles Wilson alianza kufanya utafiti wa mambo ya kale mjini Jerusalem, akatoa maoni yake kuwa Matempla walikwenda Jerusalem kwa lengo la kutafiti mabaki ya hekalu. Wilson aliona alama ya chimba chimba na fukuwa fukuwa chini ya misingi ya hekalu na akasema kuwa haya yalifanywa kwa zana za Matempla. Zana hizi hadi leo zipo katika hifadhi ya Robert Brydon ambaye anamiliki nyaraka nyingi zenye maelezo kuhusu matempla.

Waandishi wa kitabu cha Hiram key wao wanadai kuwa chimba chimba hii ya Matempla haikutoka kapa (haikuishia patupu), kwamba Matempla waligundua mambo fulani ambayo yalibadili mtazamo wao juu ya ulimwengu. Aidha watafiti wengi wanakubaliana na jambo hilo. Lazima kuna jambo fulani tu ambalo liliwapelekea Matempla kufuata utaratibu wa imani na falsafa iliyotofautiana kabisa na ile ya Ukristo licha ya ukweli kuwa kabla ya hapo walikuwa Wakristo na isitoshe walitoka katika ulimwengu wa Kikristo. Kwa fikra za watafiti wengi jambo walilogundua Matempla ambalo lilibadili mtazamo wao ni Kabbalah. Maana ya neno hili Kabbalah ni Oral Tradition (Fasihi simulizi). Kamusi mbali mbali zinaliainisha neno hili kama ni tawi la siri na la kikuhani la dini ya uyahudi. Kwa mujibu wa ainisho hili Kabbalah inafichua maana iliyofichikana ya Taurati na maandiko ya dini ya Uyahudi. Lakini tunapolichungua jambo hili kwa undani tunaona kuwa kuna mambo mengine kabisa. Mambo haya ndiyo yanayotupelekea kufikia hitimisho kuwa Kabbalah ni utaratibu ambao mzizi wake unatokea katika ibada ya masanamu ya wapagani. Hii ni kuwa Kabbalah ilikuwepo kabla ya Taurati na ilitumbukizwa katika dini ya Uyahudi baada ya kufunuliwa Taurati. Ukweli huu wa kusisimua juu ya Kabbalah unafafanuliwa hivi: Frimasoni wa Kituruki Murat Ozgen katika kitabu chake, Masonluk Nedir ve Nasildir? (Ni nini frimansori na ikoje?), anasema:

“Hatujuwi vyema wapi ilikotokea Kabbalah na jinsi ilivyostawi. Hili ni jina la jumla la falsafa ya ajabu, ya siri na ya kikuhani hususani ile inayohusiana na dini ya Uyahudi. Inasadikika kuwa ni Itikadi ya kikuhani ya kiyahudi lakini baadhi ya mambo yaliyomo katika itikadi hiyo yanaonesha kuwa ni Itikadi iliyojengwa zamani kabla ya Taurati”.

Mwana historia wa Kifaransa anayeitwa Gougenot des Mousseaux ameeleza kuwa Kabbalah ni kongwe mno kuliko itikadi ya uyahudi. Naye Mwanahistoria wa Kiyahudi Theodore Reinach anasema kuwa Kabbalah ni sumu isiyofahamika ambayo iliingia kwenye mishipa ya Uyahudi na kuidhuru itikadi nzima. Salomon Reinach anaiainisha Kabbbalah kama

ni mojawapo kati ya pogo mbaya sana za akili ya binadamu. Sababu ya dai hili la Reinach ni kuwa itikadi ya Kabbalah kwa kiasi kikubwa inahusiana na uchawi. Kwa maelfu ya miaka, Kabbalah imekuwa msingi wa kila itikadi ya kichawi. Inasadikiwa kuwa "magwiji" wa Kiyahudi wenye elimu ya Kabbalah wana nguvu kubwa za kimazingara. Halikadhalika watu wengi wasiokuwa Mayahudi wameathiriwa na Kabbalah na wamekuwa wakijaribu kufanya uchawi kwa kutumia mafundisho yake. Zile tamaduni za siri ambazo zilikuwa na nguvu Ulaya mwishoni mwa zama za kati, kwa kiasi kikubwa mizizi yake ilitokea katika Kabbalah.

Waandishi kadhaa waliothibitisha kuwa Matempla walibadili muelekeo baada ya kugundua siri fulani kwenye mabaki ya Hekalu la Selemani. Siri hiyo ni Kabbala. Kabbala ni utaratibu unaotokea katika ibada ya masanamu ya wapagani. Kwamba, itikadi hii ilikuwepo zamani kabla ya kufunuliwa kwa Taurati. Jambo la ajabu ni kuwa Uyahudi ni dini iliyoamini Mungu mmoja iliyotokana na ufunuo wa Taurati kwa Mussa (a.s). Lakini ndani ya dini hii umo utaratibu unaoitwa Kabbalah unaofuata mafundisho ya uchawi yaliyoharamishwa na dini hiyo. Jambo hili linathibitisha yale tuliyoyaeleza awali kuwa Kabbalah ni kitu ambacho kimeingia katika Uyahudi kutoka sehemu nyingine. Lakini nini chimbuko la kitu hiki? Mwanahistoria wa Kiyahudi Fabre d'Olivet anasema kuwa kabbalah ilitoka katika nchi ya Misri ya zamani. Kwa mujibu wa mwandishi huyu mizizi ya kabbalah imetambaa kutoka Misri ya kale. Kabbalah ni utamaduni ambao baadhi ya viongozi wa Waisrael walijifunza katika nchi ya Misri. Na wao wakaurithisha utamaduni huo kwa kizazi hadi kizazi kwa njia ya fasihi simulizi. Kwa sababu hii hatuna budi kuiangalia hiyo Misri ya kale ili tuvione vyanzo vya msingi vya mfungamano wa Kabbalah, Matempla na Frimansori.

## Wachawi wa Misri ya kale

Misri ya kale ya Mafirauni ilikuwa moja ya jamii kongwe Duniyani. Ilikuwa ni moja ya jamii za kidhalimu mno. Minara mikubwa ambayo bado ipo tokea enzi hizo za Misri ya Kale-Mapiramid yalijengwa na mamia kwa maelfu ya watumwa waliofanyishwa kazi kwa mijeledi na vitisho vya kunyimwa chakula. Mafirauni ndio waliokuwa watawala wakuu wa Misri ambao walistahabu kuitwa miungu na kuabudiwa na watu. Moja ya vyanzo vya habari juu ya Misri ya kale ni maandiko yao wenyewe. Maandiko haya yaligunduliwa katika karne ya 19. Na baada ya jitihada kubwa, herufi za Kimisri zikasomeka na kutoa mwanga mkubwa wa maelezo juu ya nchi hiyo. Lakini kwa vile maandiko haya yaliandikwa na wanahistoria waliofanya kazi serikalini, yalijaa maelezo ya kuisifu dola. Kwa upande wetu chanzo cha habari cha hakika juu ya jambo hili ni Qur'an. Ndani ya Qur'an, katika kisa cha Mussa, tunapata maelezo muhimu juu ya mfumo wa utawala wa Misri ya wakati huo. Aya zinabainisha kuwa kulikuwa na mihimili miwili ya utawala; Firauni na Baraza lake la ndani. Baraza hili lilikuwa na kazi ya kutoa ushauri muhimu kwa Firauni. Mara nyingi Firauni

alikutana nalo na kufuata maoni ya baraza hilo. Aya zifuatzo zinaonyesha ushawishi wa baraza hilo kwa firauni:

**Na alisema Musa: Ewe Firauni! Mimi ni Mtume nitokaye kwa Mola wa walimwengu. Yanipasa nisiseme juu ya Mwenyezi Mungu (lolote) ila haki. Kwa yakini nimekufikieni kwa dalili wazi wazi zitokazo kwa Mola wenu. Basi wapeleke wana wa Israel pamoja nami (Nchi waitakayo, usiwazuilie hapa Misri ukawa una wadhili). (Firauni) akasema: Kama umekuja na hoja basi ilete ukiwa ni miongoni mwa wasemao kweli. (Hapo Musa) akaitupa fimbo yake (chini). Na mara ikawa nyoka dhahiri. Na akatoa mkono wake. Mara ukawa mweupe kwa watazamao. Wakasema wakuu wa kaumu ya Firauni: Hakika huyu ni mchawi ajuaye. Anataka kukutoweni katika ardhi yenu. Basi mnatoa shauri gani? Wakasema muache kidogo yeye na ndugu yake (usiwaue) na watume wakusanyao mijini. Wakuletee kila mchawi ajuaye (7:104-112).**

Ikumbukwe kuwa hapa limetajwa Baraza lililokuwa likimshauri Firauni ambapo hapa linamshawishi Firauni kupambana na Musa na linapendekeza mbinu za kukabiliana naye. Tukiangalia kumbukumbu za Historia ya Misri, tunaona kuwa Baraza hili lilikuwa na matapo mawili; tapo la jeshi na tapo la makasisi. Hakuna haja ya kufafanua umuhimu wa jeshi. Kimsingi Jeshi ndilo lililojenga nguvu za tawala za Mafirauni. Tunachopaswa kukiangalia hapa ni jukumu la Makasisi. Makasisi wa Misri ya kale ni tabaka ambalo katika Qur’an linaitwa kama tabaka la wachawi. Wao waliwakilisha tabaka la wachawi lililounga mkono utawala. Ilisadikiwa kuwa watu hawa walikuwa na nguvu fulani na walimiliki elimu ya siri. Kutokana na mamlaka waliyokuwa nayo, Makasisi walikuwa na ushawishi kwa jamii ya Wamisri na kujihakikishia nafasi yao ndani ya utawala wa Mafirauni. Tabaka hili ambalo katika kumbukumbu za Misri lilijulikana kama Makasisi wa Amon, liljishughulisha na uchawi na kulipa nafasi tabaka la wapagani. Aidha walijifunza Sayansi mbali mbali kama vile unajimu, mahesabu na jeometri. Tabaka hili la makuhani lilikuwa ni kundi la siri lililomiliki elimu mahususi. Makundi kama haya hujulikana kama mashirika ya siri.

Katika Jarida liitwalo Mason Dergisi (*Masonic Journal*) ambalo huchapishwa na kusambazwa kwa masoni wa Kituruki, kuna maelezo kuwa mizizi ya Frimansori inatokea katika kundi hili la siri na hasa linatajwa lile la makasisi wa Misri ya kale. Kadri akili ya mwanadam inavyokuwa, ndivyo Sayansi inavyopiga hatua za maendeleo na kadri sayansi inavyopiga hatua za maendeleo ndivyo idadi ya mambo ya siri inavyoongezeka katika elimu ya Utamaduni wa siri. utamaduni huu wa siri ambao kwanza ulianzia mashariki; China na Tibeti na kisha kuenea India, Mesopotania na Misri ndio uliojenga msingi wa elimu ya kikuhani ambayo imefuatwa kwa maelfu ya miaka na kuunda msingi wa nguvu ya Makasisi nchini Misri. Sasa panawezaje kuwepo mahusiano baina ya falsfa ya siri ya makuhani wa Misri ya kale na Mafrimasoni wa leo? Utawala wa Misri ya kale ambao katika Qur’an unapigiwa mfano kama utawala wa kisiasa uliomkana Mungu ulitoweka maelfu ya miaka iliyopita. Je waweza kuwa

na athari zozote hivi leo? Ili kupata jibu la maswali haya, hatuna budi kuiangalia Imani ya Makuhani wa Misri ya kale juu ya chanzo cha ulimwengu na maisha.

## Imani ya Misri ya kale juu ya dhana ya Evolusheni ya Kilahidi

Katika kitabu chao The Hiram Key waandishi wa kimasoni Christopher Khight na Robert Lomas wanadai kuwa Misri ya kale inachukuwa nafasi muhimu kuhusiana na chimbuko la Masonri. Kwa mujibu wa waandishi hawa, dhana kuu ambayo imepandikizwa kwa Masonri wa hivi sasa kutoka Misri ya Kale ni lile la ulimwengu kutokea na kujiendesha wenyewe yaani kutokea kwa bahati nasibu. Wanaifafanua dhana hii ya kuchekesha kwa maneno haya:

Wamisri waliamini kuwa Maada ndiyo iliyokuwepo wakati wote; kwao wao halikuwa jambo la kimantiki kumfikiria Mungu kuwa ndiye aliyeumba kila kitu kutokana na hamna. Dhana yao ilikuwa hii kwamba Duniya ilianza pale utulivu ulipokuja baada ya mparaganyiko wa vitu na kwamba tangu wakati huo kumekuwa na ugomvi kati ya nguvu za umoja na nguvu za utengano… Ile hali ya mvurugiko iliitwa Nun, sehemu zote zilikuwa giza totoro, nguvu ya maumbile iliyokuwa ndani yake ikaamuru maisha yaanze. Nguvu hii isiyoonekana ambayo ilikuwemo ndani ya ile hali ya msambaratiko yenyewe nayo haikujitambua kama ilikuwepo.

Kushabihiana kwa Imani ya Misri ya kale na dhana ya Evolusheni.

Katika toleo lililopita tulinukuu maelezo kutoka kwenye kitabu kinachoitwa Hiram Key kilichoandikwa na waandishi wa Kimasoni Christopher Knight na Robert Lomas ambao wanadai kuwa Misri ya kale inachukuwa nafasi muhimu katika vyanzo vya Masoni. Kwa mujibu wa waandishi hawa, dhana kuu ambayo imeibuka kwa Masonri ya leo kutoka Misri ya kale ni ile ya ulimwengu kutokea kwa bahati nasibu na kujiendesha wenyewe.

Izingatiwe kuwa dhana hii inashabihiana na madai ya Walahidi ambayo yanatiwa nguvu na ajenda ya jumuiya ya wanasayansi kwa kutumia maneno haya; “Theory of Evolution” (nadharia ya evolusheni), *“Chaos Theory”* (nadharia ya mparaganyiko) na the essential organization of matter(chanzo cha mkusanyiko wa maada). Waandishi hawa wanaongeza kusema kuwa, kuna uwiano kati ya imani za kale za Misri na Sayansi ya leo lakini Sayansi wanayoimaanisha wao ni zile dhana za kilahidi. Licha ya ukweli kwamba nadharia hizi hazina msingi wowote wa kisayansi bado zimewekwa kinguvu nguvu katika fani ya sayansi kwa takribani karne mbili zilizopita na zinawasilishwa kama nadharia zilizohalalishwa kisayansi. Sasa tumefika kwenye nukta muhimu, hebu tufanye ufupisho wa maelezo ya kile ambacho tumekisoma hadi kufikia hapa:

1. Lipo kundi la Matempla linalodhaniwa kuwa ndio chimbuko la Masonri. Tumeona kuwa japo kundi hili lilianzishwa likiwa na imani ya Kikristo lakini matempla hawa wakaathiriwa na itikadi fulani za siri walizozikuta Jerusalem. Wakaachana kabisa na Ukristo na kujiundia jumuiya iliyopingana na dini.

2. Tmeona kuwa kimsingi itikadi iliyowaathiri matempla ilikuwa kabbalah.

3. Tulipoichunguza Kabbalah, tukapata uthibitisho kuwa ingawaje itikadi hiyo imenasibishwa na Uyahudi lakini ilikuwa ni itikadi ya kipagani na ya zamani kuliko Uyahudi. Kwamba itikadi hii ilitumbukizwa tu katika dini hii na kwamba mizizi yake halisi inaonekana katika Misri ya kale.

4. Misri ya kale ilitawaliwa kwa mfumo wa kipagani wa Firauni na huko ndiko ilikokutwa dhanna inayounda msingi wa falsafa za sasa zinazomkana Mungu: Kwamba ulimwengu unajiendesha wenyewe, na umetokea kwa bahati nasibu.

Kwa hakika haya yote yanatupa picha ya wazi kabisa. Sasa swali ni je ni kwa bahati nasibu tu kwamba falsafa ya makuhani wa Misri ya kale ipo hadi leo, na kwamba vipo vielelezo vya mfungamano (Kabbalah-Matempla-Masonri) ambao ndio umehusika na uboreshaji wa dhana hii hadi kufikia leo hii?

Je yawezekana kuwa wale Masoni walioweka kumbukumbu yao katika historia ya Duniya tangia karne ya 18, wakifanya mapinduzi wakijenga falsafa na mifumo ya kisiasa ndio warithi wenyewe wa wachawi wa Misri ya kale? Ili kuliweka wazi zaidi jawabu la swali hili, hatuna budi kuchunguza kwa undani ambayo tumeeleza kwa kifupi.

## Habari ya ndani juu ya kabbalah

“Kutoka” ni jina la kitabu cha pili cha Taurati. Kitabu hiki kinaelezea jinsi wana wa Israel, chini ya uongozi wa Mussa, walivyohama Misri kuepuka udhalimu wa Firauni. Firauni aliwashurutisha wana wa Israel kuishi kama watumwa na alikataa kuwaachia huru. Lakini alipokumbana na miujiza aliyoonesha Mwenyezi Mungu kupitia kwa Musa na maangamizi aliyowapelekea watu wake, Firauni alitulia. Kwa hiyo usiku mmoja wana waisrael wakajikusanya na kuanza safari ya kuhama Misri. Baadaye Firauni akawashambulia wana wa Israel lakini Mungu akawanusuru kwa muujiza mwingine alionesha kupitia kwa Mussa. Lakini katika Qur’an ndimo tunamokuta maelezo sahihi zaidi ya kuhama kwao kutoka Misri, hii ni kwa sababu Taurati imehujumiwa baada ya kufunuliwa kwa Mussa. Ushahidi madhubuti wa hili ni kuwa katika vitabu vitano vya Taurati; Kitabu cha mwanzo, Kutoka, Walawi, Hesabu na kumbu kumbu la Taurati kuna migongano mingi. Ukweli kuwa kitabu cha kumbukumbu na Taurati kimeishia na maelezo ya kufa na kuzikwa kwa Mussa ni ushahidi usiopingika kuwa sehemu hii itakuwa imeongezwa baada ya kifo cha Mussa. Katika maelezo ya Qur’an juu ya kuhama kwa wana wa Israel kutoka Misri hakuna mgongano hata kidogo kama yalivyo

maelezo mengi mengineyo. Kisa hiki kimeelezwa kwa usahihi kabisa. Isitoshe kama zilivyo habari nyingine, Mwenyezi Mungu anatufunulia hekima na siri nyingi katika jambo linalozungumziwa. Kwa sababu hii pale tunapoziendea habari hizi kwa undani, tunweza kupata mafundisho mengi ndani yake.

**Ndama wa dhahabu.**

Miyongoni mwa mambo muhimu kuhusiyana na kuhama kwa wana wa Israel kutoka Misri, kama ilivyoelezwa katika Qur'an ni kuwa waliiasi dini iliyofunuliwa kwao na Mwenyezi Mungu licha ya ukweli kwamba Mwenyezi Mungu aliwanusuru na udhalimu wa Firauni kupitia kwa Mussa. Wana wa Israel hawakuweza kuielewa ile Tawhiid ambayo Mussa aliwafikishia badala yake wao walizidi kuielekea ibada ya sanamu. Qur'an inauelezea hivi muelekeo huu wa ajabu: (Na tukawavusha wana wa Israel baharini wakasalimika na balaa la Firauni) na ikawafikia watu waliokuwa wakiabudu masanamu yao.

**"Wakasema ewe Mussa! Tufanyie miungu na sisi yaani masanamu kama wenzetu walivyo na Miungu." (Mussa) akasema hakika nyinyi ni watu mfanyao ujinga. Hawa yataangamia haya waliyonayo na ni bure waliyokuwa wakiyafanya. (7:138-139).**

**Licha ya maonyo ya Mussa, wana wa Israel waliendelea na upotevu wao na pale Mussa alipowaacha na kwenda Mlima wa Sinai, upotevu wao ukadhihirika zaidi. Akitumia fursa ya kutokuwepo kwa Mussa, mtu mmoja aliyeitwa Samir akawajia na kuwashawishi watengeneze sanamu la ndama na kuliabudu. Mussa akarudi kwa watu wake kwa ghadhabu na masikitiko. Akasema: Enyi watu wangu! Je Mola wenu hakukuahidini ahadi nzuri? Je umekuwa mrefu kwenu muda (wa) ahadi hiyo (mnaona hazitimizwi) au mmetaka ikushukieni ghadhabu kutoka kwa Mola wenu; na kwa hivyo mmevunja ahadi yangu? Wakasema: Sisi hatukuvunja ahadi yako kwa hiyari yetu walakini tulibebeshwa mizigo ya watu (vyombo vya dhahabu tulivyoviazima kwa wanawake wa Kimisri) tukaitupa (motoni ikayayuka ikaundwa mungu). Na namna hivi hivi alitia Samir (sehemu yake). Na akawatolea (Akawaundia katika myeyusho huo) Ndama, Kiwiliwili kamili kinacholia. Na wakasema: Huyu ndiye mungu wenu na mungu wa Mussa. Lakini Mussa amesahau (20:86-88).**

Kwanini wana wa Israel walikuwa na msimamo wa ukaidi namana hiyo katika kukita masanamu na kuyaabudia? Ni nini chanzo cha muelekeo huu?

Ni dhahiri kuwa jamii ambayo hapo kabla haikuwahi kuamini masanamu, isingeweza kwa ghafla kufuata mwenendo huo wa kipumbavu wa kutengeneza sanamu na kuanza kuliabudia. Ni wale tu ambao ibada ya sanamu ilikuwa ya kawaida kwao ndio ambao wangeweza kuamini upuuzi huo. Lakini, wana wa Israili walikuwa ni watu ambao hapo kabla

waliamini Mungu mmoja tangia zama za mzee wao Ibrahim. Jina hili, “Waisraili” au “wana wa Israili” mwanzoni kabisa lilitolewa kwa watoto wa Yaqubu, mjukuu wa Ibrahim. Baadaye jina hili likatumika kwa Wayahudi wote waliotokana naye. Waisraili walikuwa wameichunga ile imani ya Mungu mmoja ambayo waliirithi kutoka kwa wazee wao; Ibrahim, Is-haqa na Yaqubu (a.s). Wakiwa pamoja na Yusufu (a.s), walikwenda Misri na wakaichunga Imani yao ya Mungu mmoja kwa kipindi kirefu licha ya ukweli kwamba waliishi pamoja na Washirikina wa Misri. Katika maelezo yaliyotolewa katika Qur’an, inabainika wazi kuwa pale Musa alipowajia, Waisraili bado walikuwa watu walioamini Mungu mmoja. Isipokuwa tu, ni kuwa pamoja na kuamini kwao Mungu mmoja, Waisraili waliathiriwa na wapagani waliokuwa wakiishi nao na wakaanza kuwaiga, wakibadili dini waliyochaguliwa na Mwenyezi Mungu na badala yake kufuata Ibada ya sanamu ya jamii nyingine.

Tunapolichunguza suala hili kwa undani na kwa kuzingatia kumbu kumbu za historia, tunaona kuwa itikadi ya kipagani iliyowaathiri Waisraili ilikuwa ni ile ya Misri ya kale. Ushahidi muhimu wa kushadidia hitimisho hili ni kuwa yule ndama wa dhahabu waliyemuabudia Waisraili wakati Musa alipokwenda mlima Sinai alikuwa mfano halisi wa Masanamu ya Wamisri, Hatha na Aphis. Katika kitabu chake, *Too Long in the Sun*, Mwandishi wa Kikristo bw. Richard Rives ameandika hivi:

Hatha na Aphis Ng’ombe jike na fahari miungu ya Misri ilikuwa ikiwakilisha ibada ya jua. Ibada yao ilikuwa ni muendelezo wa historia ya utukuzo wa jua. Yule ndama wa dhahabu wa mlima Sinai ni ushahidi tosha wa kuthibitisha kuwa karamu iliyotangazwa ilihusiana na ibada ya jua…

Athari za dini ya kipagani ya Misri zilionekana katika sura nyingi tofauti. Mara baada ya kuwashinda wapagani Imani yao ya kishirikina ikadhihirika wazi kama aya inavyosema: Ewe Musa! Tufanyie miungu na sisi (yaani masanamu) kama wao walivyo na miungu. (7:138). Na kumbukeni habari hii pia (mliposema ewe Musa hatukuamini mpaka tumuone mungu wazi wazi (2:55).

Maneno yao haya yanadhihirisha kuwa nao walitaka kuabudu Mungu wa kimaada ambaye wangemuona kwa macho kama dini ya kipagani ilivyowapatia Wamisri mungu kama huyo. Mwelekeo huu wa Waisraili kufuata upagani wa Misri ya kale ambao tumeuelezea hapa, ni muhimu ueleweke kwani ndio unaotupa ufahamu wa jinsi kilivyohujumiwa kitabu cha Taurati na unatufahamisha chanzo cha Kabbalah. Tukiyatafakari mafundisho haya kwa mazingatio, tutaona kuwa ni katika vyanzo hivi unapokutikana upagani wa Misri ya kale na falsafa ya Kilahidi.

## Kutoka Misri ya kale hadi Kabbalah

Wakati Musa angali hai, Waisraili walikwishaanza kutengeneza Masanamu kama yale yale waliyoayaona Misri na kuyaabudia. Baada ya Musa kutawafu (kufariki Duniya), hakukuwa tena na kikwazo cha kuwazuia Waisraili kuzama katika upotofu. Bila shaka haiwezi

kusemwa kuwa ni Wayahudi wote waliokengeuka, lakini baadhi yao walifuata upagani wa Misri. Kwa kweli walishikilia mafundisho ya ukuhani wa Misri (mafundisho ya wachawi wa Firauni) ambayo yalijengwa kwa msingi wa imani ya jamii hiyo na wakaihujumu imani yao kwa kutumbukiza mafundisho haya ndani yake. Itikadi ambayo ilitumbukizwa katika Uyahudi kutoka Misri ya kale ilikuwa ni Kabbalah. Kama ulivyokuwa mfumo wa Makasisi wa Misri, Kabbalah nao ulikuwa mfumo wa siri na msingi wake ulikuwa utamaduni wa uchawi. Maelezo juu maumbile ambayo Kabbalah inayatoa ni tofauti kabisa na yale yaliyokutwa katika Taurati. Ni maelezo ya kilahidi yaliyoegamia dhana ya Misri ya kale juu ya uhai wa milele wa maada. Murat Ozgen, mwana Frimasonri wa Kituruki ana haya ya kusema juu ya suala hili:

Ni dhahiri kuwa Kabbalah iliundwa miaka mingi kabla ya kuja kwa Taurati. Sehemu muhimu ya Kabbalah ni ile nadharia juu ya muundo wa ulimwengu. Nadharia hii iko tofauti kabisa na maelezo juu ya maumbile yaliyopokewa na dini zinazoamini Mungu. Kwa mujibu wa Kabbalah, mwanzoni kabisa mwa hatua ya kuumbwa kwa ulimwengu, vitu vilivyoitwa Sefiroth vikiwa na maana ya miduara au mihimili yenye sifa za kiroho na kimaada iliibuka. Idadi ya jumla ya vitu hivi ilikuwa 32.

Ile kumi ya mwanzo ndiyo iliyoshikilia mfumo wa sayari na mingine iliyosalia imeshikilia makundi ya nyota angani. Imani hii ya ajabu ya Kabbalah inabainisha kuwa inahusiana kwa karibu na mifumo ya imani ya unajimu. Kwa hiyo Kabbalah inapinmgana kabisa na dini ya Uyahudi na inanasibiana kwa karibu na imani za zamani za siri za mashariki. Kwa kufuata mafundisho ya siri na ya kilahidi ya Misri ya zamani ambayo yalijengwa kwa msingi wa uchawi, Wayahudi wakapuuza mambo yaliyoharamishwa katika Taurati. Wakashikilia ibada za kichawi za Wapagani na hivyo Kabbalah ikawa itikadi ndani ya Uyahudi lakini yenyewe ikienda kinyume na Taurati. Katika kitabu chake kiitwacho *Secret Societies and Subversive Movements*, mwandishi wa kingereza Nesta H Webster anasema:

Uchawi kama tuujuavyo ulikuwa ukifanywa na Wakanani kabla ya kuvamiwa kwa Palestina na Waisraili. Misri, India na Ugiriki nazo zilikuwa na wachawi na waaguzi wao. Licha ya makemeo dhidi ya uchawi yaliyomo katika sheria ya Musa, Wayahudi walijiingiza katika uchawi na ule utamaduni mzuri waliourithi wakauchanganya na mawazo ya kichawi yaliyotoka katika jamii nyingine.

## Tamaduni za kipagani za uchawi wa zama za kale

Katika toleo lililopita tuliona kuwa Wayahudi walipuuza mambo yaliyohamishwa katika Taurati na hivyo kufuatia ibada za kipagani. Kwa ajili hii, Kaballa ikawa itikadi ndani ya dini ya uyahudi ingawaje ingawaje ilipingana na Taurati. Katika kitabu chake kiitwacho *Secret Societies, and Subversive Movements,* Mwandishi wa kiingereza Nesta Webster ameandika hivi:

Uchawi, kama tuujuavyo ulikuwa ukifanywa na Wakanani kabla Palestina haijavamiwa na Waisrail. Nazo nchi za Misri, India na Ugiriki vile vile zilikuwa ni za Wachawi na Waaguzi wao. Licha ya makatazo yaliyomo katika sheria ya Musa, Wayahudi wakauchanganya utamaduni wao mtukufu na mambo ya uchawi yaliyotoka katika jamii nyingine na mengine waliyoyatunga wenyewe. Hapa ndipo ilipo hoja ya Wapinzani wa Kabballa kuwa hii tunayoijua sisi hivi leo kama Kabbala, kimsingi haikutoka katika Uyahudi. Katika Qur'an, kuna aya inayozungumzia jambo hili. Mwenyezi Mungu anasema kuwa; wana wa Israili walijifunza tamaduni za kichawi za kishetani kutoka nje ya dini yao.

**Wakafuata yale waliyofuata mashetani(wakadai kuwa yalikuwa katika Ufalme wa Suleiman na Suleiman hakukufuru, wakafundisha watu uchawi(waliokuwa wakiujua wenyewe tangu zamani), na(uchawi) ulioteremshwa kwa Malaika wawili, Haruta na Maruta katika(mji wa) Babil. Wala(Malaika hao) hawakumfundisha yeyote ila mpaka wamambie, hakika sisi ni mtihani(wa kutazamwa kutii kwenu) basi usikufuru. Wakajifunza kwao mambo ambayo kwayo waliweza kumfarakanisha mtu na mkewe(na mengineyo) wala hawakuwa webye kumdhuru mtu yeyote kwa hayo ila kwa idhini ya Mwenyezi Mungu. Na wanajifunza ambayo yatawadhuru wala hayatawafaa. Na kwa yakini wanajua kwamba aliyekhiari haya hatakuwa na sehemu yoyote katika Akhera. Na bila shaka ni kibaya kabisa walichouzia nafsi zao laiti wanagelijua(2:102).**

Ayah ii inabainisha kuwa japo, Wayahudi Fulani walijua kuwa watapata hasara katika maisha ya Akhera lakini bado walijifunza na kufuata tamaduni za kichawi.

Hivyo walikengeuka na toka katika sheria ambayo Mungu aliwashushia. Wakawa wamezitia hasarani nafsi zao kwa kutumbukia katika upagani(Itikadi za wachawi). Mambo yaliyoelezwa katika aya hii yanaweka bayana vinpengele vikuu vya mfarakano katika historia ya Wayahudi. Mapambano yalikuwa baina ya Mitume na wafuasi wai kwa upande mmoja na kwa upande wmingine Wayahudi waliopotoka na kuasi amri za Mungu na kuiga tamaduni za kipagani. Ni muhimu kukumbuka kuwa maovu ya Wayahudi wapotevu yamendikwa katika agano la kale. Ndani ya agano la kale kuna kitabu cha Nehemia ambamo Wayahudi wanaungama na kutubu. Waliokuwa wazawa wa Israili wakajitenga na wageni wote, wakasimama mahali pao, wakasoma katika kitabu cha Torati ya Bwana, Mungu wao, muda war obo ya siku, na siku nyingine, wakaungama, wamuabudu Bwana Mungu wao. Ndipo wakasimama madarajanai ya walawi, Yeshua na Bani, na Kadimieri na Shebania na Kenani, wakamlilia Bwana Mungu wao kwa sauti kuu.

(Wakasema) walakini (Baba zetu) hawakutii, wakaasi, wakaitupa sheria yako nyuma yao, wakawaua manabii wako walioshuhudia juu yao wapate kuwarejeza kwako; wakatenda machukizo makuu. Kwa sababu hiyo ukawatia katika mikono ya adui zao, waliowasumbua na wakati wa shida yao walipokulilia, uliwasikia kutoka mbinguni; na kwa wingi wa rehema zako ukawapa waokozi waliowaokoa katika mikono ya adui zao. Lakini walipokuwa

wamekwishastarehe, walitenda mabaya tena mbele zako; kwa hiyo ukawaacha katika mikono ya adui zao, nao wakawatawala; hata hivyo waliporejea na kukulilia, uliwasikia toka mbinguni, ukawaokoa mara nyingi kwa rehema zako, ukawashuhudia ili uwarudishe tena katika sheria yako; lakini walitakabari wasisikilize amri zako,(ambazo mtu akizitenda ataisi katika hizo0 nao wakayaondoa, wakafanya shingo zao kuwa ngumu, wasitake kusikiliza. Ila kwa rehema zako nyingi hukuwakomesha kabisa wala kuwaacha; kwa maana wewe u Mungu Mwenye neema, Mwenye rehema. Basi sasa Ee Mungu, Mkuu Mwenye Uweza, Mungu wa kuogofya mwenye kushika maagano yote yaliyotupa sisi, wafalme wetu wakuu wetu wa makuhani wetu wa manabii wetu, na baba zetu na watu wako wote, tangu zamani za Wafalme wa Ashuru hata leo, na yasihesabiwe kuwa ni madogo. Lakini wewe u mwenye haki, katika hayo yote yaliyotupata; maana wewe umetenda yaliyotenda yaliyokeli lakini sisi tumetenda yaliyo mabaya na Wafalme wetu na wakuu wetu na wakuu wetu na makuhani wetu na Baba zetu hawakushika sheria yako wala hawakusikiliza amri zako na shuhuda zako ulizowashuhudia. Kwa kuwa hawakukutumikia wewe katika Ufalme wao na katika wema wako mkuu uliowapa na katika nchi ile kubwa yenye neema uliyowapa mbele yao wala hawakughairi na kuacha mabaya yao.(Nehemia 9:2-4, 26-29, 31-35).

Kifungua hiki kinalezea tamaa ya kurejea katika imani ya Mungu mmoja ambayo Wayahudi wengi walikuwa nayo, isipokuwa katika kipindi Fulani cha historia kundi moja lilimeguka na kupta ushawishi kidogo kidogo, na baadae likaja kuwa tawala Wayahudi na baadae likaigeuza kabisa dini yenyewe. Kwa sababu hii, katika Taurati na katika vitabu vingine vya Agano la Kale kuna masalia yanayotoka katika mafundisho ya kipagani. Katika kitabu cha mwanzo inaelezwa kuwa Mungu aliumba Ulimwengu kwa siku sita wakati ambapo hapakuwa na chochote. Hii ni im'ani sahihi kabisa na inatokana na ufunuo sahihi. Lakini hapo hapo inasema kuwa Mungu alipumzika siku ya saba huu ni uzushi kabisa. Ni dhanna potofu iliyotoka katika upagani amabo unampa Mungu sifa za kibinaadamu:

Katika aya hii ya Qur'an Mwenyezi Mungu anasema:

**Na tumeziumba mbingu na ardhi na vilivyomo katika yao katika nyakati sita wala hayakutugusa machovu(50:38).**

Katika sura nyingine za Taurati kuna staili ya uandishi ambayo ni ya utovu wa heshima kwa Mwenyezi Mungu hasa zaidi katika zile sehemu ambazo sifa za kibinaadamu anapewa Mungu. Imani hizi potofu za kulinganisha udhaifu wa kibinaadamu ndizo imani ambazo wapagani walikuwa nazo kwa miungu yao bandia. Maneno mengine ya kufuru ni yale yanayodai kuwa Yakobo, Baba wa Waisrail alipigana mieleka na Mungu akashinda. Ni wazi kabisa hiki ni kisa cha kutungwa ili kuwatukuza Waisrail ni mwigo kutoka katika jamii za Wapagani. Katika agano la kale kuna mtindo wa kumuelezea Mungu kama Mungu wa Utaifa yaani Mungu wa Waisraili peke yao. Lakini Mungu kwa Ulimwengu na viumbe sote. Dhana hii

ya dini ya Utaifa katika agano la kale inafanana na dhana za kipagani ambapo kila kabila linaabudia Mungu wake. Katika baadhi ya vitabu vya Agano la kale(mfano, Yeshua) amri zinazotolewa kufanya maovu dhidi ya watu wasiokuwa Wayahudi. Mauaji ya halaiki yanamrishwa bila kujali wanawake, watoto wala wazee. Mwenendo huu wa kinyama unakwenda kinyume kabisa na sheria ya haki ya Mungu, badala yake unarandana na ushenzi wa tamaduni za kipagani za kuabudu Mungu bandia wa vita.

## Mafundisho ya kipagani yalivyoongezwa katika Taurati

Katika toleo lilipita tulimalizia kwa maelezo haya; kwamba katika baadhi ya vitabu vya Agano la kale(mfano Yeshua) zinatolewa amri za kufanya maovu dhidi ya watu wasiokuwa Wayahudi. Mauaji ya halaiki yannamrishwa bila kujali Wanawake, watoto wala wazee. Mwenendo huu wa kinyama unapingana kabisa na sheria ya haki ya Mungu, badala yake unarandana na ushenzi wa tamaduni za kipagani za kuabudia Miungu bandia wa vita. Mawazo haya ya kipagani ambayo yametumbukizwa katika Taurati yumkini yana chanzo chake. Lazima tu kulikuwa Matyahudi ambao walifuata mila isiyokuwemo katika Taurati.

Wakaishika na kuitukuza mila hiyo. Kisha, baadaye, Wakatumbukiza katika Taurati mawazo yaliyotokana na mila hii ambayo wao walikubaliana nayo. Chimbuko la Mila hii linaanzia nyuma kabisa kwa makuhani wa Misri(Wachawi katika utawala wa Firauni). Kwa kweli ilikuwa ni Kabbala iliyorithiwa na Wayahudi wengi. Kabbala ilikuwa na sura ambayo iliziwezesha itikadi nyigine za kipagani kujipenyeza katika dini ya Uyahudi na kustawi ndani yake. Wadau wa Kabbalah, bila shaka wanadai kuwa Kabbalah inafafanua tu kwa kina siri zilizofichikana katika Taurati, lakini kwa kweli, kama asemavyo mwanahistoria wa Kiyahudi kuwa Kabbalah si sumu isiyotambulia ambayo imeingia katika dini ya Uyahudi na kuiathiri kabisa. Hapo sasa inawezekana kukuta ndani ya Kabbalah yale masalia ya itikadi ya ulahidi ya Wamisri wa zama za kale.

Kabala-Itikadi inayopingana na itikadi ya kuumbwa kwa ulimwengu.

Katika Qur’an, Mwenyezi Mungu anabainisha kuwa Taurati ni kitabu cha Mungu ambacho kilishushwa kama muongozo kwa Wanadamu.

**Hakika tuliteremsha Taurati yenye uongozi na nuru ambayo kwayo Manabii waliojisalimisha waliwahukumu Mayahudi na Watawa na Maulamaa pia, kwa sababu walitakiwa kuhifadhi kitabu hicho cha Mwenyezi mungu, nao walikuwa mashahidi juu yake(5:44).**

Kwa hiyo basi, Taurati, kama ilivyo Qur’an, ni kitabu chenye ilimu na maamrisho yanahusiana na Tauhidi inayobainisha kuwepo kwa Mwenyezi Mungu na upweke wake, sifa

zake, kuumbwa kwa Wanaadamu na viumbe vingine lengo la kuumbwa kwa binaadamu na kanuni za maadili za Mwenyezi mungu kwa Wanadamu. Hata hivyo, ile Taurati ya asili haipo tena hivi leo. Tuliyonayo hivi leo ni Taurati iliyoandikwa upya na kuhujumiwa na mikono ya binaadamu. Nukta muhimu ni kuwa ile Taurati ya asili na Qur'an zinashabihiana. Mote humo, Mwenyezi Mungu anatambuliwa kama Muumba. Anatambuliwa kama aliyetakasika na aliyeepukana na upungufu wowote ule na amekuwepo bila mwanzo. Chochote kile miinghairi yake ni kiumbe chake. Yeye ndiye aliyeumba ulimwengu wote, maumbile ya angani, maada isiyo na uhai, binaadamu na vyote hai. Mwenyezi mmoja tu.

Wakati ambapo huu ndio ukweli wa mambo, kuna malelezo tofauti kabisa yanyokutikana katika Kabbala, ambayo ni sumu iliyopenya katika mishipa ya uyahudi na kuathiri kabisa mafundisho yake juu ya Mungu; maelezo hayo yanapinga na kabisa na ule ukweli unaokutikana katika ile Taurati ya asili na katika Qur'an. Katika moja ya maandiko yake juu ya Kabbala, mtafiti mmoja wa Amerika, Lance S. Owens anatoa maoni yake juu ya vyanzo hasa vya itikadi hii. Itikadi ya Kabbalah imezaa dhana kadha wa kadha kuhusu Mungu. Nyingi kati ya hizo zimetoka nje kabisa ya mtazamo wa dini. Msingi mkuu wa imani ya WanaIsraili ulikuwa ni Kalima kwamba Mungu wetu ni mmoja. Lakini Kabbala ikdai kuwa wakati Mungu akiishi katika umbile la peke yake ambalo, katika Kabbalah linaitwa Ein Sof- asiye na udhaifu-upweke huu usiojulikana laima utakuwa umeanzia katika maumbile mengi ya kiungu.

Yaani kundi la Miungu. Miungu hii ambayo mwanakabbala aliita sefiroth yaani sura au nyuso za miungu. Jinsi ambavyo mungu alitokea katika umoja usioeleweka na kuingia katika wingi ilikuwa ni siri ambayo Wanakabbalah walihangaika kuitafuta.

Ni dhahiri kuwa hii sura ya Miungu inakubaliana na madai ya Washirikina siyo tu Mungu alikuwa katika wingi katika itikadi ya Kabbala bali hata upweke usiojulikana kulichukuwa sura mbili; ya kiume na ya kike, Baba na Mama, Hokhmah na Binah. Hizi ndizo sura za mwanzo za Mungu. Wafuasi wa Kabbala walikuwa wakitumia tamathali za kijinsia kuelezea jinsi maingiliano ya kimaumbile kati ya Hokhma na Binah yalivyozaa maumbile mengine. Jambo jingine la kuchekesha katika theolojia hii ya kishirikina ni kuwa, binaadamu hawakumbwa bali kwa kiasi Fulani na wao Wanaasili ya Kiungu. Bwana Owens, mtafiti wa Kiamerika anaielezea hivi dhana hii.

Picha ya ajabu ya Mungu iliyobuniwa na Kabbalah ina sura ya Upweke na wingi. Kwa mujibu wa dhanna hii ya Kabbalh, Mungu alikuwa Adamu Kadnoni. Mtu alikuwa sawa na Mungu nkatika ile sifa ya asili ya kutoumbwa na katika lile umbile lisilofahamika. Dhana hii ya ajabu inayomuelezea Adamu kana Mungu ilishadidiwa na mafundisho ya Kabbala; thamani ya tarakimu ya majina Adamu na Yehova na Adamu walikuwa sawa, hivyo Adamu alikuwa Mungu. Kwa dai hili binaadamu wote wanapofikia daraja la juu kabisa huwa sawa na Mungu. Theolojia hii inayojumuisha dhanna ya upagani ndiyo iliyojenga msingi uliopotosha chini ya

Uyahudi. Wanakabbalah wa kiyahudi wakakiuka mipaka ya kawaida ya binadaamu kiasi kwamba wakafika mahala pa kuthubutu kufanya binaadamu miunga. Mbali na ishara hivyo, kwa mujibu wa theolojia hii, sio tu binaadamu walikuwa miungu bali miungu wenyewe ni wayahudi peke yao; watu wa jamii nyingine walihesbiwa kama binaadamu tu wa kawaida. Matokeo yake ndani ya ndani ya dini ya Uyahudi ambayo, kimsingi, ilianzishwa kwa ajili ya kumtii na kumtumikia Mungu, itikadi hii potofu ilianza kumea lengo likiwa kutimiza ujinga wa Wayahudi.

Licha ya kupinga kwake na Tautrati, Kabbal ikaingizwa katika Uyahudi na hatimaye ikaanza kuihujumu Taurati. Jambo jingine la kuzingatia kuhusiana na mafundisho potofu ya Kabbala ni ule uwiano wa fikra baina yake na upagani wa Misri ya zamani.

Kama tulivyosema awali, wamisri wa zamani waliamini kuwa maada na uhai; kwa maneno mengine walikanusha kuwa maada iliumbwa pasipo chochote. Kabbalah nayo inadai vivyo hiovyo kuhusiana na binaadamu. Inadai kuwa binaadamu hawa kuumbwa na kwamba Wanajiendeashea wenyewe maisha yao.

Kulizungumzia hili kwa maneno ya sasa ni kuwa Wamisri wa kale walikuwa walahidi na kimsingi itikadi ya Kabbala yaweza kuitwa secular Humanism. Ni muhimu kukumbuka dhanna hizi mbili; ulahidi na Secular Humanism ndizo zilizozaa itikadi ambayo imetawala Duniyani kwa zaidi ya karne mbili zilizopita.

Yafaa kuuliza iwapo kuna watu ambao wameziendeleza itikadi za Misri ya kale na Kabbalh tokea katikati ya kipindi cha nyuma cha historia hadi leo hii.

## Wale waliokuwa Matempla ndio hao wakawa Mafrimansori

Wakati tulipowazungumzia Matempla huko nyuma, tulisema kuwa kundi hili mahususi la Makruseda liliathiriwa na "siri" waliyoikuta Jerusalem.

Katika kitabu Foucaut's Pendulum Mwanafasihi mashuhiri wa Italia umberto Eco, naye anauelezea ukweli huu. Katika riwaya yake yote anasimulia kupitia vinywa vya wahusika wakuu wa riwaya yake kuwa Matempal waliathiriwa na Kabbala na kwamba wale Makabbala walikuwa na siri ambayo chanzo chake chaweza kuwa ni Mafirauni wa Misri ya kale.

Kwa mujibu wa Eco, baadhi ya Wayahudi mashuhuri walijifunza siri Fulani kutoka kwa wamisri wa zamani na baadae wakazi tumbukiza katika vitabu vitano vya kwanza Agano la kale.

Lakini siri hii ambayo ilisambazwa chinichini, ilikuwa ikijulikana kwa Wanakabbala peke yao. Baada ya kuelezea kuwa Wanakabbala waliisoma siri hii ya Misri ya kale katika Hekalu la selemani, Eco pia anaandika kuwa Matempla nao wakaisoma siri hii kutoka kwa walimu wa Kabbala mjini Jerusalem.

Siri hii ilikuwa ikijulikana kwa kikundi kidogo sana cha Waalimu wa Kiyahudi waliobakia Palestina. Matempla wakaisoma kutoka kwa Waalimunhao. Pale Matempla walipofuata itikadi mseto ya Misri ya Kabbal ndipo walipofarakana na dhehebu la Kikristo lililokuwa likiwatawala Ulaya.

Ulikuwa ni mfarakano ambapo wao walishirikiana na nguvu nyingine kubwa ya Wayahudi. Baada ya Matempla kutiwa mbaroni kwa amri ya pamoja ya Mfalme wa Ufaransa na Papa mnamo mwaka 1307, kundi hili likatokomea chini chini lakini athari zake zikabakia. Tena zikawa mbaya zaidi na zilizokuwa na uelekeo madhubuti.

Kama tulivyosema awali, idadi ndogo ya Matempla walinusurika katika kamata kamata na kukimbilia kwa Mfalme wa Scotland, utawala pekee wa Kifalme barani Ulaya ambao hakuyatambua mamlaka ya Papa.

Kule Scotland, Matempla wakajipenyeza katika jumuiya ya Well Builders na wakaitawaa. Jumuiya zikafuata ule utamaduni wa Matempla na hapo ndipo ilipopandwa mbegu ya Masoni.Kama ilivyofafanuliwa kwa kina katika kitabu kiitwacho The New Masonic order, kuanzia karne ya kumi na nane ndipo yanapoonekana masalia ya Matempla na Mayahudi kadhaa walioshirikiana nao katika vipindi mbali mbali vya historia ya Ulaya.

Bila kutoa maelezo mengi, zifuatazo ni nukta muhimu za utafiti. Katika mji wa Province nchini Ufaransa kulikuwa na kambi ya Matempla waliokimbilia nchini humo na kujificha wakati wa ile kamatakamta.

Kielezeo kingine ni kuwa huko ndiko kulikokuwa na kituo mashuhuri cha Ukabbal. Province ndipo mahali ambapo fasihi simulizi ya kabbala iliandikwa katika kitabu. Kwa mujibu wa wanahistoria, uasi wa wakulima nchini Uingereza mwka 1381 ulichochewa na jumuiya Fulani ya siri.

Watafiti wa historia ya Frmasonri wamekubaliana kuwa jumiya hii ya siri ilikuwa ya Matempla. Ule uasi haukuwa tu wa kizalendo bali pia ulilenga kulishambulia kanisa katoliki.

Nusu karne baada ya uasi huu, Kasisi mmoja wa Bohenia John Hus akaanzisha vurugu kulipinga Kanisa Katoliki. Kama kawaida, nyuma ya uasi huu walikuwepo Matempla.

Isitoshe Huss mwenyewe alikuwa akiipenda sana Kabbal. Yeye alikuwa akimpenda sana Avigdor Ben Isaac Kara. Mtu huyu alikuwa Mwalimu mashuhuri wa kiyahudi mjini Prague na pia alikuwa Mwanakabbala.

Vielezeo hivi vinaonesha kuwa ushirikiano baina ya Matempla na Wanakabbala ilileng kubadilisha mfumo wa jamii ya Ulaya. Mabadiliko haya yalijumuisha misingi ya utamaduni wa Kikristo ambao ndio utamaduni mama wa ulaya na badala ya utamaduni huu uwekwe utamaduni uliojengwa kwa misingi ya kipagani kama vile kabbal. Kisha yafuate mabadiliko ya kisiasa. Mfano ni mapinduzi ya Ufaransa na Italia.

Huko mbele tutaona vipindi vya mabadiliko ya Historia ya Ulaya. Katika kila kipindi tutakutana na ukweli kuwa kulikuwa na nguvu iliyotaka kuitenganisha Ulaya mbali kabisa na mafundisho ya Kanisa na badala yake iweke itikadi ya kisekula na hivyo izisambaratishe taasisi zote za dini.

Nguvu hii ilijaribu kuichaguzi Ulaya kuikubali itkadi iliyorithiwa kutoka Misri ya kale kupitia Kabbala. Tulikwishabainisha huko nyuma kuwa misingi ya Usekula ni dhana za Humanism na Matearialism au utu mtu na ulahidi.

## Itikadi ya utu - ‘Humanism’

Yasadikiwa na wengi kuwa Humanism ndiyo itikadi madhubuti ambayo inampandikiza mtu hisia za upendo, utulivu, na udugu. Lakini kifalsafa dhana hii ina maana kubwa zaidi. Humanism ni utaratibu wa fikra ambao unaichukulia dhana ya utu kuwa ndio msingi wa lengo lake kuu.

Kwa maneno mengine unawataka watu wajitenge mbali na Mungu Muumba, kisha washughulike tu na maisha yao na utu wao. Kamusi ya kiingereza iitwayo *Common Dictionary* inaliainisha neon Humanism kama ni mfumo wa itikadi uliojengwa juu ya msingi wa maadili, sifa, na tabia, ambazo zinaaminika kuwa bora zaidi kwa vigezo vya binaadamu wenyewe bila kutegemea mwongozo wowote wa kiungu.

Ainisho la wazi zaidi la humanism limetolewa na wale wanaunga mkono dhana hii. Mmoja kati ya wapiga debe wakuu wa itikadi ya humanism ni bwana Carloss Lamont. Katika kitabu chake, the philosophy of humanism, mwandishi huyu ameandika; “ kwa ujumla Humanism inaamini kuwa maumbile yanatokana na mkusanyiko wa vitu halisi ambavyo msingi wake na nguvu ya maada”.

Kitabu hiki kinazidi kueleza kuwa maada ndio msingi wa Ulimwengu, na kwamba nguvu za kiungu hazipo.

Dhana ya nguvu za Kiungu kwa upeo wa Binaadam haina ushahidi. Kwamba watu hawana roho za kudumu milele yaani zisizokufa, na ulimwengu kwa ujumla hauna Mungu aliyeuumba wala Mungu wa milele.

Kama tunavyojionea wenyewe katika nukuu hizo, Itikadi ya humanism inafanana kabisa na itikadi ya Atheism, na ukweli huu unakubaliwa bila ubishi na Wahumanisti wenyewe.

Zilikuwepo ilani mbili muhimu zilizochapishwa na Wahumanisti katika karne iliyopita. Ilani ya kwanza ilichapishwa mwaka 1933 na ikapitishwa na watu wao muhimu wa wakati huo.

Miaka arobaini baadaye (yaani mwaka 1973), ilani ya pili ya Wahumanisti ikachapishwa. Ilani hii ilithibitisha ile ya awali, lakini ilitiwa nyongeza kufuatia hatua Fulani za maendeleo ambazo zilipigwa wakati huo. Maelfu ya wanafikra, waandishi wa vitabu, na wanahabari, walisaini ilani hii ya pili, ambayo inaungwa mkono na chama cha harakati za wahumanisti wa Amerika. Tukiziangalia ilani hizi tunagundua kuwa, katika kila ilani kuna msingi mmoja mkuu ambao ni dhana ya Atheism.

Dhana hiyo inasema kwamba Ulimwengu haukuumbwa, na Wanaadamu pia hawakuumbwa.. Kwa msingi huo wanaadam wanaishi kwa kujiendesha wenyewe na kwamba hawawajibiki kwa mamlaka yeyote isipokuwa kwa wao wenyewe.. Na kwamba imani juu ya Mungu inadumaza maendeleo ya watu na jamii. Kwa mfano vipengele sita vya kwanza vya ilani ya Wahumanisti ni hivi vifuatavyo;

Mosi, Wahumanisti wanaitakidi kuwa Ulimwengu unajiendesha wenyewe na haukuumbwa.

Pili, dhana ya humanism inaitakidi kwamba mtu ni sehemu ya maumbile, na kwamba ameibuka kutokana na mfumo unaojiendesha wenyewe.

Tatu, wakishikilia mtazamo wa maisha ya kiagoniki, wahumanisti wanaona kuwadhana ya pande mbili za nafsi na mwili lazima ipingwe kabisa.

Nne, itikadi ya humanism inatambua kuwa utamaduni wa kidini wa mtu na ustaarabu wake kama ulivyoelezwa na historia ni zao la hatua za polepole za maendeleo zitokanazo na mahusiano baina yake na mazingira na mazingira yake. Mtu anayezaliwa katika utamduni Fulani, kwa kiasi kikubwa, anajengeka kwa utamaduni huo. Tano, dhana ya humanism inatangaza kuwa maumbile ya ulimwengu yaliyoelezwa na sayansi ya leo yanatupilia mbali nguvu yeyote ya mbinguni kuhusiana na maadili ya binadamu. Sita, tunaamini kuwa dhana ya theism, deism, modernism na aina kadhaa za itikadi mpya zimepitwa na wakati.

Katika vipengele hivyo, tunaiona waziwazi nafasi ya falsafa ya common ambayo inajidhihirisha yenyewe kwa majina ya Materialism, Darwinism atheism na agnosticism. Katika kipengele cha kwanza dhana ya ulahidi ya uhai wa milele wa ulimwengu umeelezwa wazi. Kipengele cha pili kinasema kuwa binadamu hawakuumbwa. Hivi ndivyo isemavyo nadharia ya evolusheni. Kipengele cha tatu kinakanusha mamlaka ya Mwenyezi Mungu juu ya ulimwengu na walimwengu na kipengele cha sita kinaikataa imani juu ya Mungu. Ikumbukwe kuwa madai haya ndiyo yale yale ya zile duru zenye chuki na dini sahihi. Sababu ni kuwa dhana ya humanism ndio msingi mkuu wa hisia zote zinazopinga dini.

Hii ni kwasababu dhana hii inasema kuwa mtu ataachwa hivyo hivyo bila kuhesabiwa. Katika historia yote huu ndio umekuwa msingi wa madai ya kumkanusha Mungu. Katika aya hii ya Qur'an Mwenyezi Mungu anasema; Je anafikiri binadamu kuwa ataachwa bure? Je hakuwa tone la manii lililotonwa? Kisha akawa kidonge cha damu, kisha akamfanya namna mbili, mwanaume na mwanamke. Je! Hakuwa huyo ni muweza wa kuhuisha wafu?

Hapa Mwenyezi Mungu anasema kuwa watu hawakuachwa tu hivi hivi na anawakumbusha kuwa wao ni viumbe wake. Hii ni kuwa pale mtu anapotanabahi kuwa yeye ni kiumbe wa Mungu, basi aelewe kuwa haishi bila ya kuangaliwa

Miaka sita baada ya kuchapishwa ilani ya humanism, vita vya pili vya Duniya vikaripuka

Katika aya hii ya Qur'an Mwenyezi Mungu anasema, Je! Binadamu anafikiri kuwa ataachwa bure tu (asipewe amri za Mwenyezi Mungu wala makatazo yake)? Je! Hakuwa tone la manii lililotonwa? Kisha akawa kidonge cha damu, kisha akamuumba na akamsawazisha (kuwa mtu kamili)? Kisha akamfanya namna mbili. Mwanaume na mwanamke. Je! Hakuwa hayo ni muweza wa kuhuisha wafu?

Hapa Mwenyezi Mungu anawakumbusha binadamu kuwa wao ni viumbe vyake. Pale mtu anapotanabahi kuwa yeye ni kiumbe wa Mungu basi aelewe kuwa haishi bila ya kuangaliwa bali anawajibika kwa Mwenyezi Mungu.

Dai kuwa binadamu hawakuumbwa ndio msingi wa falsafa ya humanism. Vipengele viwili vya ilani ya kwanza ya Wahumanisti vinatoa ufafanuzi wa itikadi hii.

Zaidi ya hivyo Wahumanisti wanashikilia kuwa sayansi inaunga mkono madai haya. Lakini ni waongo wakubwa.

Tokea ilani yao ya kwanza ilipochapishwa, hoja mbili ambazo wanahumanisti wamezitoa kama hakika za kisayansi, kwamba ulimwengu ni wa milele na wa kievolusheni, zote zimevunjiliwa mbali.

Dhana kwamba ulimwengu ni wa milele ulivunjiliwa mbali na mlolongo wa vumbuzi za angani zilizofanywa wakati ilani ya kwanza ya wanahumanisti ilipokuwa inaandikwa.

Vumbuzi kama vile ulimwengu kutanuka, chanzo cha mionzi ya angani na mahesabu ya uwiano ya Haidrojeni hadi Helium, zimethibitisha kuwa ulimwengu ulikuwa na chanzo chake na kwamba ulitokea kwa mlipuko mkubwa- Big Bang takriban miaka bilioni 15 au 17 iliyopita.

Ingawa wale wanashabikia falsafa ya kihumanisti na ya kilahidi walikataa kuikubali nadharia ya Big Bang lakini hatimaye walishindwa vibaya sana kutokana na ushahidi wa kisayansi ambao umejitokeza.

Jamii ya wanasayansi hatimaye ikaikubali nadharia ya Big Bang kwamba ulimwengu ulikuwa na chanzo chake. Hivyo, Muatheisti Anthony Flew alilazimika kukiri hivi;

….Sasa nitaanza kukiri kuwa Muatheisti lazima atatizike kwa hizi fikra za sasa za maumbile. Kwani inaonekana kuwa wanakosmolojia wanatoa ushahidi kuwa kile alichodai mtakatifu Thomas hakiwezi kuthibitishwa kifalsafa, hii ikiwa na maana kuwa ulimwengu ulikuwa na mwanzo wake.

Nadharia ya evolusheni ambayo ndio hoja kuu iliyomo katika ilani ya kwanza ya humanisti, ikaanza kupoteza nguvu miongo kadhaa baada ya kuandikwa kwake.

Inafahamika hivi leo kuwa ubabaishaji uliofanywa na wanaevolusheni na Waatheisti (na bila shaka Wahumanisti) kama vile A.I. Oparin na J.B.S Haldane katika miaka ya thelasini kuhusiana na chanzo cha uhai hauna msingi wa kisayansi.

Viumbe haviwezi kutokea kwa bahati nasibu kutokana na maada isiyo na uhai kama ilivyodaiwa katika ubabaishaji huo. Kumbu kumbu ya mabaki ya kale inaonesha kuwa viumbe hai hawakuwa hivi walivyo kutokana na hatua za mabadiliko madogo madogo bali walitokea kuwa pamoja wakiwa na sifa zao mbalimbali.

Ukweli huu umekubaliwa na wanaevolusheni wenyewe tangia miaka ya sabini. Sayansi ya viumbe hivi leo imebainisha kuwa viumbe hai hawakutokana na bahati nasibu na kanuni za maumbile bali katika kila kiumbe kuna mfumo madhubuti unaothibitisha kuwa msaniii mwenye hekima ndiye aliyeviumba. Kwa maelezo zaidi rejea kitabu kiitwacho Darwinism refuted. Zaidi ya hivyo, lile dai la uongo kuwa imani ya dini ndiyo sababu inayokwaza watu kuendelea na kuwatumbukiza matatizoni limetupiliwa mbali na ushahidi wa kihistoria. Wahumanisti wamedai kuwa kuondolewa kwa imani ya dini kutawaletea watu faraja na furaha, lakini hali ya mambo imekuwa kinyume chake.

. Vita hii ni kielelezo cha kihistoria cha misiba mikubwa iliyoletwa na itikadi za kifashisti za kisekula. Ikachipuka itikadi ya kikomunisti ya wahumanisti kwanza ilianzia kwa watu wa Urusi, kisha kwa watu wa China, Cambodia, Vietnam, Korea kaskazini, Cuba na katika baadhi ya nchi za Afrika na Latin Amerika. Ulifanyika ushenzi usio na mfano. Jumla ya watu milioni 120 waliuliwa na tawala au Jumuiya za kikomunisti. Ni dhahiri kuwa kundi la Wahumanisti wa magharibi (mabepari) nalo limeshindwa kuleta amani na furaha katika jamii zao na katika maeneo mengine ya Duniya. Kuvunjwa kwa hoja ya Wahumanisti juu ya dini pia kunadhihirika katika fani ya saikolojia. Misingi ya dhana ya Kiatheisti ilibatilishwa na matokeo ya tafiti tokea mwanzoni mwa karne ya ishirini (The Freudian myth). Patric Glynn wa chuo kikuu cha George Washington anaufafanua ukweli huu katika kitabu chake kiitwacho God, The Evidence, The Reconciliation of Faith and reason in a Post Secular World.

## Lengo la  Masoni ni kujenga Duniya ya kufuru

Falsafa ya kihumanisti ambayo masoni wanaamini kuwa ndiyo falsafa kuu imejengwa kwa msingi wa kumkanusha Mungu. Lakini hii inazusha swali muhimu je masoni wanaitaka falsafa hii kwa ajili yao tu  au wanataka ifuatwe na wengine pia tunapoyaangalia maandiko ya masoni tunaliona bayana jawabu la swali hili. Lengo la jumuiya hii ni kuieneza falsafa hii Duniyani kote ili kuzifutilia mbali dini zinazoamini Mungu muumba. Mathalani katika makala yake iliyochapishwa katika jarida la masoni Mimar Sinan imeelezwa hivi, “masoni hawatafuti chanzo cha fikra za maovu, haki na uadilifu nje ya ulimwengu wa kimaumbile, wao wanaamini kuwa fikra hizi zinaibuka kutoka na mazingira ya jamii ya mtu, mahusiano ya kijamii na vile mtu anavyohangaikia kwa ajili ya maisha yake. masoni wanajitahidi kueneza itikadi hii ulimwenguni kote”. Selami Isindag masoni wa ngazi ya juu wa kituruki ameandika hivi; kwa mujibu wa masoni ili kuwatoa wanadamu katika imani ya nguvu za kiungu inayotokana na maandiko ya dini, ni lazima yajengwe maadili yanayotokana na upendo kwa walimwengu.

Katika kanuni zao za maadili masoni wamezingatia umbile la mwanadamu, mahitaji yake na maridhio yao, kanuni za maisha ya jamii na taasisi zao , hiyari, uhuru wa kufikiri na kusema mambo yote yanayojumuishwa katika maisha ya kimaumbile. Kwa sababu hii, lengo lake ni kujenga na kuboresha maadili ya utu katika jamii zote. Hapa bwana Isindag ana maana ya kuwatoa wanadamu katika maadili yanayojengwa na vitabu vya dini. Hii ni kuwatenganisha watu wote mbali na dini.  Katika  kitabu hicho hicho Isindag anafafanua lengo hili pamoja na misingi yake ya kujenga utamaduni ulioendelea;

Misingi madhubuti ya masoni ni ya lazima na inajitosheleza kujenga utamaduni ulioendelea.

Nayo ni kukubali kuwa muasisi mkuu wa Ulimwengu ni evulusheni pekee, kunanusha imani ya ufunuo, usufi na imani nyingine, kuikweza dhana ya utu na kazi. Kipengele cha kwanza hapo juu kinataka watu wakanushe kuwepo kwa Mungu. [masoni hawaamini Mungu

bali wanaamini evolusheni] kipengelea cha pili kinakanusha ufunuo kutoka kwa Mungu. Na kipengele cha tatu kinatukuza dhana ya utu na dhana ya kazi [kama ilivyokuwa katika ukomunisti].Tukitafakari jinsi mawazo haya yalivyojikita katika ulimwengu wa leo, basi twaweza kujionea ushawishi wa masoni ulimwenguni. Jambo jingine la kukumbuka hapa ni je masoni wameziendeshaje harakati zao dhidi ya dini? Tunapoyangalia maandiko ya masoni tunaona kuwa wanakusudia kuingamiza dini hasahasa katika ngazi ya jamii kwa njia ya propaganda. Selami Isindag anatoa mwangaza juu ya jambo hili katika ibara hii ya kitabu chake; Hata tawala za kikatili mno hazikufanikiwa katika jitihada zao za kuingamiza taasisi ya dini. Kwa kweli kutumia kwao mbinu nyingi za kisiasa katika jitihada za kuielimisha jamii ili kuwatoa watu katika imani na masonge ya dini walisababisha upinzani mkali. Nyumba za ibada walizotaka kuzifunga, leo hii zimejaa tele kuliko zilivyokuwa huko nyuma na imani ambayo walitaka kuififiliza imepata wafuasi wengi zaidi. Kwa usemi mwingine tunabainisha kuwa katika masuala yanayogusa nyoyo na hisia, marufuku na mabavu hayafai kitu. Njia pekee ya kuwatoa watu gizani na kuwaleta kwenye mwanga ni sayansi halisia na kanuni za hoja na hekima. Iwapo watu wataelimishwa kwa njia hii wataheshimu upande wa wahumanisti na kujinusuru wenyewe na imani za kibubusa.

Ili kuelewa kinachosudiwa hatunabudi kuichambua ibara hiyo kwa makini. Isindag anasema kuwa ukatili dhidi ya dini utawafanya watu wa dini wawe na ari zaidi na utaiimarisha dini yenyewe. Hivyo basi ili kuifanya dini isiwe na nguvu Isindag anaona kuwa masoni wanapaswa kuiuwa dini katika ngazi ya elimu anachokikusudia katika sayansi halisia na kanuni za hoja na hekima kwa kweli sio sayansi, sio hoja wala hekima. Anachokikusudia yeye ni falsafa ya kihumanisti na kilahidi ambayo hutumia misamiati ya ujanja kama mbinu kama vile inavyoonekana katika nadharia ya itikadi ya Darwin. Isindagi anadai kuwa pale dhana hizi zinaposambazwa katika jamii basi wahumanisti watapata heshima yaani kitakachobaki katika dini ni yale mambo tu yanayokubaliwa na falsafa ya kihumanisti. Wao wanataka kukanusha ukweli wa msingi uliomo katika msingi wa dini ya Mungu mmoja. Kwa kifupi masoni wanataka kufutilia mbali chembechembe za imani zinazojenga msingi wa dini. Wanataka kuitweza kazi ya dini iwe kama kipengele tu cha utamaduni ambacho kinazungumzia tu fikra zake juu ya masuala ya kimaadili. Njia ya kutimiza hili, kwa mujibu wa masoni ni kusimika dhana ya kukanusha Mungu katika jamii kwa kisingizio cha sayansi na hoja.

Na hatimaye kufikia lengo lao na kuiondoa dini katika nafasi yake hiyo ya kipengelea cha utamaduni na hivyo kujenga ulimwengu kamili wa kufuru. Katika makala ya Isindag iiyochapishwa na jarida la masoni liitwalo *“ Positive Science- The obstacles of mind and Mansonry”* anasema matokeo ya haya yote nataka kusema kuwa wajibu muhimu wa masoni sio kuipa mgongo sayansi na hoja kukiri kuwa hii ndio njia bora kwa mujibu wa evolusheni, kueneza imani yetu miongoni mwa watu na kuwaelimisha watu sayansi halisia. Maneno ya Ernest Renan yanabeba uzito zaidi; “iwapo watu wataelimishwa na kuamshwa kwa hoja na sayansi halisia, imani za kibubusa za dini zitaporomoka zenyewe”. Lessing naye anaunga

mkono wazo hili; “iwapo wanadamu wataelimishwa na kuamshwa kwa sayansi halisia ipo siku moja hawatakuwa na haja na dini”hili ndilo lengo kuu la Masoni. Wanataka kuifuta kabisa dini na kujenga Ulimwengu unaoegemeya dhana ya utu yaani wanataka kujenga mfumo mpya wa ujahili ambapo watu wamkanushe Mungu aliyewaumba na wajione wao wenyewe ni Miungu. Haya ndio makusudiyo ya kuwepo kwa jumuiya ya Frimasonri

## Ulemavu wa hoja za wahumanisti juu ya Dini

Ulemavu wa hoja ya Wahumanisti juu ya Dini pia umedhihirika katika fani ya kisaikolojia. Ile hekaya ya Freud, msingi wa dhana ya ukafiri imefutiliwa mbali kuwa ni uwongo mtupu tokea mwanzoni mwa karne ya ishirini, hekaya hiyo imebatilishwa na data za uchunguzi. Patrick Glynn wa chuo kikuu cha George washington analifafanua jambo hili katika kitabu chake kiitwacho *God: The Evidence, The Raconciliation of Faith and Reason in Post secular World*.

---

Ngwe ya mwisho ya karne ya ishirini haikuuendekeza mtazamo wenye mushikeli kiakili. Muhimu zaidi ni kuanikwa hadharani kwa fikra za Freud juu ya Dini (ukiacha mambo mengi mengine) kwamba ni potofu kabisa. Utafiti wa kisayansi katika saikolojia, katika kipindi cha miaka 25 iliyopita umeonesha kuwa, badala ya kuwa bumbuwazi kama Freud na wafuasi wake walivyodai, imani ya dini ni moja ya mambo yanayowiana mno na afya ya akili na maisha ya furaha. Utafiti mmoja baada ya mwingine umeonesha uhusiano madhubuti baina ya imani na mwenendo wa kidini kwa upande mmoja, na maadili kwa upande mwingine, hasa kushughulikia matatizo kama vile vifo vya kujiua, ulevi, madawa ya kulevya, mfadhaiko, mipaka ya starehe ya ngono ndani ya ndoa. Kwa kifupi, ile iliyodhaniwa kuwa hoja ya kisayansi nyuma ya dhana ya Uhumanisti imethibitika kuwa haina ukweli, na ahadi zake zimeishia patupu.

Hata hivyo wadau wa dhana hii hawajaachana na falsafa yao, badala yake wameendelea na jitihada za kuieneza Duniyani kote kwa njia za propaganda. Hasahasa katika nyanja za sayansi, falsafa, muziki, fasihi, sanaa na sinema. Ujumbe wenye mvuto lakini wa uongo ulitungwa na wanaitikadi wa kihumanisti umekuwa ukipandikizwa kwa watu. Wimbo uitwao *“Imagine”* ulitungwa na Johnn Lennon, mpiga gitaa wa kundi mashuhuri la muziki liitwalo “The Beatles” ni mfano wa propaganda hizo.

Wimbo unasema; “Itakidi hakuna pepo.
Ni rahisi tu hebu jaribu.
Hakuna Jahannamu.
Juu yetu kuna anga tu.
Itikadi watu wote wanaishi hapa tu.
Hakuna cha kuuliyana wala cha kufiya.
Na wala hakuna Dini.

Huwenda mtasema labda naota ndoto lakini siko peke yangu.
Natumai siku moja mtaungana nasi na Duniya itakuwa moja".

Wimbo huu ulichaguliwa kama "wimbo wa Karne"katika kura kadhaa za maonizilizopigwa mwaka 1999. Baada ya kukosa msingi wa kisayansi na wa hoja, uhumanisti unapandikizwa kwa njia za namna hii. Dhana ya humanisti haina uwezo wa kujenga hoja za kupinga Dini na ukweli, inajaribu tu kutumia mbinu za kupumbaza kama hizi. Pale ahadi za ilani ya mwaka 1933 ya wahumanisti ziliposhindikana, ikapita miaka arobaini ambapo baada ya miaka hiyo wahumanisti wakawasilisha rasimu ya pili.

Mwanzoni mwa kitabu, lilifanyika jaribio la kuelezea kwa nini ahadi za kwanza zilishindikana. Licha ya ukweli kwamba ufafanuzi ulikuwa hafifu lakini bado Wahumanisti wakakumbatia falasafa yao. Kipengele kikuu cha manifesto hii kilikuwa kile cha kulinda msingio wa kukana Dini kwa ilani ya 1933. Kama ilivyokuwa mwaka 1933, wahumanisti bado wanaamini kuwa imani ya jadi ya Mungu mmoja, hasahasa imani ya Mungu anayesikia maombi (sala), anayedhaniwa kuwa yu hai na anawaangalia watu, akisikia na kuelewa sala zao na kuweza kuwafanyia jambo fulani, ni imani isiyo na ushahidi na imepitwa na wakati. Sisi tunaamini kuwa Dini za jadi za kibubusa au za nguvunguvu ambazo zinaweka ufunuo, Mungu, ibada au itikadi juu ya mahitaji na maisha ya binaadamu haziwasaidii kitu binaadamu. Sisi kama wapinzani wa imani hiyo, tunaanza na binaadamu sio Mungu. Kwa kweli haya ni maelezo ya juujuu sana. Ili kuielewa Dini, kwanza mtu anahitaji akili na mafuhumu kuweza kuelewa mambo ya ndani mno. Kitu cha kwanza ni ukweli wa moyo na kuepuka chuki. Jitihada za wahumanisti kuielezea imani juu ya Mungu na 'Dini za Mungu Mmoja' kuwa haina msingi na imepitwa na wakati si jitihada mpya, ni mwendelezo wa dai lilelile, ambalo limetolewa kwa maelfu ya miaka na wale wanaomkana Mwenyezi Mungu.

Katika Qur'an, Mwenyezi Mungu analielezea dai hili kongwe lilitolewa na wale wasioamini. Mungu wenu ni Mungu mmoja. Lakini wale wasioamini akhera nyoyo zao zinakataa, nao wanatakabari. Bila shaka Mwenyezi Mungu anayajua wanayoyaficha na wanayoyadhihirisha. Kwa hakika yeye hawapendi wanaotakabari. Na wanapoambiwa (makafiri) "Mola wenu ameteremsha nini? Wanasema'hadithi za uwongo za watu wa zamani" Qur'an (16-22-24). Aya inabainisha kuwa sababu halisi ya wasioamini kuikataa Dini sahihi ni kiburi kilichomo nyoyoni mwao. Falsafa inayoitwa 'humanism' ni taathira ya nje ya kiburi hicho cha kumkana Mungu. Kwa maneno mengine 'humanism' sio utaratibu mpya wa fikra kama wanavyodai wale wanaounga mkono dhana hii. Ni fikra kongwe ambayo wamekuwa nayo wale wote wanaomkadhibisha Mungu kwa jeuri.

## Mizizi ya dhana ya Ukomunisti katika Kaballa

Tumeona kuwa Kaballa ni itikadi ya zamani ya Misri na ikaingia na kuchanganyika na dini iliyofunuliwa na Mungu kwa WanaIsraili. Aidha tumeona kuwa msingi wa Kaballa ni

welewa potofu kuwa binadaamu hawakuumbwa. Dhana ya Ukomunisti iliingia Ulaya kwa msingi wa itikadi hii ya Kaballa. Imani ya Kikristo ilijengwa kwa msingi wa imani ya kuwepo kwa Mungu, na imani kuwa Wanadamu ni waja wake walioumbwa naye. Lakini kwa kule kuenea kwa utamaduni wa Matempla sehemu zote za Ulaya, Kaballa ikaanza kuwavutia Wanafalsafa wengi. Kwa hali hiyo, katika karne ya 15 ikaibuka hii dhanna ya sasa ya "humanism" na imeacha taathira zisizofuta katika uimwengu wa fikra wa Ulaya. Uhusiano huu wa humanism na Kaballa umeelezwa zaidi katika vitabu kadha wa kadha. Mojawapo ya vitabu hivi ni kitabu cha Mwandishi mashururi Malachi Martin, kiitwacho *The keys of this Blood*. Martin ni Profesa wa Historia katika chuo cha mafunzo ya uaskofu na Biblia cha Vatican-Vatican's Pontifical Bible Institute: Yeye anasema kuwa athari za Kaballa zadhirihirika wazi kwa Wakomunisti. Katika mazingira ya kuatatanisha na kwa changamoto iliyoweka historia y awali ya Italia, ukaibuka mtandao wa jumuiya za kihumanisti. Jumuiya hizi, mwanzoni zilikuwa za siri. Mbali na usiri jumuiya hizi zilizkuwa na sifa kuu mbili.

Sifa ya kwanza ni kwamba zilipinga tafsiri iliyozoeleka ya Biblia kama ilivyodumishwa na mamlaka za kikasisi na za kijamii na pili zilizpinga misingi ya kifalsafa na kitheolojia iliyotolewa na Kanisa kwa ajili ya maisha ya kijamii na kisiasa. Kwa kifupi jumuiya za kihumanisti zilizoundwa katika kipindi hicho zilizotaka kuingiza utamaduni mpya wenye mizizi ya Kaballa ndani ya utamaduni wa kikatoliki barani Ulaya. Zilikusudiya kuleta mabadiliko ya kijamii na kisiasa. Mbali na Kaballa katika msingi wa utamaduni huu mpya pia kulikuwa na itikadi za misri ya kale. Prof. Martin ameandika. Waasisi wa zile jumuiya za Kihumanisti walikuwa Waumini wa nguvu kuu- Mwasisi mkuu wa Ulimwengu-ambaye walimwakilisha kwa sura ya Tetragramatton-neno la herufi nne YHWH..(Wahumanisti) wakaazima alama nyingine –Piramid na jicho moja linaloona mambo yote..kutoka kwenye vitabu vya Misri. Wahumanisti Wanatumia dhana ya mkuu wa ulimwengu-Great Architect of the universe; Msamiyati unaotumiwa na Masoni hadi leo. Hii inaonesha kuwa lazima yawepo mahusiano kati ya Wahumanisti na Masoni.

## Alama za Misri ya kale katika maskani za Masoni

Moja kati ya mambo muhimu yanayothibitisha uhusiyano kati ya Misri ya kale na Masoni ni zile alama zao. kwa Masoni alama ni kitu muhimu sana. Masoni wenyewe hubainisha maana ya falsafa yao kwa wanachama wao kwa njia ya alama. Masoni anayepanda ngazi kati ya ngazi 33 za mamlaka ya kimasoni hujifunza maana mbalimbali za kila alama katika kila hatua. sote twajua kuwa Masonri huelezea dhana zake na maadili yake kwa njia ya alama na hadithi yaani tamthilia. Tamthilia hizi hurejea historia ya zama za nyuma. Twaweza hata kusema kuwa zinagusia hekaya za nyuma kabisa ya historia. Kwa utaratibu masonri imeonesha mambo ya kale ya mafundisho yake. Dhana za Wamisri wa zamani ndizo zinazowakilishwa na alama hizi . Kila mahala katika maskani za masoni na mara kwa mara katika machapisho ya masoni michoro ya mapiramidi na masanamu huonekana. Iwapo tutaichagua Misri ya kale kuwa ni jamii kongwe zaidi, sidhani kama tutakuwa tumekosea.

Isitoshe ule ukweli kuwa ibada, na falsafa inayokutikana katika Misri ya kale ndiyo hiyo hiyo iliyomo katika masonri, unavuta hisia zetu. Katika zama za kale za Misri ibada za awali katika hekalu la *Memphis* zilizodumu kwa muda mrefu, zilifanywa kwa mazingatio makubwa na shauku kubwa na zimeonesha mlingano na ibada za kimasoni. Hebu tuiangalie mifano michache ya uhusiano kati ya Misri ya kale na masoni.

Piramidi chini ya jicho; Alama mashuhuri kabisa ya masoni inaonekana katika nembo (ngao) ya Taifa la Marekani. Katika nembo hii kuna nusu Piramidi ambapo juu yake kuna jicho ndani pembe tatu. Jicho hili ndani ya pembe tatu ndiyo alama ya kudumu inayokutwa katika maskani za masoni na katika machapisho yao yote. Idadi kubwa ya maandiko yanayozungumzia masoni husisitiza ukweli huu. Lile *Piramid* chini ya jicho ndani ya pembe tatu lenyewe lina mvuto mdogo sana. Hata hivyo piramidi hili lina maana kubwa mno ya kufahamia falsafa ya masoni. Mwandishi ya kimarekani Robert Hieronimus amendika tasnifu ya kiitikadi juu ya nembo ya Marekani ambapo ametowa maelezo muhimu sana. Anuwani ya tasnifu ya *Hieronimus ni "An Historic Analysis of the Reverse of the America great seal and its relationship to the Ideology of Humanist Psychology"* (utafiti wa kihistoria wa siri ya nembo kuu ya Marekani na uhusiano wake na itikadi ya saikolojia ya kihumanisti). Tasnifu yake inaonesha kuwa waasisi wa America ambao kimsingi walitumia nembo hiyo walikuwa ni Masoni na hivyo waliiunga mkono falsafa ya kihumanisti. Uhusiano kati ya falsafa hii na Misri ya kale unabainishwa na alama ya Piramidi iliyowekwa katikati ya nembo hiyo. Piramid hili linawakilisha Piramidi la Cheops moja ya minara mikubwa kabisa ya Firauni.

Maana ya nyota ya pembe sita ya Masoni;Alama nyingine mashuhuri ya masoni ni nyota yenye pembe sita iliyoundwa kutokana na pembe tatu kuwa juu ya pembe tatu nyingine. Hii pia ni alama ya utamaduni wa Wayahudi na leo hii inaonekana kwenye bendera ya Israel. Inafahamika kuwa kwa mara ya kwanza Nabii Suleiman aliitumia kama nembo. Hivyo basi nyota ya pembe sita ni nembo ya Nabii na alama ya kiungu lakini Masoni wana dhana tafauti. Wao hawaikubali nyota ya pembe sita kama alama ya Nabii Suleiman, bali wanasema ni alama ya itikadi ya kipagani ya Misri ya kale. Makala yenye kichwa '*Allegory and symbols in our Rituals'* [Isitiari na alama katika ibada zetu] iliyochapishwa katika jarida la Mimar Sinan, inaelezea mambo mengi kuhusu jambo hilo kama ifuatavyo; mchoro wa alama mbili za pembe tatu moja juu ya nyingine unaonesha kuwa zina thamani sawa. Alama hii inayotumiwa na Masoni inajulikana kama nyota ya Daud, ni mchoro unaotokana na alama moja ya pembe tatu kuwa juu ya alama nyingine ya pembe tatu, leo hii inajulikana kama alama ya Uyahudi na inaonekana katika bendera ya Israel lakini ukweli ni kuwa asili ya alama hii ni Misri ya kale. Nembo hii kwanza kabisa ilitengenezwa na Matempla, ambao waliitumia kama urembo katika nakshi za kuta za Makanisa yao. Hii ni kwa sababu wao ndio walikuwa watu wa kwanza kugundua mambo muhimu kuhusu Ukristo mjini Jerusalem. Baada ya Matempla kusambaratishwa alama hii ikaanza kutumika katika Masinagogi. Lakini kwa Masonri bila shaka tunaitumia alama hii kwa maana ya jumla ya Ulimwengu mzima kwamba ilitokea katika

Misri ya kale.  Kwa maana hii tumeunganisha nguvu mbili pamoja. Kwa kweli hatuna budi kuzitafsiri alama zote za masoni kwa mnasaba wa hekalu la Selemani. Kama ilivyobainishwa na Qur'an Selemani alikuwa Nabii ambaye baadhi ya watu walitaka kumpaka matope na kuonesha kwamba hakuwa Muumini wa Mungu mmoja. Katika aya hii ya Qur'an Mwenyezi Mungu anasema; "Wakafuata yale waliyoyafuata mashetani, wakadai yalikuwa katika Ufalme wa Nabii Suleiman, na Suleiman hakukufuru" [2:202].  Masoni wamejenga dhana hii kimakosa kwa kumsingizia Nabii Seleman kuwa ni muwakilishi wa itikadi za kipagani za Misri ya kale kwa sababu hiyo wanampa nafasi muhimu katika itikadi zao.  Katika kitabu chake "*The occult Conspiracy*" mwanahistoria wa kimarekani Michael Hoarld anasema kuwa tangia zama za kati, Suleiman (astaghfirullah!) amekuwa akisadikiwa kama "mchawi" na kwamba yeye ndiye aliyetumbukiza mawazo ya kipagani ndani ya dini ya Uyahudi!

Hoarld anaendelea kueleza kuwa masoni wanaliitakidi hekalu la Seleman kuwa ni hekalu la kipagani, na kwa sababu hiyo ni muhimu kwao. Picha hii potofu anayopachikwa Nabii Seleman, ambaye alikuwa mja mnyenyekevu na mtiifu kwa Allah (s.w) inabainisha misingi ya Masonry.

Alama ya nguzo mbili; Alama nyingine muhimu katika maskani ya Masoni ni ile ya nguzo mbili katika lango la kuingilia. Maneno "Jachin" na "Boaz" yamechongwa juu ya nguzo kwa kuiga nguzo mbili kwenye lango la hekalu la Selemani. Lakini kwa kweli Masoni hawana maana kuwa nguzo hizi ni alama ya kumbukumbu ya Seleman bali ni ishara ya mambo ya kumuhujumu Seleman. Chanzo cha nguzo hizi ni Misri ya kale. Makala yenye kichwa 'Allegory and symbols in our Rituals' inaeleza hivi; kwa mfano nchini Misri Horus na Set walikuwa waanzilishi pacha na washikiliaji wa mbingu.  Nguzo mbili katika maskani zetu asili yake ni Misri ya kale. Moja kati ya nguzo hizi ilikuwa kusini mwa Misri katika jiji la Thebes, na nguzo nyingine ilikuwa kaskazini katika mji wa Heliopolis. Katika lango la kuingilia hekalu la Amenta lililotengwa kwa ajili ya Ptah Mungu mkuu wa Misri kulikuwa na nguzo mbili kama zile zilizopo kwenye hekalu la Selemani.Katika riwaya za kale zinazohusu Jua nguzo hizo zinatajwa zikipewa majina ya akili na kipawa.

## Istilahi za Kimisri zitumiwazo na Masoni

Katika kitabu chao, The Hiram Key, Masoni wa Kiingereza Christopher Knight na Robert Lomas, wanaonesha mizizi ya Masoni katka jamii ya wamisri wa zama zilizopita. Jambo muhimu wanalofichufua ni kuwa maneno yatumikayo katika hafla ya kumpandisha masoni ngazi iitwayo *Master Mason* ni; ma'at-neb-men-aa,ma'at-baa' na. Knight na Lomas wanaeleza kuwa maneno haya, mara nyingi hutumiwa bila kuzingatia maana yake, lakini ni maneno ya Wamisri wa zama za nyuma, ambayo yana maana hii; "Great is the established master of freemasonry, great is the spirit of Freemasonry" "Aliyepandishwa ngazi ya masta Masoni juu, juu zaidi, mori wa masoni juu, juu zaidi"

Waandishi hawa wanasema kuwa neno Ma'at maana yake ni ufundi wa majengo[maboma] na tafsiri ya karibu zaidi ya neno hilo ni masonry yaani uwashi. Hii ina maana kuwa Masoni wa hivi leo bado wanaienzi lugha iliyotumika maelfu ya miaka iliyopita katika Misri ya zama hizo.

## Filimbi ya wachawi ya Mozart

Mojawapo ya vitu vilivotengenezwa na Masoni ni filimbi ya wachawi *magic flute*, huu ni wimbo wa mtunzi mashuhuri wa nyimbo aliyeitwa Mozart. Mozart alikuwa Masoni. Ni jambo linalofahamika kuwa sehemu kubwa ya wimbo huo ina ujumbe wa Masoni. Na ujumbe huu unanasibiana kwa karibu na upagani wa Misri.  Jarida la *Mimar Sinan* linafafanua jambo hili kama ifuatavyo;

Yafahamika kuwa, kuna uhusiano wa wazi kati ya ibada za Misri ya zama za nyuma na ibada za Kimasoni. Hata wakijaribu vipi wale wanaojaribu kuitafsiri filimbi ya wachawi kwamba eti ni hadithi tu kuhusu mashariki ya mbali, lakini msingi wake ni ibada za Wamisri. Ni miungu wa kiume na wa kike wa mahekalu ya Misri ambao wameshajiisha utunzi wa maneno ya filimbi ya wachawi.

## Minara ya pembe nne iliyochongoka juu

Alama nyingine muhimu ya Masoni ni obelisk. Huu ni mnara mrefu wa pembe nne , umechongoka kwa juu, ambao ni sehemu ya ubunifu majengo wa Misri ya kale. Piramidi ndio ncha ya mnara huu. Minara hii ilichongwa na wasanii wa uchongaji wa Misri ya kale. Kwa karne nyingi ilikuwa imezikwa chini hadi pale ilipokuja kuoenekana mnamo karne ya kumi na tisa. Ikahamishiwa kwenye miji mikuu ya nchi za Magharibi kama vile New York, London na Paris.

Mnara mkubwa kabisa kuliko yote ulipelekwa Marekani. Mpango wa kuupeleka huko ulifanywa na Masoni. Hii ni kwa sababu minara hiyo pamoja na michoro yake inadaiwa na Masoni kuwa ni alama zao halisi. Jarida la Masoni linataja mnara wenye urefu wa mita 21 uliopo New York. Mfano hai wa minara hii ni mnara uitwao Cleopatra's needle, uliotolewa na Gavana wa Misri bw. Ismail kama zawadi kwa Marekani mwaka 1878. Mnara huu hivi sasa upo katika eneo la center park la NewYork. Sehemu yake ya chini imesilibwa kwa nembo za Kimasoni. Huu ni mnara ambao kwanza kabisa uliirikwa mnamo karne ya kumi nasita kabla ya Yesu, kwenye lango la kuingilia ndani ya hekalu la *Sun god* katika eneo la Heliopolis.

## Hadithi ya mjane

Dhana muhimu ya utambulisho wa Masoni ni ile ya mjane. Masoni hujiita watoto wa mjane, na picha za wajane mara nyingi huonekana katika machapisho yao. Ni nini chanzo cha dhana hii? Huyu mjane ni nani? Tunapoyapekua maandiko ya Masoni, tunaona kuwa alama ya mjane kimsingi inatokana na hadithi ya paukwa pakawa ya Wamisri wa zamani za kale. Hii ni hadithi ya Osiris na Isis. Osiris alikuwa mungu wa kimila na Isis ndio mkewe. Kwa mujibu wa hekaya hii, Osiris alikuwa muhanga wa kifo cha mahaba "*a victim of a crime of passion"*ambapo Isis akawa mjane. Kwa hiyo mjane huyo wa Masoni ni Isis.

Makala moja katika jarida la *Mimar Sinan* inalifafanua jambo hili kama ifuatavyo; Hadithi ya Osiris na Isis inazungumziwa sana katika makala nyingi na katika mihadhara mingi. Ni moja ya hadithi za Misri ya kale zinazohusishwa mno na Masoni. Sifa ya kuwa kasisi wa hekalu la Isis ni ile ya mtu kuwa na uanachama wa masoni. Humo mwangaza wa jua huwa tunu muhimu ili mtu azikwe kwenye giza la mashariki, kila siku jua la asubuhi linapoanza kutua mchana, hufanya kazi ya Osiris , kama vile Horus kwa nuru yake kubwa, alivyochukua nafasi ya baba yake aliyeuawa. Hivyo mjane ambaye watoto wake ni sisi si mwingine zaidi ya Isis mjane wa Osiris. Tunaona kuwa masonri ambayo inajieleza kuwa imejengeka kutokana na akili na sayansi, kwa kweli ni hadithi ya paukwa pakawa iliyojaa imani za ajabu ajabu za uchawi.

## Bikari na pimamraba

Bikari (*compass)* na pimamraba (square) ni miongoni mwa alama mashuhuri za masoni. Bikari huwekwa juu ya pimamraba. Masoni wanapoulizwa juu ya alama hii, husema kuwa alama hiyo huwakilisha dhana za sayansi, jiometri na kipawa cha akili. Lakini kwa kweli alama hizo zina maana nyingine kabisa.

Tunaweza kuiona maana hii katika kitabu kilichoandikwa na mmoja wa Masoni mashuhuri, Albert Pike. Katika kitabu chake kiitwacho *Marals and Dogmas*, ameandika hivi; Pimamraba … ni alama ya kimaumbile inayowiyana na duniya hii. Ni alama ya mke na mume. Ni alama ya asili mbili ambayo hapo kale ilihusishwa na mungu,,… Braham na Maya kwa Waariyan, Osiris na Isis kwa Wamisri. Kwa vile jua ni dume basi mwezi ni jike.

Hii ina maana kuwa pima mraba na bikari , nembo mashuhuri ya masoni, ni alama ya wapagani wakiariyani ambayo historia yake inaanzia Misri ya kale kabla ya Ukristo. Mwezi na Jua katika nukuu hiyo ya Pike ni alama muhimu katika jumuiya ya Masoni na haina maana nyingine zaidi ya kuwa kielelezo cha imani potofu za jamii za kale ambazo ziliabudu mwezi na jua.

## Falsafa ya kipagani ya masoni

Hadi hapa tulipofika, tumejifunza kuwa misingi ya masoni imeegemeya itikadi ya kipagani inatokeya Misri ya kale na kwamba huko ndiko inakofichama maana halisi ya dhana na alama za masoni. Kwa sababu hiyo, masoni wanapingana na dini zinazoamini mungu mmoja. Masonri ndio itikadi ya wahumanisti, walahidi, na wanaevolusheni. Mwana historia wa Kiamerika, Michael Hoard anaielezea siri hii ambayo hufichuliwa kwa masoni wa ngazi za juu tu. Kwa nini Wakristo wanaikosoa Frimasonri?….. Jibu la swali hili lipo katika siri za Frimasonri. Laiti "siri hizi" zingetolewa hadharani, inatia shaka kama maana ya "siri hizo" ingeliweza kueleweka kwa wale ambao hawakuyajua mafundisho ya jamii za kichawi na dini ya kale. Kwa kweli yatia shaka kama wadau wa kawaida wa masoni wanaelewa "siri hizi" zinawakilisha nini. Katika duru za ndani za masoni, *Inner cicle of Masonry*, miongoni mwa wale waliopata daraja za juu, wamo wanaoelewa kuwa, wao ni warithi wa utamaduni wa kale uliokuwepoa kabla ya Ukristo ambao ni wa zama za upagani. Tukitazama andiko la masoni wa Kituruki, tunaona kuwa wale masoni wa ngazi za juu ndio tu wenye kujua mambo ambayo wenzao wengine wanafichwa. Masta masoni Necdet Egeran anaelezea jinsi masoni wa ngazi za juu wanavyolitazama jambo hili.

Kwa upande mwingine, Frimasonri ni Shirika jingine la Wayahudi. Uanachama wa Shirika hili umegawanyika katika ngazi mbalimbali zinazoitwa *"Degrees.*" Ili kuingia katika kila ngazi , kuna sheria na kanuni mahususi zinazoambatana na masharti maalum. Mtu anayehusika na ngazi fulani anaweza tu kusuhubiana na mwanachama wa ngazi hiyo hiyo na uhusiano huu hutazamwa kwa makini sana kiasi kwamba mdau anayehusiana na ngazi fulani hawezi kusikia mipango, shabaha wala malengo ya siri ya wadau wa ngazi nyingine.

Malengo ya ngazi za juu za Frimasonri yanafichwa na kuhifadhiwa kwa siri kubwa kwenye faili nyeti mno kiasi ambacho mtu anaweza kupitisha hata maisha yake yote ndani ya shirika hili bila kuambulia kitu. Mbinu za jumuiya hii na njia za ufanyaji kazi wake ni za siri kubwa kiasi kwamba *Encyclopedia Britannica* ambayo ina habari nyingi juu ya masuala mengi, imelazimika kukiri kuwa ushahidi ni haba sana kuwezesha undani wa *lodges* kung'amuliwa. Kumbukumbu za *lodge* na mambo yanayoihusu "zinafichwa" kwelikweli ambapo wale wasio wanachama hawawezi kusikia hata neno moja kuhusiana zao. Wanachama Frimasonri huwasiliana kwa mfumo maalum wa maandishi *(code)* na huwatambua wanachama wenzao kwa mfumo wa siri wa alama na maneno. Pia wana utaratibu wa kivyao wa kubishiana (kupigiana) hodi milangoni mwao ambapo wenyewe huweza kutambuana haraka hasa wanapokuwa katika nchi za kigeni.

Mdau Frimasonri anapofanya ziara katika nchi ya kigeni, hahitaji utambulisho rasmi kwa wadau wenzie mahala popote pale. Yeye anachohitaji ni kuwa na anuani tu kisha ule utaratibu maalum wa kupiga hodi humfanya yule aliyemo chumbani kutambua na kwenda mlangoni kumkaribisha. Katika mikusanyiko na mikutano na katika hafla ndani ya nchi mbalimbali wao

hutambuana na kusabahiana bila shida yoyote na bila kusemeshana hata neno moja. Hujuana na kusalimiana kwa njia ya alama, maneno ya siri, ishara na uchezeshajichezeshaji wa mikono na viwiliwili vyao. Kwa mfano alama yao kuu ni pembe tatu ambayo wenyewe huuita *EYE*.

Iwapo Masoni yupo katika mazingira ya ugenini na anataka kujua kama kuna wenzie wangapi katika hafla ya kijamii na kadhalika au kama yeye ndiye anayetaka kujitambulisha kwa masoni waliopo kwenye umati wa watu, kitu pekee anachotakiwa kufanya ni kuweka vidole vyake vya mkono katikati ya vifungo[vishikizo] vya koti lake au kizibao chake na kufanya alama ya pembe tatu kwa vidole vyake kwa upande mmoja na pindo la koti kwa upande mwingine. Wanachama wenzie wote waliopo hapo mara moja watamuitikia kwa ishara na pia kila mmoja atawajua wengine bila kusemeshana neno. Masoni hupendelea kuwaingiza katika jumuiya yao Viongozi wakuu wa nchi, Viongozi wa kiraia au viongozi wa kijeshi au Vigogo wa makampuni ya biashara ya wenyeji na wageni. Hakuna kipingamizi cha tabaka,rangi , dini wala utaifa katika kujiunga na jumuiya hiyo.

Bali viongozi wa nchi hushawishiwa zaidi na wakitiwa mkononi, huendeshwa kwa mujibu mpango uliowekwa. Wanatumiwa kwa namna ambayo wenyewe hawawezi kuyatambuwa malengo yaliyofichikana ambayo yanatimizwa kupitia kwao. Pengine kuna watu wawili watatu tu au pengine hakuna hata mmoja mwenye asili ya utaifa wa kiyahudi ambaye ni mwanachama wa umoja huu wa siri katika nchi. Lakini jumuiya daima hutimiza malengo ya Uzayuni [mtandao wa kimataifa wa wayahudi]. Jumuiya hii kwanza ilianzishwa Uingereza mnamo mwaka 1717. muungano wa lodges zipatazo nne ukaunda Lodge kuu *grand lodge* mjini London pamoja mfumo mpya wa alama za siri. Kuhusiana na kazi na majukumu ya Masoni, pitio la itifaki litafichua ukweli. Haya ni maelezo yanayobainisha kila kitu, na serikali inayotaka kuinusuru nchi yake na hatari ya malengo ya chombo hiki chenye nguvu na ushawishi, basi haina njia nyingine ila kuking'olea mbali. Hapana shaka hiyo haitakuwa kazi rahisi kwani mizizi ya shirika hilo imeota ndani kabisa ya mfumo wa serikali ya nchi. Kwa kweli mikono ya masoni ni mirefu mno.

## Masoni maana yake ni kuachana na dini

Tunapoyatupiya macho maandiko ya Masoni, tunaona kuwa Masoni wa ngazi za juu wanaelewa mambo ambayo wenzao wa ngazi za chini wanafichwa wasiyajuwe. Masoni wa ngazi ya juu aitwaye Necdet Egeran anafafanuwa kuwa;

Baadhi ya Masoni huelewa kuwa Mansori ni aina ya **nusu-dini** na **nusu -Taasisi** ya hisani ambapo wanaweza kujenga uhusiyano na kuyaendesha kwa utaratibu huwo. **Wengine wanadhani kuwa Lengo la Masonri ni kuwafanya watu wawe tu wema zaidi. Aidha wengine wanaona kuwa Mansori ni Taasisi ya kujenga maadili. Kwa kifupi wale**

**wasiojuwa kusoma wala kuandika lugha ya Masoni wanaelewa alama na hekaya za masoni kwa maana hii au kwa maana iliyosawa na hii. Lakini kuna masoni wachache sana wanaoweza kujuwa undani wa mambo.**

Mansori iko tafauti kabisa na malengo hayo. Mansori maana yake ni Elimu ya ufunuwo, kujibuwa na kuanza upya. Maana yake ni kuachana na utaratibu wa zamani wa maisha na kuingiya katika maisha mapya na matakatifu zaidi. Katika siri ya chimbuko la Masonri na katika msingi wa dhana ya alama, kuna msururu wa siri zinazotusaidiya kuingiya katika maisha ya ndani zaidi na kujuwa siri ya maisha yetu. Hivyo, ni katika maisha haya ya ndani zaidi na kwa kuingiya katika maisha hayo ndipo inapowezekana kupata elimu ya Masonri. Hapo tu ndipo inapowezekana kuujuwa undani na nyendo za maendeleo na mageuzi.

Nukuu hiyo inabainisha kuwa japo Masoni wachache wa ngazi ya chini huwona kuwa masonri ni Taasisi ya hisani na ya kijamii, lakini kwa kweli inahusiyana na siri za maisha ya Mwanadamu yaani haiba ya nje ya mansori kama shirika la hisani na la kijamii, kwa kweli ni mwavuli tu wa kufunika falsafa ya jumuiya hiyo. Kwa uhalisi wake Mansori ni shirika lenye shabaha ya kushajiisha falsafa fulani kwa wadau wake na kwa watu wengine kwa kutumiya mfumo maalumu. Kama tulivyosema mwanzoni, kipengele cha msingi cha falsafa hii ambacho kimepandikizwa kwa masoni kutoka tamaduni za kipagani hasa hasa upagani wa Misri ya kale ni Ukafiri.

## Ukafiri katika vitabu vya Mansori

(1) Imani juu ya maada inayojitegemeya

Mansoni wa hivi leo **,** kama walivyokuwa mafirauni, makuhani na matabaka mengine ya jamii ya Misri ya zamani, huamini umilele wa maada na dhana ya maada kutoumbwa na Mungu Muumba, na kwamba kutokana na maada hii isiyo na uhai, viumbe hai vikazuka kwa bahati nasibu. Katika maandiko ya Masoni, tunapata maelezo ya kina ya vipengele vya msingi vya falsafa ya ukafiri. Katika kitabu chake, *Mason luktan Esin meleler* (Funuwo za Frimasonri, Masta Mason Selami Isindag ameandika kuhusu falsafa hii ya ulahidi:

“Anga lote, angahewa, Nyota, Silika, vitu vyote vilivyo hai na visivyo hai vinajengwa na Atomu. Wanadamu si chochote bali ni mkusanyiko tu wa Atomu uliojizukiya wenyewe kibahati bahati. Ule Urari katika mtiririko wa umeme kwenye Atomu ndio unaouhakikishiya uhai viumbe hai. Pale urari huu unapovurugika, ndipo tunapokufa, tunarejeya udongoni na kusambazika katika chembechembe za Atomu.

Yaani sisi viyumbe tumetokana na Atomu na nishati, na tutarudi tena katika maada na nishati. Mimeya hutumiya Atomu zetu na viumbe vyote hai tukiwemo sisi hutumiya mimeya. Kila kitu hutengenezeka kwa vitu hivyo. Lakini kwa vile ubongo wetu umekuwa zaidi ya wanyama wote, akili ikazuka. Tukiyangaliya matokeyo ya uchunguzi wa kisaikolojiya, tunaona kuwa maisha ya utu wetu wenye sehemu tatu za hisiya, akili na hiyari ni matokeo ya utendaji kazi madhubuti wa seli katika tabaka la nje la ubongo na homoni.

....Sayansi yakinifu inakubali kuwa hakuna kilichopata uhai kutokana na hamna kile na hakuna kitakachotoweka kabisa kabisa. Kwa hiyo yaweza kuhitimishwa kuwa hakuna muweza yeyote ambaye watu wanahitaji kumshukuru na kuwajibika kwake.

Ulimwengu huu ni mkusanyiko tu wa nishati isiyo na mwanzo wala mwisho. Kila kitu kinazalishwa kutokana na mkusanyiko huu wa nishati, huibuka na kufa lakini hakitoweki moja kwa moja. Vitu hubadilika na kubadilika hali na muundo. Hakuna mambo kama vile kifo au kutoweka; Yapo tu mabadiliko yanayoendeleya daimadumu, mabadiliko ya hali moja kwenda nyingine na mabadiliko ya muundo wa kitu. Lakini ni vigumu kulifafanuwa jambo hili kubwa na ni vigumu kufafanuwa siri za ulimwengu kwa kutumiya kanuni za kisayansi. Lakini fafanuzi nyingine zaidi ya zile za kisayansi ni yale maelezo yatokanayo na njozi tu, imani tu ya kibubusa na tena ni Imani ya kipumbavu. Kwa mujibu wa sayansi yakinifu na hoja ya kiyakili, hakuna roho inayotengana na mwili.

Hapa msomaji ataona fikra zinazofanana kabisa na zile za vitabu vya wanafikra wanaokanusha Muumba kama vile: K. Marx , F,. Engels, B. I. Lenin, G.Politzer, C.Sagan na J. Monod. Wote hawa wanaamini dhana ya msingi ya ulahidi kuwa ulimwengu umekuwepo wakati wote. Maada ndiyo muhimili pekee wa maisha. Wanadamu wanajengeka kwa maada na hawana roho. Maada ndiyo iliyomjenga mtu ndani na nje na uhai ukatokeya kwa bahati nasibu. Ni sahihi kutumiya neno dhana kwani kinyume na dai la Isindag kuwa maelezo haya yanatokana na sayansi yakinifu na hoja ya kiakili, fikra zote hizi zimebatilishwa (zimefutiliwa mbali) na vumbuzi za kisayansi katika nngwe ya pili ya karne ya Ishirini.

Kwa mfano nadhariya ya mlipuko mkuu inayokubalika katika duru za kisayansi kuwa ni sahihi, inabainisha kisayansi kwamba ulimwengu uliumbwa kutokana na **hamna** mamiliyoni ya miyaka iliyopita. Kanuni za *'Thermodynamics'* zaonesha kuwa maada haina uwezo wa kujipangiliya yenyewe na kwamba Urari na mpangiliyo uliyopo ulimwenguni ni matokeyo ya kazi ya uumbaji iliyofanywa kwa nguvu yenye utambuzi. Kwa kule kubainisha kwake usanii wa kuajabisha katika viumbe hai, Baiolojiya inathibitisha kuwepo kwa Muumba aliyeumba vyote[1]. Katika makala yake moja, Isindag anazidi kufafanuwa kwamba, kwakweli Masoni ni Wakanusha Mungu na kwa hivyo ni wapinzani wa Dini zinazoamini Mungu na kwamba wanatumiya dhana ya Great Architect Of the Universe kwa maana ya Evolusheni ya Maada:

**Kwa kifupi sana, nataka kugusiya kanuni na dhanna fulani zinazofuwatwa na Masoni: Kwa mujibu wa Masonri, uhai huwanza na seli moja, inayojibadilsha na kugeuka kutoka hali moja kwenda nyingine na kuendeleya hivyo hivyo hadi kuwa mtu. Chanzo, au sababu, au lengo au mazingira ya mwanzo huu hayawezi kufahamika.**

Maisha hutokana na mchanganyiko wa maada na nishati na kisha hurejeya tena katika vitu hivyo. Anasema endapo tutakubali kuwa Great Architect of the Universe ndiyo msingi mkuu na ndiyo upewo usiyo ukomo wa wema na uzuri, na kuwa ndiyo kilele cha evolusheni, na kuwa ndiyo hatuwa yake kuu kabisa na ndiyo lengo ambalo wanadamu wahangaike kuliendeya, na kama hatulipi sifa ya umbile, basi twaweza kuepukana kabisa na itikadi za kibubusa. Kama tuonavyo, moja ya misingi mikuu ya falsafa ya Masoni ni kwamba vitu hutokana na maada na hurejeya tena katika maada. Muhimu katika mtazamo huu ni kuwa, Masoni hawaioni falsafa hii kama ipo kwa ajili yao tu; bali wanataka kusambaza mawaza haya katika jamii zote. Isindag anaendeleya;

Masoni aliyepata mafunzo kwa misingi ya itikadi hizi huikubali dhima ya kuelimisha watu... Na kuwaadilisha kwa kuwafundisha misingi ya hoja na sayansi yakinifu. Kwa utaratibu huwo, Masonri huenezwa kwa watu, hufanyakazi kwa niyaba ya watu licha ya watu wenyewe kuwepo. Maneno haya yanabainisha vipengele viwili vya jukumu la Masoni katika jamii:

Mosi, chini ya mwavuli wa Sayansi yakinifu na hoja, Masoni hujaribu kupandikiza katika jamii falsafa ya kilahidi ambayo ni dhana ya Misri ya kale. Pili, wanakusudiya kufanya hivi bila kujali watu. Yaani hata kama jamii inaamini Mungu na haina utashi wa kuikubali falsafa ya kilahidi, Masoni watakazana tu kufanya jitihada za kuubadili mtazamo wa watu juu ya ulimwengu bila ridhaa yao. Kuna jambo muhimu ambalo hatuna budi kulitiliya maanani hapa. Lugha ambayo Masoni huitumiya ni ya **ghiliba**. Katika maandiko yao hasa hasa yale yanayolengwa kwa watu wa jamii nyingine, huwa wanatumiya lugha inayokusudiya kuonesha kuwa falsafa yao haina ubaya, ni ya busara na stahamala.

Mfano wa hili waweza kuonekana katika nukuu ya hapo juu. Katika dhana ya kuwabadilisha watu kwa kuwafundisha misingi ya hoja na sayansi yakinifu. Kwa kweli falsafa ya Masoni haihusiyani kabisa na sayansi wala hoja. Yenyewe inahusiyana na dhana ya kale ambayo inavuma kwa sura ya sayansi. Si lengo la Masoni kuwaadilisha watu bali kusudiyo lao ni kupandikiza watu falsafa yao. Kwa kukamiya kwao kuwa watafanya hivyo hata bila ya ridhaa ya watu, tunaona kuwa wao si watu wenye stahamilivu. Ikiwa ni sehemu ya itikadi zao za kilahidi, Masoni wanakanusha kuwepo kwa roho na maisha baada ya kifo. Masoni hawaamini kuwepo kwa roho ya binadamu na wanapinga kabisa imani ya kuwepo kwa maisha mengine baada ya kifo.

## Kampeni dhidi ya dini Ujerumani: Masoni walimtumiya Bismarch kuupiga vita Ukatoliki

Miyaka 150 iliyopita, haikuwa na nchi iliyoitwa Ujerumani. Taifa linaloitwa Ujerumani hivi sasa lilitawaliwa na tawala (mamlaka) nyingi tu.

Mamlaka kubwa kabisa ilikuwa Prussia ambayo ilikaliya upande wa mashariki ya Ujerumani ya leo na sehemu kubwa ya Poland.

Katika miyaka ya 1860, Prussia ikaanza kukaliya majimbo mengine madogo madogo ya Ujerumani na kuanzisha dola ya Ujerumani mwaka 1871. Mtawala wa dola hii mpya alikuwa ni Waziri Mkuu wa Prussia na Kansela wa dola mpya ya Ujerumani, Otto von Bismarck.

Bismarck alikuwa mtawala aliyefanikiwa hasa katika siyasa za nje lakini hakupata mafanikio kama hayo katika siyasa za ndani.

Moja ya sababu ni kwamba kundi la wasomi lililojulikana kama "National Liberals" kama lilivyokuwa lile la Ufaransa dhidi ya ukasisi lilifuata sera ya kupiga vita dini.

Ili kufaulu kuleta umoja Ujermani National Liberals waliamini kuwa lilikuwa ni jambo la lazima kuwaondoshea watu hisiya za udugu nje ya mipaka yao na likaona kuwa uhusiyano baina ya theluthi moja ya umma na Papa wa Kikatoliki ulikuwa kizingiti kikubwa kwa jambo hilo.

Kwa kupata msukumo wa Nationa Liberals, Bismarck akaanzisha kampeni dhidi ya Ukatoliki zilizojulikana kama Kulturkampf au Culture war (vita vya kiutamaduni) pia kampeni hiyo ilielezwa kuwa ni mapambano ya kudhibiti bongo za wajerumani.

Wakati wa kampeni hiyo, wakatoliki, hasa hasa Ujerumani Mashariki walipata madhila. Mnamo mwaka 1872 kwa kutekeleza sheriya iliyokuwa imepitishwa, Makasisi wote nchini humo walizingirwa usiku mmoja na Taasisi zao zikataifishwa.

Kwa kufuata sheriya iliyoitwa, "May laws" (maigesetze) iliyopitishwa mwaka 1873, Makasisi wote waliokuwa wakifanya kazi serikalini, wakafukuzwa kazi, Kanisa likapigwa marufuku kujihusisha na maswala ya ndowa na elimu na mambo ya mahubiri yakawekewa mipaka. Maaskofu wengi wakuu wakatiwa mbaroni ambapo Makanisa 1300 yakabaki bila Kasisi hata mmoja.

Lakini kwa vile mbinu hizi zilizaa upinzani mkubwa miongoni mwa Wakatoliki nchini humo dhidi ya serikali kampeni za Kulturkampf zikalegeza uzi.

Bismarck akapuuziliya mbali maoni ya National Liberals waliokuwa wamemtumbukiza katika kampeni hiyo na akaimaliza kampeni hiyo kidogokidogo hadi pale ilipokwisha kabisa.

Kampeni yote hiyo haikuwa na kingine zaidi ya madhila kwa wakatoliki wa Ujermani. Wanahistoria wengi hivi leo wanaamini kuwa ilikuwa ni kampeni ambayo iliuwa mfumo wa usalama wa Ujermani.

Zaidi ya hivyo, baada ya Ujerman wimbi la Kampeni hiyo likaigubika Austria, Switzerland, Belgium na Holland, na kusababisha hofu kubwa katika nchi hizo.

Jambo muhimu la kukumbuka hapa ni kuwa walikuwa ni wasomi wa kimasoni ambao walimrubuni Bismarch hata kuingiya katika kampeni hiyo. Buku la Ensaiklopidia la Wakatoliki linasema hivi:

Lakini wao (Masoni), kwa kweli, wakaendeleza harakati ambapo kwa kampeni hizo Prussia hatuwa baada ya hatuwa likawa dola lililoshika uongozi wa Ujerumani, ikionwa kama ndio mwakilishi na mlinzi wa evolusheni mpya dhidi ya ubinafsi na unyang'anyi wa Papa.

Masoni piya ndio waliochocheya Kulturkampf (Vita dhidi ya dini) Mshauri mashuhuri wa maswala ya kisheriya ambaye ni Masoni, Grandmaster Bluntschli alikuwa mmoja wa wachochezi wakubwa katika vita hiyo dhidi ya dini.

Frimasoni wa Ujerumani wakafanya jitihada kutowa msukumo wa kushajiisha ushawishi wao kwa Taifa zima kufuwata misingi ya kimasoni na hivyo wao kudumisha kimya kimya kampeni yao ya kupiga vita dini.

Njiya kuu ambazo walitumiya ni maktaba za umma, mikutano, uhusiyano wa jumuiya na taasisi na kama ililazimu basi hata kuanzisha Taasisi mpya ambazo kupitiya kwazo ushawishi wa masoni ungepenya katika Taifa.

Hiyo ni kusema kuwa, licha ya ukweli kuwa Kulturkampf ilizuiwa rasmi na Bismarch, bado iliendelezwa na Masoni na kuwa vita endelevu dhidi ya dini katika jamii kwa ujumla.

Matunda machungu ya vita hivi yalivunwa katika miyaka ya 1920: Wanazi ambao walikusudia kulirejesha Taifa la Ujerumani katika ule upagani uliokuwepo kabla ya Ukristo kidogo kidogo wakapata nguvu na kuingiya madarakani mwaka 1933.

Moja ya mambo makubwa waliyoyafanya Manazi ni kuanzisha vita ya pili dhidi ya mamlaka ya kidini (au Kulturkampf ya pili).

Mchambuzi mmoja wa mambo wa Amerika Elbridge Colby anasema kuwa; "Manazi walianzisha vita mpya dhidi ya Kanisa Katoliki, wakawafunga jela makasisi, wakawatimuwa Maaskofu. Tofauti na mwaka 1874, Hitler alipinga hata Uprotestanti.

Kwa kifupi harakati zilizoanzishwa na Masoni kuitenga jamii mbali kabisa na dini zilizaa utawala katili mno wa kidikteta katika historiya, "Utawala wa Manazi" ambao uliitumbukiza duniya katika Vita ya Pili ya Duniya ambapo watu miliyoni 55 walipoteza maisha yao.

## Vita dhidi ya dini Italia

Nchi nyingine ambayo harakati za masoni zilidhihiri ni Italia. Hadi kufikiya mwaka 1870, Italia ilikuwa ikikaliwa na na dola kadhaa ndogo ndogo zikiwa ni masaaliya ya enzi za ukabaila. Kubwa kabisa miongoni mwa dola hizo ni Dola ya Papa.

Makao yake yalikuwa Roma iliyotawaliwa na Papa na kumiliki sehemu kubwa ya Italia. Masoni wa Italiya waligundulika kuwa ni mwendelezo wa Masoni wa Ufaransa ambapo walianza kuwa na ushawishi nchini Italia kuanziya mwanzoni mwa karne ya kumi na tisa.

Masoni hao walikuwa na niya ya kusambaratisha dola ya Papa na kuyang'owa kabisa mamlaka ya Kanisa katika nchi nzima ya Italia. Kwa mujibu wa mwandishi wa kitabu kiitwacho, *The Roman Catholic Church and the Craft*, Mdau wa Frimasonri:

"Nchini Italia chanzo cha harakati za Masoni, kwa kiyasi kikubwa, kilikuwa ni siyasa; zilichanganya Umasoni na vita dhidi ya mamlaka ya Papa.

Masoni walianza mapambano yao dhidi ya dini nchini Italia kwa kutumiya Jumuiya nyingine ya siri ambayo waliianzisha na kuimiliki. Jumuiya hii ilijulikana kama "Carbonari"

Jumuiya hii ambayo kwanza kabisa ilisikika Naple mwanzoni mwa karne ya kumi na tisa, ilichukuwa jina la wachoma mkaa.

Kama vile masoni walivyotumiya nembo ya uwashi-Wall-builder na kueneza mawazo yao kwa alama, ndivyo hivyo ilivyokuwa kwa Carbonari ambayo ilijipa nembo ya mchoma mkaa (Charcoal Burner).

Wakati kumbe Jumuiya hiyo ilikuwa na malengo yaliyojificha. Wadau wa Jumuiya hii walitaka tu kuanzisha programu ya kisiyasa kwanza nchini Italia halafu Ufaransa ili kuvunjiliya mbali nguvu ya Kanisa, kuanzisha serikali na kuzigeuza taasisi zote kuwa za kisekula.

Uhusiyano baina ya Frimasonri na Carbonari ukadhihirika. Ilitokeya kuwa Masoni wote wakawa wadau wa taasisi za Carbonari na pale walipoingiya tu katika jumuiya hiyo moja kwa moja wakapata digrii ya Masta (wakati ambapo kwa wadau wa kawaida wa Carbonari, iliwalazimu kupita hatuwa kwa hatuwa kwa muda mrefu kabla ya kupata digrii hii)

Mnamo Agosti 15, 1814 Makadinali wawili; Consalvi na Paca walitowa tamko kuwashutumu masoni na makabonari kuwa ndio waliopanga vurugu za kisiyasa na maasi ya mtutu wa bunduki kwa malengo ya kisiyasa na kwa uwaduwi dhidi ya dini.

Uwasi wa kutumiya silaha uliotokeya Macerata Juni 25, 1817, ulipangwa na Carbonari, lakini ukazimwa na majeshi ya usalama ya dola ya Papa.

Mnamo mwaka 1820 nchini Hispania na Naples na mnamo mwaka 1821 kule Piedmont, maasi ya kimapinduzi yalipangwa na Carbonari dhidi ya Kanisa na mfumo wa jamii.

Ni ukweli uliokubalika kuwa Carbonari iliasisiwa na Masoni ambao walishiriki katika harakati za mapinduzi. Baada ya mapinduzi ya Julai 1830 nchini Ufaransa jumuiya hii ikapoteza nguvu zake na kutoweka kidogo kidogo.

Nchini Italia jumuiya hii ikaungana na harakati za "Young Italy" zilizoanzishwa na Guiseppe Mazzini.

Mazzini ambaye alifahamika kuwa ni mpinzani wa dini alikuwa amepambana kwa miyaka mingi dhidi ya dola ya Papa na Kanisa na mwishowe akawa Masoni wa hadhi ya juu ambaye akaja kuwa mwasisi wa Muungano wa Italia.

Kwa kusadiwa na Masoni wawili mashuhuri, Guiseppe Garibaldi na Count di Cavour, Mazzini aliasisi Muungano wa Italia mwaka 1870, na akachora mipaka ya dola ya Papa ndani ya mipaka yake ya sasa.

Baada ya hapo Italia ikaingiya katika hatuwa ambapo ilizidi kusukumwa mbali kabisa na dini na hiyo ilikuwa ni kuandaa msingi wa udikteta wa Fashisti Mussolini katika miyaka ya 1920

Kwa kifupi tunaweza kusema kuwa Mazzini, Garibaldi na Cavour walikuwa ni viongozi watatu mashuhuri waliofanya kazi kubwa katika harakati dhidi ya dini barani Ulaya.

Siyo tu Mazzini alikuwa ni kiongozi wa kisiyasa katika mapambano dhidi ya dini bali alikuwa mwanaitikadi (wa kimasoni).

Kauli mbiu yake *"every nation a state"* ilikuwa cheche iliyowasha moto wa uwasi ambao ukawa chanzo cha kuanguka kwa dola za kienyeji kama vile Austro-Hugarian na dola ya Uthumaniya.

Kauli mbiu hii ya Mazzini iliwatenga watu mbali na hisiya za udugu wa kidini; ulikuwa ni mwito uliowatumbukiza katika mfarakano wa makabila.

Ule ukweli kuwa mwito huu ulitoka kwa Masoni wa ngazi ya juu ndio wa kuutiliya maanani hapa Kwa mujibu wa maelezo ya jarida la Masoni liitwalo 10,000 Famous Freemasons, Mazzini aliibuka kutoka ndani ya Jumuiya ya Masoni na miyaka mingi baadaye, mwaka 1867 akaja kuchaguliwa kuwa Masta Masoni wa Grand Orient ya Italia.

## Masoni walitaka kusambaratisha mamlaka ya Papa?

KATIKA baadhi ya maandiko yetu tumeelezeya mchango mkubwa uliotolewa na Masoni katika Mapinduzi ya Ufaransa. Idadi kubwa sana ya wanafalsafa wa Elimu hasa hasa wale wenye chuki na dini walikuwa Masoni. Wale walioandaa mazingira ya Mapinduzi na halafu kuwa vinara wake walikuwa wadau wa Masoni.

Mamluki mmoja katika mapinduzi hayo aliyejulikana kwa jina la Count Cagliostro alikiri namna Masoni walivyoshiriki katika mapinduzi hayo.

Mnamo mwaka 1789, Cagliostro alitiwa mbaroni na Mahakama ya Kanisa Katoliki (Inquisition) ambapo alifichuwa mambo muhimu wakati alipokuwa akihojiwa.

Alianza kwa kusema kuwa Masoni katika bara lote la Ulaya ndio waliokuwa wakipanga mfulululizo wa mapinduzi. Alisema kuwa shabaha kuu ya Masoni ilikuwa ni kusambaratisha au kuyanyakuwa mamlaka ya Papa.

Katika maelezo hayo ya kukiri, Cagliostro piya alikiri kuwa Mabenki ya Wayahudi yalisaidiya kifedha kufanikisha harakati za mapinduzi hayo, na ni pesa za Wayahudi zilizotowa mchango mkuwa katika Mapinduzi ya Ufaransa.

Kimsingi Mapinduzi ya Ufaransa yalikuwa ni mapinduzi dhidi ya dini. Ilikuwa ni juhudi ya dhati ya wanamapinduzi kuondosha ukasisi na lile lililokuwa tabaka la juu. Ndio maana Makasisi wengi waliuliwa, Taasisi za dini ziliteketezwa na nyumba za Ibada zikaangamizwa.

Wanamapinduzi hao walitaka hata kuuangamiza kabisa Ukristo wenyewe na badala yake kuweka itikadi ya kipagani waliyoiita "religiun of reason" (dini ya hoja au dini ya kutumiya akili). Lakini kwa muda mfupi tu wakapoteza udhibiti wa mapinduzi hayo na Ufaransa ikatumbukiya katika machafuko matupu.

Mkakati wa Masoni katika nchi hiyo haukuishiya katika mapinduzi. Machafuko yaliyotokeya kutokana na mapinduzi hayo hatimaye yakatulizwa pale Napoleon alipokamata madaraka.

Lakini utulivu huo nao haukudumu muda mrefu. Tamaa ya Napoleon ya kuitawala Ulaya yote ndiyo iliyoponza madaraka yake. Yalipoanguka madaraka ya Napoleon, mgogoro ukazidi kurindima Ufaransa kati ya watawala na wanamapinduzi.

Katika miyaka ya 1830, 1848 na 1871, mapinduzi matatu zaidi yakatokeya. Mnamo mwaka 1848, "Jamhuri ya Pili" ikaasisiwa; mwaka 1871, "Jamhuri ya Tatu ikaundwa.

Masoni walifanya pilika pilika kweli kweli katika kipindi chote hiki cha vurugu. Shabaha yao kuu ilikuwa ni kulidhoofisha Kanisa na taasisi zake, kuvuruga maadili ya dini na kufuta athari zake katika jamii pamoja na kufuta elimu ya dini. Masoni waliona kuwa kuupiga vita ukasisi, "anti-clericalism" ndiyo kitovu cha harakati zao za kijamii na kisiyasa.

Buku-rejeleo la Kikatoliki (Catholic Encyclopedia) linatowa maelezo muhimu kuhusu harakati za kupiga vita dini za Masoni nchini Ufaransa chini ya nembo ya Grand Orient ambalo ndilo jina lilitumiwa na shirika la frimansori kule Ufaransa.

Kutokana na nyaraka rasmi za shirika hilo la frimansori la Ufaransa ambazo, kwa kiyasi kikubwa, zilijumuisha taarifa rasmi za Grand Orient, imethibitika kuwa mikakati yote ya kupiga vita ukasisi iliyopitishwa katika Bunge la Ufaransa kwanza kabisa ilitangazwa katika shirika la Masoni na ikatekelezwa chini ya maelekezo ya Grand Orient ambayo lengo lake lilikuwa ni kudhibiti na kuendesha kila kitu na kila mtu nchini Ufaransa.

Ilibainishwa kuwa jukumu kubwa la Frimasonri ni kujiingiza katika harakati za kisiyasa. Kwamba mafanikio katika kupiga vita ukasisi kwa kiyasi kikubwa yalitokana na Frimasonri kwani ari, programu na mbinu za Masoni ndizo zilizoleta ushindi.

Spika wa Bunge hilo wa mwaka 1903 anasema, "Nilisema katika mkutano wa bunge wa 1898 kuwa ni wajibu wa Frimasonri kujiingiza katika harakati za kila siku za kisiyasa.

Mafanikiyo katika kuupiga vita ukasisi, kwa kiyasi kikubwa yanatokana na Frimasonri kwani ile ari yake, programu zake na mbinu zake ndizo zimeleta ushindi. Kama nguvu imeimarika basi hii ni kutokana na Frimasonri na mafunzo kutoka shirika hilo."

Anazidi kusema kuwa "tunahitaji umakini na moyo wa kujiamini kama tunataka kufanikisha kazi yetu kwani bado haijesha. Mnajuwa, kazi hii ya kupambana na ukasisi bado inaendeleya. Nchi lazima iondokane na mijumuiko ya kidini, kuifagiliya mbali kwa bakora ya nguvu."

Buku la Ensaiklopidiya la kikatoliki linazidi kutowa maelezo kuhusu mapambano ya Frimasonri dhidi ya dini nchini Ufaransa:

Kwa kweli mageuzi yote ya Masoni dhidi ya ukasisi yaliyofanyika Ufaransa tangu mwaka 1877, kama vike kuibadili elimu katika mfumo wa kisekula, harakati dhidi ya shule binafsi za Kikristo na taasisi za Hisani, kufutwa kwa taratibu za kidini ni matokeo ya harakati dhidi ya Ukristo na dhidi ya dini siyo tu Ufaransa bali duniyani kote.

Frimasonri ya Ufaransa ambayo ndiyo kinara inataka kuanzisha Jamhuri ya Kimasoni ulimwenguni, yenye undugu wa watu wote na mataifa yote.

Kiongozi mkuu wa Grand Orient (shirika la Frimasonri la Ufaransa), Seneta Delpech, mnamo mwezi Septemba, mwaka 1902 alisema, Ushindi wa Galilean umedumu kwa karne ishirini.

Lakini sasa ni zamu yake kufa...Kanisa la Roma lililoasisiwa kwa mkasa wa Galilean, lilianza kuharibikiwa pale Jumuiya ya Masoni ilipoanzishwa.

Kwa hili neno la “Galilean” (Galilaya) Masoni wana maana ya Yesu kwa sababu kwa mujibu wa Biblia, Yesu alizaliwa katika mji wa Galilii (Galilaya) Palestina. Kwa hiyo chuki ya Masoni dhidi ya Kanisa ni kielelezo cha chuki yao dhidi ya Yesu na dini ya Mungu mmoja.

Mwaka 1902, sheriya zilizopitishwa mfululizo nchini Ufaransa zilipanuwa wigo wa upinzani dhidi ya dini. Shule tatu za kidini zikafungwa na ikapigwa marufuku kufundisha elimu ya dini mashuleni.

Makasisi wengi wakakamatwa, baadhi yao wakafukuzwa nchini na watu waliofuata dini wakatazamwa kama raiya daraja la pili.

Kwasababu hii mnamo mwaka 1904, Vaticani ikavunja mahusiano yote ya kidiplomasiya na Ufaransa. Lakini hili halikubadili msimamo wa Ufaransa.

Maisha ya mamia kwa maelfu ya Wafaransa yalipotea katika vita ya kwanza ya dunia dhidi ya Jeshi la Ujerumani. Kabla ya jeuri ya nchi hiyo haijamalizwa na hapo ndipo ilipoanza tena kuona umuhimu wa mafundisho ya kiroho.

Kama linavyosema buku la Ensaklopidia la Kikatoliki, vita dhidi ya dini tokea mapinduzi ya Ufaransa hadi karne ya ishirini ilitekelezwa kwa mikakati ya kupiga vita ukasisi iliyopitishwa katika bunge la Ufaransa.

Mikakati hiyo ilikwishaandaliwa hapo kabla katika Jumuiya ya Mason na kutekelezwa kwa maelekezo ya Grand Orient (Jina la Jumuiya ya Mason ya Ufaransa.

Ukweli huu unathibitika katika maandiko ya Mason. Mathalani nukuu kutoka Jarida la Kituruki liitwalo *“A Speech Made by Brother Gambetta* la Julai 8 1875 inasema:

Wakati mzuka wa Jazba ulipotishiya Ufaransa, Itikadi ya dini na mawazo duni yakaingia katika vita dhidi ya kanuni na sheriya za kisasa za jamii miongoni mwa Taasisi zenye mtazamo wa mbali kama vile Frimansori iliyojitoleya kujenga misingi ya udugu, tunapata nguvu na faraja dhidi ya matakwa ya kukalifisha ya kanisa, maneno yake ya kashfa na mila zake zilizopindukia kiasi. Lazima tuwe imara na kuendelea na mapambano. Ili kuweza kuimarisha mfumo wa kibinadamu na kuleta maendeleo, tuvumiliye ili ngao zetu zisivunjike.

Itaonekana kuwa maandiko ya Masoni huyaelezea mawazo yao kama ni mawazo ya watu wanaoona mbali na huku wakiwaponda watu wa dini kuwa ni watu duni.

Hata hivyo huu ni mchezo wa maneno. Dhana ya mzuka wa jazba iliyotajwa katika nukuu ya hapo juu ni jambo ambalo watu wa dini wanalipinga lakini Masoni wanaitumiya kushambuliya dini katika jitihada za kuwatenga watu mbali nayo.

Zaidi ya hivyo lazima isisitizwe kuwa falsafa ya Kilahidi na Kihumanisti inayoungwa mkono na Masoni ni ya ushirikina mtupu, ni mfumo duni wa mawazo ni muendelezo wa mila za kipagani za Misri na Ugiriki ya kale.

Kwa sababu hiyo matumizi ya maneno kama vile mtazamo wa mbali na uduni yanayotumiwa na masoni hayana msingi wa ukweli.

Kusema kweli ni upuuzi mtupu kwa sababu ugomvi kati ya masoni na watu wa dini si mwingine bali ni uendelezo wa mgongano kati ya itikadi mbili ambazo zimekuwepo tangu zama za mwanzo kabisa za historiya.

Ni dini inayotangaza dhana ya kwanza kwamba ulimwengu uliumbwa kwa amri ya Mungu na kwamba wanadamu wanawajibika kumuabudiya yeye. Huu ndiyo ukweli.

Na dhana ya upinzani ni kwamba binadamu hawakuumbwa bali wanaishi maisha holela yasiyo na lengo ni dhana iliyotoka kwa wale wanaokanusha kuwepo kwa Mungu.

Pale inapoeleweka kwa usahihi basi ya weza kuonwa kuwa maneno haya ya uduni na mtazamo wa mbali hayana msingi. Kwa kuitumiya dhana ya maendeleo, Masoni wanataka kuibomowa dini. Ensayiklopidiya ya Katoliki inasema:

Zifuatazo ni njiya kuu za Frimansori:

(1) Kulisambaratisha kabisa kanisa kwa madhila ya wazi au kwa mfumo wa hadaa wa kutenganisha dola na kanisa. Kutenganisha nguvu za jamii na nguvu za dini, kupiga vita ukasisi na ikiwezekana kulisambaratisha kabisa kanisa.

(2) Kuweka mfumo wa kisekula ambao ni mfumo wa udanganyifu unaotenganisha maisha ya kidini na maisha ya kijamii. Na unaotenganisha elimu ya jamii. Maisha yasiyo na dini kama yanavyo fahamika kwa masoni ni vita dhidi ya ukatoliki na Ukristo. Uhuru wa mawazo na uhuru wa dini lazima ukuzwe kiufundi kwa watoto wa shule na ulindwe kwa kadri iwezekanavyo dhidi ya athari mbaya siyo tu za kanisa na makasisi bali pia hata za wazazi wa watoto hao.

Frimansori inaona kuwa hii ni njiya ya lazima na ya hakika ya kuweka jamuhuri ya ulimwengu.

Hapa inaonekana kuwa frimansori imeweka programu “kwa jina la ukombozi wa jamii” ambayo lengo lake ni kufutiliya mbali dini, program ambayo bado inatekelezwa hadi leo.

## Kampeni dhidi ya dini Ujerumani: Masoni walimtumiya Bismarch kuupiga vita Ukatoliki

MIYAKA 150 iliyopita, haikuwa na nchi iliyoitwa Ujerumani. Taifa linaloitwa Ujerumani hivi sasa lilitawaliwa na tawala (mamlaka) nyingi tu.

Mamlaka kubwa kabisa ilikuwa Prussia ambayo ilikaliya upande wa mashariki ya Ujerumani ya leo na sehemu kubwa ya Poland.

Katika miyaka ya 1860, Prussia ikaanza kukaliya majimbo mengine madogo madogo ya Ujerumani na kuanzisha dola ya Ujerumani mwaka 1871. Mtawala wa dola hii mpya alikuwa ni Waziri Mkuu wa Prussia na Kansela wa dola mpya ya Ujerumani, Otto von Bismarck.

Bismarck alikuwa mtawala aliyefanikiwa hasa katika siyasa za nje lakini hakupata mafanikio kama hayo katika siyasa za ndani.

Moja ya sababu ni kwamba kundi la wasomi lililojulikana kama “National Liberals” kama lilivyokuwa lile la Ufaransa dhidi ya ukasisi lilifuata sera ya kupiga vita dini.

Ili kufaulu kuleta umoja Ujermani National Liberals waliamini kuwa lilikuwa ni jambo la lazima kuwaondoshea watu hisiya za udugu nje ya mipaka yao na likaona kuwa uhusiyano baina ya theluthi moja ya umma na Papa wa Kikatoliki ulikuwa kizingiti kikubwa kwa jambo hilo.

Kwa kupata msukumo wa Nationa Liberals, Bismarck akaanzisha kampeni dhidi ya Ukatoliki zilizojulikana kama Kulturkampf au Culture war (vita vya kiutamaduni) pia kampeni hiyo ilielezwa kuwa ni mapambano ya kudhibiti bongo za wajerumani.

Wakati wa kampeni hiyo, wakatoliki, hasa hasa Ujerumani Mashariki walipata madhila. Mnamo mwaka 1872 kwa kutekeleza sheriya iliyokuwa imepitishwa, Makasisi wote nchini humo walizingirwa usiku mmoja na Taasisi zao zikataifishwa.

Kwa kufuata sheriya iliyoitwa, “May laws” (maigesetze) iliyopitishwa mwaka 1873, Makasisi wote waliokuwa wakifanya kazi serikalini, wakafukuzwa kazi, Kanisa likapigwa marufuku kujihusisha na maswala ya ndowa na elimu na mambo ya mahubiri yakawekewa mipaka. Maaskofu wengi wakuu wakatiwa mbaroni ambapo Makanisa 1300 yakabaki bila Kasisi hata mmoja.

Lakini kwa vile mbinu hizi zilizaa upinzani mkubwa miongoni mwa Wakatoliki nchini humo dhidi ya serikali kampeni za Kulturkampf zikalegeza uzi.

Bismarck akapuuziliya mbali maoni ya National Liberals waliokuwa wamemtumbukiza katika kampeni hiyo na akaimaliza kampeni hiyo kidogokidogo hadi pale ilipokwisha kabisa.

Kampeni yote hiyo haikuwa na kingine zaidi ya madhila kwa wakatoliki wa Ujermani. Wanahistoria wengi hivi leo wanaamini kuwa ilikuwa ni kampeni ambayo iliuwa mfumo wa usalama wa Ujermani.

Zaidi ya hivyo, baada ya Ujerman wimbi la Kampeni hiyo likaigubika Austria, Switzerland, Belgium na Holland, na kusababisha hofu kubwa katika nchi hizo.

Jambo muhimu la kukumbuka hapa ni kuwa walikuwa ni wasomi wa kimasoni ambao walimrubuni Bismarch hata kuingiya katika kampeni hiyo. Buku la Ensaiklopidia la Wakatoliki linasema hivi:

Lakini wao (Masoni), kwa kweli, wakaendeleza harakati ambapo kwa kampeni hizo Prussia hatuwa baada ya hatuwa likawa dola lililoshika uongozi wa Ujerumani, ikionwa kama ndio mwakilishi na mlinzi wa evolusheni mpya dhidi ya ubinafsi na unyang’anyi wa Papa.

Masoni piya ndio waliochocheya Kulturkampf (Vita dhidi ya dini) Mshauri mashuhuri wa maswala ya kisheriya ambaye ni Masoni, Grandmaster Bluntschli alikuwa mmoja wa wachochezi wakubwa katika vita hiyo dhidi ya dini.

Frimasoni wa Ujerumani wakafanya jitihada kutowa msukumo wa kushajiisha ushawishi wao kwa Taifa zima kufuwata misingi ya kimasoni na hivyo wao kudumisha kimya kimya kampeni yao ya kupiga vita dini.

Njiya kuu ambazo walitumiya ni maktaba za umma, mikutano, uhusiyano wa jumuiya na taasisi na kama ililazimu basi hata kuanzisha Taasisi mpya ambazo kupitiya kwazo ushawishi wa masoni ungepenya katika Taifa.

Hiyo ni kusema kuwa, licha ya ukweli kuwa Kulturkampf ilizuiwa rasmi na Bismarch, bado iliendelezwa na Masoni na kuwa vita endelevu dhidi ya dini katika jamii kwa ujumla.

Matunda machungu ya vita hivi yalivunwa katika miyaka ya 1920: Wanazi ambao walikusudia kulirejesha Taifa la Ujerumani katika ule upagani uliokuwepo kabla ya Ukristo kidogo kidogo wakapata nguvu na kuingiya madarakani mwaka 1933.

Moja ya mambo makubwa waliyoyafanya Manazi ni kuanzisha vita ya pili dhidi ya mamlaka ya kidini (au Kulturkampf ya pili).

Mchambuzi mmoja wa mambo wa Amerika Elbridge Colby anasema kuwa; “Manazi walianzisha vita mpya dhidi ya Kanisa Katoliki, wakawafunga jela makasisi, wakawatimuwa Maaskofu. Tofauti na mwaka 1874, Hitler alipinga hata Uprotestanti.

Kwa kifupi harakati zilizoanzishwa na Masoni kuitenga jamii mbali kabisa na dini zilizaa utawala katili mno wa kidikteta katika historiya, “Utawala wa Manazi” ambao uliitumbukiza duniya katika Vita ya Pili ya Duniya ambapo watu miliyoni 55 walipoteza maisha yao.

## Vita dhidi ya dini Uingereza

Tangazo rasmi la kuwepo kwa Masonri nchini Uingereza lilitolewa mwaka 1717. Kabla ya tarehe hiyo, Masonri ilikuwa imeshaeneya Uingereza, halafu Ufaransa na kisha sehemu nyingine za Ulaya,

Kimsingi Ulaya ndiyo eneo la kwanza walilokutaniya wapinzani wa dini. Masoni wengi walikuwa wakikutana katika maskani zao wakijinadi kuwa wao ni “wanafikra huru” wakiwa na maana kuwa hawakuwa wakiitambuwa dini ya Mungu.

Makala moja iliyopewa kichwa “The First Periods of Masonry” iliyochapishwa katika Jarida la Mimar Sinan inasema hivi; “Mahali ambapo Masoni walijikusanya kutafuta ukweli nje ya makanisa pakawa hifadhi.

Kundi hili lililotafuta ukweli nje ya dini piya lilijenga chuki kubwa dhidi ya dini. Kwa sababu hii Jumuiya hiyo ikawa kitovu cha ile nguvu iliyolinyima raha Kanisa hasa hasa Kanisa Katoliki.

Vita kati ya Masonri na Kanisa vikazidi kupamba moto na vikaacha alama katika bara la Ulaya katika karne za kumi na nane na kumi na tisa. Masonri ikaanza kujitanuwa katika nchi nyingine nje ya Ulaya.

Katika nngwe ya pili ya karne ya kumi na tisa, kila ilikojitandaza, ikawa kitovu cha mapambano dhidi ya falsafa na harakati za kidini. Makala iliyopewa anuwani “Politics and

Freemasonry” iliyotoka katika Jarida la Mimar Sinan linaeleza yafuwatayo kuhusiyana na mapambano dhidi ya dini:

Pamoja na kutokuwa chama cha siyasa, Frimasonri iliimarika mwanzoni mwa karne ya kumi na tisa na kuwa taasisi ya kijamii kwa upeo wa kimataifa ikijihusisha na matukio ya kisiyasa na kijamii.

Ili kuyasaidiya madhehebu katika jitihada zao za kutumiya uhuru wa kidini, Frimasonri ikajiingiza katika mapambano dhidi ya mamlaka na nguvu za ukasisi ikijaribu kufanikisha shabaha yao ya kuangusha mamlaka ya Kanisa.

Kwa sababu hiyo mnamo mwaka 1738 na mwaka 1751, Jumuiya hii ilitangazwa na Papa kuwa inampinga Mungu.

Katika zile nchi zilizofuwata misingi ya uhuru wa dini, Frimasonri ilikuwa ni jumuiya ya siri siri ikijulikana kwa jina tu. Katika nchi hizi Masonri ilipuuziwa tu na kupata wanachama miongoni mwa viyongozi wa ngazi ya kati na wa ngazi za juu ambao walikuwa na muda na wasaa na ikawaweka viyongozi wa dola katika nyadhifa za uwongozi wa jumuiya zake.

Katika nchi za kusini ambako kila mtu alilazimika kuwa mkatoliki, waliendeleya na mwenendo wao kama shirika la siri, la kimapinduzi lililopaswa kudhibitiwa kisheriya.

Katika nchi hizi vijana wenye fikra huru na Maafisa waliokuwa hawaridhiki na serikali wakaanza kuingiya katika maskani za Masoni na ndipo mipango ya mapinduzi ikaanzishwa na kuzilenga tawala za Hispania, Ureno na Italia ambazo zilikuwa chini ya utawala wa Vatikani.”

Hapana shaka kuwa hapa mwandishi wa kimasoni anatumiya lugha ya kulipendeleya shirika lake pale anaposema kwa Masonri inapigana vita dhidi ya utawala wa Kanisa.

Lakini pale tunapoangaliya jambo hili kwa makini zaidi, tunaona kuwa katika nchi nyingi “utawala” huwo huwo ukaonekana unafaa kwa tawala zilizoanzishwa au kuungwa mkono na Masoni. Twaweza kutambuwa kirahisi tu kuwa dai la Masoni la kupiga vita “utawala” ni kisingizio tu.

Licha ya ukweli kuwa Kanisa-kwa vile Ukristo wenyewe ulikuwa umeshaharibiwa-lilizuia mawazo ya kisomi na kufanya matendo ya ukandamizaji lakini uwaduwi wa Masoni dhidi ya Kanisa haukutokana na hili bali ulitokana na chuki dhidi ya dini zilizoamini Mungu.

Yafaa tuuangaliye muundo wa Masonri na ibada zake ili kulielewa jambo hili.

## Mfano wa Maskani ya Masoni

Ili kufahamu jinsi masonri ya karne ya kumi na nane ilivyoanza, na kuelewa kile ilichotaka kukitimiza, moja ya mambo tunayolazimika kuyafanya ni kuziangaliya jumuiya mbali mbali za siri za kimasoni zilizoibuka katika kipindi hicho.

Moja ya jumuiya hizo ilikuwa “Hell-Fire Club” ambayo ilikuwa ikifanya kazi Uingereza katikati ya karne ya kumi na nane. Mfumo wa Kimasoni wa jumuiya hii na mwenendo wake wa kipagani uliopingana na dini unaelezewa na Mwandishi wa kimasoni Daniel Willens katika makala yake, “The Hell-Fire Club: Sex, Politics and Religion in Eighteenth-Century in England”. Zifuwatazo ni baadhi ya ibara muhimu kutoka katika makala hayo yaliyochapishwa katika Jarida la Gnosis:

Katika usiku wa mbalamwezi wakati wa utawala wa King George III (Mfalme George wa Tatu) wa Uingereza wadau waliokuwa na mamlaka makubwa katika serikali yake, wasomi wakubwa, wasanii mashuhuri kuna nyakati walikuwa wakionekana kusafiri kuelekeya juu Mto Thames kupitiya gondola hadi abbey jirani na Wycombe.

Huko walivaa majoho ya kitawa na kufanya kila jambo baya, ambapo walikuwa wakiishiya na misa iliyokuwa ikifanywa juu ya mwili wa mwanamke mtakatifu uliokuwa uchi wa mnyama na misa hiyo iliongozwa na Francis Dashwood. Ibada yao ya kishetani ilipokwisha, duru za ndani zilikuwa zikipanga muwelekeo wa Utawala wa Uingereza.

Kulikuwa na uchunguzi mwingi wa harakati za siri za Jumuiya hii na mnamo mwaka 1765, Charles Johnstone alichapisha makala iliyokuwa na kichwa, Chrysal, or the Adventures of a Guinea ambayo ilisadikiwa kufichuwa siri za watawa hao wa Medmenham japo wenyewe walijulikana kwa jina la “The Hell-Fire Club.”

“Utambulisho muhimu wa watawa hawa ni Hell-Fire Club” iliyoanzishwa mjini London mnamo mwaka 1719 ambapo mwasisi wake alikuwa Philip, mtawala wa Wharton (1698-1731).

Wharton alikuwa mwanasiyasa, Frimasoni na Muathesti mashuhuri aliyekuwa akidharau dini...na Wharton akaja kuwa Masta Masoni Mkuu wa Jumuiya ya Masoni ya Uingereza mnamo mwaka 1722. Mnamo mwaka 1739, Dashwood alikuwa safirini.

Alipokuwa njiyani, alisimama Florence kumuona Abbe Nicolini na hapa ndipo alipokutana na Lady Mary Wortley Montagu... ambaye hatimaye akajiunga na Dashwood katika Divan Club... Kwa bahati mbaya mambo hayakuiendeya vyema Frimasonri nchini Italia.

Papa Clement wa Kumi na mbili (Pope Clement XII) masiku machache tu nyuma alikuwa ametangaza amri (the bull) ya kuondowa hukumu dhidi ya Jumuiya za Masoni.

Mwanzoni mwa mwaka 1740 Papa akafa na Dashwood akaenda Roma kwa ajili ya mkutano wa kumchaguwa Papa mpya. Alipokuwa huko, kwa kebehi alijifanya yeye ndiye Kadinali Ottiboni, mmoja wa watesaji wakuu wa Masoni na akamkejeli hadharani katika ibada ya iliyojaa matusi (kashifa).

“Chapter-room” ndiyo jambo muhimu la kufahamiya harakati za Watawa. Maelezo juu ya Chapter-room hayafahamiki na kwa hali hiyo matumizi ambayo kwayo chapter-room iliwekwa yanabakiya kuwa kitendawili.

Waandishi wa udaku wanadai kuwa palikuwa ni mahala pa ibada za kishetani, japokuwa inafaa zaidi kuhitimisha kuwa ilikuwa ikitumika kwa shughuli za kimasoni.

John Wilkes, mdau muhimu wa duru za Medmenham ameandika hivi katika makala yake; “hakuna jicho lisilohusika lililoweza kupenya ndani ya Chapter-room kuona siri ambapo watawa walikuwa wakikusanyika nyakati zote, ibada za siri sana zilikuwa zikifanyika .

Mmoja wa Mahasimu wa kisiyasa wa Dashwood Bw. Horace aliwahi kubeza hivi: Vyovyote zilivyokuwa itikadi zao, mila yao ilikuwa ya kipagani kabisa: Bacchus na Venus ndio waliokuwa miungu wao ambao waliwatoleya mihanga hadharani.

Uwanachama wa Watawa wa Medmenham haupo tena hivi leo. Majina ya watu waliojihusisha nayo ni Nduguye Dashwood; Dashwood-King; John Montagu; John Wilkes;

George Bubb Dodington; Baron Melcombe; Paul Whitehead na watu wengine wa kawaida na wasomi.... Yaelekeya kuwa “Chapter-room” lilikuwa ni hekalu la Masoni.

Sababu ya kuichukuwa nukuu hii ndefu ni kupata ile dhana nzima ya mazingira ambamo Masonri ya karne ya kumi na nane ilivyozidi kuendeleya na ushawishi wake kwa watu.

Masonri ilijitokeza kama jumuiya ya siri yenye mvuto ambayo upinzani wake dhidi ya imani zote za jamii ulikuwa na aina fulani ya pumbazo la kisaikolojoiya kwa wadau wake.

Sifa ya msingi ya ibada za Masoni kama ilivyoelezwa hapo juu ilikuwa ni kutukuza alama na imani za kipagani badala ya dini zilizoamini Mungu.

Kwa hiyo wale walioupa mgongo Ukristo na kuwa Masoni wakawa wapagani japo si lazima kuwa waukubali upagani kama itikadi ila angalau wafuwate tu alama zake.

Pamoja na hivyo Masoni hawakutosheka tu kufuwata mila za ajabu bali walitekeleza mkakati uliolenga kuitenga Ulaya mbali na dini zilizoamini Mungu na kuitumbukiza katika upagani.

Katika matoleo mawili yaliyopita ya gazeti hili tuliona vita vilivyoendeshwa na Masoni dhidi ya dini katika nchi za Ulaya. Na nchi ya Kwanza ilikuwa Ufaransa ambayo mapinduzi yake yalichangiwa na Masoni.